**23 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 23 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**23 JUNI, 2025**

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 648

### Msaada wa Kisaikolojia kwa Watu Wenye Ulemavu

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati upi katika kusimamia na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Patrobas Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia na kutoa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Sura 183, kama ifuatavyo: -

(1) Utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisaikolojia wa Mwaka 2020; na

(2) Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma wa msaada wa kisaikolojia ili kutoa huduma hiyo kwa ufanisi na ubora hitajika kwa watu wenye ulemavu. Watoa huduma hao ni pamoja na Maafisa

Ustawi wa Jamii, Wataalamu wa Saikolojia, Wauguzi, Madaktari na Walimu wa Elimu wa Shule za Msingi na Sekondari, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Je, ni kwa namna gani Serikali inaweza kuwashirikisha wanafamilia katika elimu hii ya saikolojia, kwa kuwa, wao ndio wanaowalea kwa muda mrefu watu hawa wenye ulemavu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali inawafikia wanafunzi wenye ulemavu katika Shule za Msingi na Sekondari ili kuweza kuwapatia huduma hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba, katika upande wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu, pia tumeanza utaratibu huo wa kutumia mwongozo ule wa Kitaifa wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa watu wenye ulemavu. Mwongozo huu ni wa mwaka 2020 na umekuwa ukitumika hasa kwenye hayo maeneo na hata katika upande ambao siyo wa shule.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, kuhusiana na familia, ni kwamba katika maeneo ambayo Maafisa wa Ustawi wa Jamii wanahusika zaidi kwanza, katika kufanya utambuzi wa mapema wa watu wenye ulemavu, na tuna mwongozo mahususi unaohusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ni kwenye halmashauri zote. Wale Maafisa Ustawi wanaenda kwenye maeneo ya familia kulingana na taarifa ambazo zinatolewa, na tunaanza kufanyia kazi na kuyachakata hayo. Kwa hiyo, watu wenye ulemavu ambao wana changamoto za kisaikolojia walio shuleni wanapata huduma hiyo kulingana na mwongozo ambao tunao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili, wale ambao wapo nje ya mfumo wa elimu wanaokutwa huko, pamoja na wataalam wetu, hasa Maafisa Maendeleo ya Jamii, kwenye taasisi za madawati ya jinsia na wataalam, madaktari, wamepewa mafunzo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ni namna gani kuweza ku-*handle* hizi *issues* zinazoleta changamoto kwa watu wenye ulemavu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, suala la saikolojia ni la kitaalam, na kwenye halmashauri, hatuna wataalam wa saikolojia. Ni lini Serikali sasa mtaona umuhimu wa kuajiri watu wa saikolojia kwa ajili ya watu wenye ulemavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, hawa Maafisa Ustawi na Maendeleo ya Jamii waliopo katika masomo yao, saikolojia ni moja ya somo, lakini pia, walimu katika vyuo mbalimbali vya ualimu wa ngazi ya shule za msingi na sekondari na pia, walimu wa vyuo vikuu saikolojia ni moja ya somo muhimu.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo, wapo ambao wamesoma masuala ya *sociology,* ambao tunawatumia kama Serikali, kuweza kufanya taratibu hizo za *counselling*. Tunao hao ma-*psychosocial* kwenye maeneo mbalimbali ambao tunawatumia. Pia, ninalichukua kama eneo lingine la nyongeza la muhimu katika Serikali kuweza kuangalia ni namna gani tunaweza tukaboresha zaidi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

Na. 649

**Ukarabati wa Barabara ya Igalako – Mapala, Mbarali**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kukarabati Barabara ya Igalako – Mwatenga hadi Mapala Mbarali?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Igalako – Mwatenga – Mapala yenye urefu wa kilometa 15. Barabara hiyo ni kiunganishi muhimu kwa wananchi wa Kata ya Mwatenga na Mahongole katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilifanya matengenezo ya barabara hiyo, ambapo shilingi milioni 50 zilitumika na kuwezesha ukarabati wa kilomita mbili za barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, katika mkakati wa haraka wa kukarabati Barabara ya Igalako – Mwatenga hadi Mapala, Mbarali, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 325.5 kwa ajili ya ukarabati huo. Jumla ya kilomita 9.3 zitafanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe. Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja ya Wilaya ya Mbarali kwa kujenga, kukarabati na kuifanyia matengenezo mara kwa mara kadiri ya uhitaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, 90% ya Barabara za Wilaya ya Mbarali zinaelekea kwenye mashamba makubwa.

Kutokana na shughuli kubwa za uchumi, barabara hizi kila mwaka zimekuwa zikiharibika na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali. Hamuoni haja sasa barabara zenye shughuli nyingi za kilimo kuanza kufikiria kuzitengea bajeti ya kuanzia kilometa chache, ili ziwe za kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wilaya ya Rungwe, Tukuyu Mjini, kuna barabara ambayo ni ya muhimu sana inayounganisha kata tatu. Barabara hiyo ni ya Kata ya Bagamoyo, Ibigi na Buliyaga, ambayo inaitwa Mafurasopo – Soko Mjinga kutokea Katumba, kilometa mbili na nusu. Sasa, je, ni lini Serikali itaanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ili wananchi wa Wilaya ya Rungwe waweze kupona kulingana na barabara hiyo ilivyo muhimu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ni moja ya halmashauri zenye shughuli nyingi za kiuchumi, hususan kilimo cha mpunga, na kwa hiyo, barabara zile zinakwenda kwenye mashamba makubwa ambayo magari yenye uzito mkubwa huenda kuchukua bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeongeza sana Bajeti ya *TARURA* kwa Halmashauri ya Mbarali kwa zaidi ya mara tano ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021 mpaka sasa 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeendelea kuchukua hatua. Siku za nyuma barabara zile zilikuwa zinalimwa kwa hatua ya udongo, lakini sasa zote zinalimwa kwa hatua ya changarawe.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba, tungependa kuwa na barabara za lami, lakini safari ni hatua, tunakwenda kwa awamu kadiri ya bajeti zetu. Kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha tutaendelea kutenga kwa ajili ya kuendelea kujenga barabara hizo kwa

changarawe na huko mbele tutaona uwezekano wa kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Barabara ya Bagamoyo – Buliyaga katika Halmashauri ya Rungwe, ni kweli ni barabara muhimu na inaunganisha kata kadhaa kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Nakuhakikishia Mheshimiwa Fyandomo kwamba, Serikali hii itaendelea kutenga bajeti kwa awamu kuhakikisha kwamba, barabara hiyo inalimwa kwa kiwango cha changarawe, lakini kadiri ya bajeti inavyozidi kwenda, tutafanya tathmini na kuona uwezekano wa kuanza kwa awamu barabara hizo kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Jimbo la Busokelo, hususan kuanzia Ruangwa – Itete – Kilugu – Kibole – Segese, ni lango muhimu la kuunganisha Kata ya Jimbo la Busokelo na Kyela. Barabara hii imekatika na hivi sasa ninavyosema hakuna mawasiliano kati ya hizi kata zote. Je, ni mpango gani wa dharura wa Serikali kwa ukarabati barabara hii, ili wananchi waendelee na shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika kila bajeti, Serikali inaweka fungu kwa ajili ya matengenezo ya dharura na katika huu mwaka wa fedha 2024/2025 tuna fungu la matengenezo ya dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Rungwe waende mara moja wakafanye tathmini maeneo korofi ambayo yamesababisha barabara hii kutopitika kabisa, tuweze kuona namna ya kupata fedha mapema iwezekanavyo kufanya matengenezo katika barabara hiyo, ili wananchi wa Jimbo la Busokelo na Jimbo la

Kyela waendelee kuwa na mawasilino na shughuli za kiuchumi na kijamii ziendelee kama kawaida. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 650

**Ujenzi wa Daraja la Sambu, Kata ya Masagalu**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Sambu katika Kata ya Masagalu - Kilindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza azma ya ujenzi wa Daraja la Sambu, inakusudia kufanya usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutumia wataalam wa ndani wa *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kukamilisha usanifu huo, na gharama halisi za mradi kujulikana, Serikali itatafuta fedha ili kuwezesha utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Sambu. Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja ya Wilaya ya Kilindi kwa kujenga, kukarabati na kuifanyia matengenezo kwa awamu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, kwenye mwaka 2025 watafanya usanifu kwa ajili ya madaraja hayo. Je, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya usanifu wa daraja hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, kuna Daraja la Kata ya Kisangasa kwenye Kijiji kile cha Mgela ambapo na Taasisi za Serikali, kwa maana ya Mahakama, shule za msingi na sekondari, mkandarasi hayuko *site*. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, mkandarasi huyo anakwenda *site* na kuanza ujenzi wa daraja hilo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika mwaka wa fedha ujao 2025/2026 Serikali kwa kutambua umuhimu wa Daraja la Sambu imetenga fedha kwa ajili ya kwenda kufanya usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya *figure,* ninaomba muda, nitafutilia na kumpa jibu Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua kwamba, kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya usanifu wa kina wa Daraja la Sambu na tutakwenda kutekeleza katika mwaka wa fedha ujao, 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusiana na daraja, ni kweli kwamba, Serikali ilipeleka mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo, lakini tunafahamu kwamba, mkandarasi hayupo *site*. Ninaomba nitumie nafasi hii kwanza nimwelekeze Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Kilindi na Mkoa wa Tanga waende kukutana na mkandarasi husika waweze kuona changamoto ni nini, ili tuweze kuitatua mapema iwezekanavyo na Mkandarasi arejee *site* kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, huduma muhimu kwa wananchi ziweze kurejea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Nkwenda na Songambele zinaunganishwa na Kijiji cha Migina ambacho kuna eneo linaitwa Bwema. Eneo hilo yanapita maji na kwa muda mrefu limekuwa halina miundombinu ya daraja kubwa la kupitisha maji. Ninataka kujua mkakati wa Serikali kupitia *TARURA,*

kuwajengea wananchi hilo daraja, ili kuunganisha hizi kata mbili za Nkwenda na Songambele. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, moja ya mkakati wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kutambua maeneo yote korofi ambayo yanakwamisha shughuli za usafiri, zikiwemo barabara muhimu, madaraja, makalavati na kutenga bajeti kwa awamu kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Theonest kwamba, tutakwenda kulifanyia kazi eneo hilo la daraja ambalo linaunganisha Kata ya Nkwenda na Songambele, ili tuweze kujua kwanza ni kiasi gani cha fedha kinahitajika, kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kagera pamoja na wa Wilaya ya Kyerwa waende wakafanye tathmini na kuleta ripoti rasmi Ofisi ya Rais, TAMISEMI juu ya mahitaji ya gharama, kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, ili tuweze kuona namna ya kuanza kutenga fedha kwenye bajeti tuweze kujenga daraja hilo na kuboresha huduma za usafiri kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kasikazini, sasa aulize swali lake.

Na. 651

**Utaratibu wa Kugawa Miradi ya Kimkakati Nchini**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, ni utaratibu gani unatumika kugawa miradi ya kimkakati katika maeneo mbalimbali nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa ruzuku ya miradi ya kimkakati katika halmashauri kwa lengo la kuziwezesha kujitegemea kimapato, kupitia utekelezaji wa miradi ya kuzalisha mapato. Fedha hizo hutolewa kwa Halmashauri inayokidhi vigezo vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Miradi ya Kimkakati wa Mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo ni pamoja na halmashauri kuwa na andiko linalokidhi vigezo vya uwekezaji, kuwa na fursa za kimapato zenye kuhitaji msukumo wa Serikali Kuu na uwekezaji mkubwa. Kuwa na umiliki halali wa eneo, miradi kubainika kuwa na viashiria vya uhimilivu wa mradi baada ya kuchambuliwa, halmashauri kuwa na mkakati wa kujitegemea, mradi kuwa kwenye bajeti pamoja na halmashauri kuwa na hati safi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nimeyasikia majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, wanaopashwa kuandika maandiko wanatoka kwenye halmashauri na wanatofautiana uwezo, kwa sasa tuna Wizara inayohusika na mipango na uwekezaji. Serikali haioni kuna haja sasa, ili kuweka usawa kwenye halmashauri zote, kupata miradi ya kimkakati Wizara hiyo inayohusika na mipango ikabeba jukumu hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Vigezo alivyovitaja, Halmashauri ya Nkasi, tayari tumekidhi kwa ajili ya kujenga stendi na soko. Je, Serikali mpo tayari kutujengea katika Mji wa Namanyere? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli

kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Aida Khenani, kwamba sasa tuna Wizara mahsusi kabisa ya Mipango na Uwekezaji ambayo inaratibu shughuli zote za mipango na uwekezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi Ofisi ya Rais,TAMISEMI tunashirikiana kwa karibu na Wizara ya Mipango na Uwezekezaji, na sasa tunaendelea kuratibu kupitia Wizara hiyo, miradi yote ya kimkakati katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hiyo ndiyo kinara ambayo inafanya *mapping* ya miradi yote katika nchi nzima, katika halmashauri zote na kuifanyia tathmini kama inakidhi vigezo na baadaye kuifanyia uchambuzi na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara hiyo ndiyo ambayo inashika jukumu hilo na tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na picha ya ujumla ya miradi katika nchi nzima ambayo inakidhi vigezo kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili, Halmashauri ya Nkasi iliwasilisha maombi ya mradi wa kimkakati wa stendi katika Mji wa Namanyele, pamoja na soko, na uchambuzi unaendelea. Tunaamini kama itakidhi vigezo ambavyo vimeainishwa, tutahakikisha kwamba tunaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi huo kwa mapato ya ndani, lakini pia kwa fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hilo limepokelewa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaendelea kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa matamko kila wakati hapa Bungeni, kwamba miradi iliyotolewa, ahadi za viongozi wakuu wa Serikali inapewa kipaumbele katika utekelezaji, je, sasa Serikali inatoa kauli

gani kwa miradi kama hiyo ambayo haijatekelezwa, kama ule wa Barabara ya Bofo – Mandaka – Kilema kule Vunjo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Dkt. Charles Kimei kwamba, kama ambavyo Serikali imekuwa ikitoa ufafanuzi hapa Bungeni, kwamba maelekezo na ahadi za viongozi wa Kitaifa ni kipaumbele namba moja katika mipango yetu, utekelezaji wake umekuwa ukifanyika kila mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, viko vituo vya afya ambavyo ni ahadi za viongozi wa Kitaifa, zaidi ya 90% ya ahadi hizo zimetekelezwa kwa kupeleka fedha, vituo vya afya vimejengwa, zahanati zimejengwa, hospitali zimejengwa, barabara zinaendelea kujengwa. Kwa hiyo, katika kila bajeti, moja ya kipaumbele cha juu kabisa ni ahadi za viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, hatuwezi kumaliza siku moja katika mwaka mmoja wa fedha, tunakwenda kwa awamu. Nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kimei kwamba, hata huo mradi alioutaja ambao ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, tutakwenda kuufanyia kazi kwa sababu ni moja ya vipaumbele vya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 652

**Kuigawa Halmashauri la Wilaya ya Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili kurahisisha shughuli za kiutawala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, halmashauri huanzishwa au kupandishwa hadhi kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mwongozo, uanzishaji wa halmashauri mpya huanza na kusudio ambalo hupaswa kujadiliwa katika vikao vya ngazi za vijiji/mitaa, kata, Halmashauri, Wilaya na Mkoa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Katibu Tawala wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa kugawa baadhi ya maeneo mapya ya utawala, lakini kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Wilaya yetu ya Kilwa ina ukubwa unaozidi Mkoa mzima wa Dar es Salaam na Mkoa mzima wa Kilimanjaro, je, Serikali ina mkakati gani katika vipaumbele ilivyoviweka katika kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini katika Kata saba za Kinjumbi, Mingumbi, Chumo, Namayuni, Kipatimu, pamoja na Kandawale?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Wilaya yetu ya Kilwa ina mtawanyiko mkubwa kiasi kwamba baadhi ya kata zinapatikana umbali wa zaidi ya kilometa 200 kutoka makao makuu ya wilaya, Kata kama za Kandawale, Kibata, Likawage, na Nanjilinji, je, Serikali haioni kuna haja kwa kata kama hizi ambazo zinapatikana umbali mrefu

kutoka makao makuu kutengewa utaratibu maalumu wa upendeleo ili kuzisukuma mbele kimaendeleo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika kutenga bajeti kwa ajili ya miundombinu ya barabara kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini *(TARURA),* kuna vigezo. Vigezo hivyo kwanza ni ukubwa wa kijiografia wa halmashauri husika ambayo inachukua alama kubwa.

Mheshimiwa Spika, tunaangalia ukubwa wa halmashauri yenyewe, tunaangalia hali ya kijiografia kwa maana ya milima, mabonde, na pia tunaangalia hali ya mvua. Kwa hiyo vigezo hivi vyote vinazingatiwa katika kutenga bajeti ya barabara katika halmashauri zote kote nchini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Kumba Francis Ndulane kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inanufaika kwa kigezo cha ukubwa wa kijiografia, na ndiyo maana bajeti ya *TARURA* imeongezeka sana katika Halmashauri ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba bajeti yake imeongezwa kwa zaidi ya mara tatu, mara nne katika miaka hii mitatu ya fedha. Tutaendelea kuongeza bajeti hiyo kwa awamu kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika na kupeleka huduma muhimu za usafirishaji na pia huduma muhimu za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Jimbo la Kilwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ni kweli kwamba Jimbo la Kilwa ni kubwa na lina mtawanyiko mkubwa wa vijiji na kata. Unatembea umbali mrefu kutoka kata moja kwenda kata nyingine, na hivyo Serikali imeendelea kwanza kusogeza huduma za kijamii na za kiuchumi karibu na kata hizo kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, shule, na barabara ili kuwawezesha wananchi katika maeneo hayo kupata huduma muhimu za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba, kata hizo pia zinapata huduma zote muhimu ili wananchi waweze kufurahia matunda ya Serikali yao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Halmashauri ya Iringa Vijijini itagawanywa ili ipatikane halmashauri mbili, Lukuvi abaki na ya kwake Ismani; na mimi nibaki na ya kwangu Kalenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kisanga, uliposema Lukuvi ulikusudia kusema Mheshimiwa Lukuvi ama kuna Lukuvi mwingine?

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ni huyu huyu Lukuvi tunatoka halmashauri mbili. Ninataka tugawane, tulikwishaanza mchakato. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa, akiwa humu ndani ni lazima aitwe Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lukuvi wa Ismani abaki na ya kwake na mimi Kiswaga nibaki na ya kwangu, Kalenga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi, kwamba upo utaratibu wa kuomba kupata halmashauri au wilaya mpya ambao unashirikisha ngazi za vijiji, kata, halmashauri yenyewe au wilaya, mkoa na hatimaye kuwasilishwa Ofisi ya Rais,TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Kiswaga kwa kuwa amesema tayari utaratibu ulianza. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumhakikishie kwamba tutafuatilia kuona andiko hilo kama limeshafikishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Katibu Tawala wa Mkoa wa

Iringa. Kama hajafikisha, basi nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimwelekeze Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa wawasilishe andiko hilo na maombi hayo ili Serikali iweze kufanya tathmini ya vigezo.

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu kwa sasa ni kwamba, tumeweka vipaumbele katika kuboresha miundombinu kwenye mamlaka zilizopo kwa sasa. Tunajenga ofisi za Wakurugenzi, ofisi za Wakuu wa Wilaya, nyumba za Wakuu wa Idara na viongozi mbalimbali na miundombinu mingine ya huduma za kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, basi tutaona namna ambavyo tunaweza kupata fursa ya kuanza kupandisha hadhi maeneo mengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kiswaga nikuombe, tutalifuatilia na tutaona namna ya kwenda nalo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Itigi iko katika Wilaya ya Manyoni ambayo ni 58% ya Mkoa wa Singida. Je, Serikali iko tayari sasa kuipa hadhi ya wilaya Halmashauri ya Itigi kuwa wilaya kamili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Itigi ina eneo kubwa la kijiografia, lakini kuna vigezo vingine ambavyo tutavifanyia tathmini baada ya mawasilisho ya mamlaka husika na kuona kama inakidhi vigezo ili tuweze kuona huko mbeleni namna ya kuchukua maamuzi ya kupandisha hadhi kuwa wilaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 653

**Kuratibu Zoezi la Kuhama kwa Walimu**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuratibu zoezi la Walimu kuhama vituo vya kazi hasa maeneo ya Vijijini kwenda Mijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 106 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, uhamisho katika utumishi wa umma hufanyika kwa lengo la kuboresha utendaji wa kazi. Aidha, uhakiki wa rasilimali watu uliofanywa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ulibaini uwepo wa mahitaji mengi ya rasilimali watu hususani, walimu katika maeneo ya vijijini tofauti na mijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utaratibu wa kufanya msawazo wa watumishi wa umma kwa kuongeza rasilimali watu katika maeneo ya vijijini na yale yenye uhitaji mkubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa utaratibu wa sasa wa watumishi kuhama kuwafuata wenza wao hasa kwenye kada ya walimu kumeathiri sana maeneo ya vijijini na kusababisha upungufu mkubwa wa walimu maeneo ya vijijini ukilinganisha na mijini. Nilitaka nijue, je, Serikali ina utaratibu gani sasa wa kupeleka walimu Mkoa wa Mara hasa Wilaya ya Rorya ili kufidia na kutengeneza msawazo kutokana na upungufu wa walimu kujitokeza kwa Mkoa huu wa Mara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Jafari Chege kwa namna anavyofuatilia masuala yanayohusu watumishi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Ofisi ya Rais, Utumishi tulitoa waraka wa watumishi wenye uhitaji wa kuwafuata wenza na walijitokeza watumishi takribani 10,000 ambao walikuwa na uhitaji wa kuwafata wenza. Zoezi hili tumeanza kulifanyia kazi, ambapo watumishi takribani 500 tayari tumetoa vibali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tumeweka utaratibu wa kuweka, baada ya kumtoa yule anayemfuata mwenza, basi tutaweka *replacement* kwa ajira mpya; na wengine ambao tutawatoa sehemu zenye watumishi wengi kuwapeleka pale tulipowahamisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Jafari, pia nitoe rai kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara kuleta orodha kwa maeneo ambayo wale watumishi wamehama ili tuweze kupeleka watumishi hawa haraka, kwa sababu tayari Mheshimiwa Rais katika vibali vile 33,000 alivyovitoa tayari tuna walimu 10,652 ambao tutajaziliza mahali pale tulipowahamisha hao ambao wamehama kwa kuwafuata wenza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ucheleweshwaji wa walimu wanaoomba kuhama pamoja na watumishi wengine, zoezi linachukua muda mrefu sana, unakuta ameshakamilisha taratibu zote na anabaki kwenye kituo akiwa *stranded* kwa muda mrefu bila kupata majibu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha majibu ya uhamisho kwa watumishi wa umma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Mafuwe, ni kweli tumeweka mfumo kupitia *ESS,* kwamba kuna sehemu ya *e*-Uhamisho ambapo walimu au watumishi wengine wanapaswa kuomba uhamisho kwenye mfumo. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi wakiomba wale ma-*supervisor* wao hawawapi kibali kwa haraka. Kwa hiyo, unakuta ombi hilo linakaa kwenye ngazi ya *supervisor* kwa muda mrefu kiasi kwamba mtumishi anabaki anasubiri kwa muda mrefu akidhani kwamba jambo lake limeshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa Ofisi ya Rais, Utumishi tumeweka utaratibu kwamba, sasa mfumo ule tunabadilisha, kama mtumishi ataomba kuhama, basi kama *supervisor* wake hatatoa au hatafanya *action* kwa muda husika, ombi lile litahama kwenda ngazi ya juu ili kuweza kufanyika uhamisho kwa maana ya ngazi ya juu ifanye maamuzi ili hao watumishi wasicheleweshwe kusubiri uhamisho ambao unakwama katika ngazi za *supervisors*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Nishati tutaiweka mwisho. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu. Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 655

**Kusaidia Wahanga wa Ukatili wa Kijinsia**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kusaidia wahanga wanaopata mimba kutokana na ukatili wa kijinsia wa mashambulio ya kingono na ubakaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuzuia vitendo vya ukatili na kuhudumia wahanga na manusura wa vitendo vya ukatili kupitia Mpango wa II wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto 2024/2025-2028/2029.

Mheshimiwa Spika, wahanga wa mimba zitokanazo na ukatili wa kijinsia wanapata hifadhi za muda katika nyumba salama ili kuwalinda watoto pia kuzuia kuharibu, ushahidi ambao utahitajika katika mnyororo wa hakijinai. Vilevile, wanapata huduma mbalimbali ikiwemo unasihi, huduma za afya, mafunzo ya stadi za maisha na fani mbalimbali za ujuzi ili waweze kujimudu kimaisha watakaporejea katika jamii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina ombi tu kwa Serikali. Majibu yao ni mazuri, ila nilikuwa ninaomba tuwatafutie wataalamu wa akili kwa maana watu wengi wakishafanyiwa vitendo hivyo wanakuwa na matatizo, wawe wanawafanyia *counselling* mara kwa mara. Pia ikiwezekana wale wanaopata mimba kutokana na njia hiyo wapatiwe posho kidogo kwa sababu wengi wao hawana uwezo wa maisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, nimepokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge, wataalamu hao wapo. Kadiri tunapopata kibali cha ajira, tunazidi kuwaajiri kwa sababu tuzidi kuwahudumia watu hao

na kuondokana na matatizo mbalimbali ambayo wananchi wanayapata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha ambazo tuwapatie watu ambao wanapata manusura ya ujauzito, Wizara inaendelea kuwasaidia katika hatua mbalimbali za kimaisha ili waondokane na changamoto za maisha na waweze kuendelea na maisha yao yawe mazuri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Elimu ni ufunguo wa maisha. Kwa kuwa wengi wa vijana hawa wanaofanyiwa ukatili, wanakosa elimu, lakini Serikali yetu imetambua kwamba kuna haja ya kuwa na *re-entry*, yaani wanapewa fursa ya kurudi shuleni. Je, watoto wale wanapozaliwa, wakakosa malisho (ulezi), Serikali iko tayari kuwasaidia wale bibi na babu wa wanafunzi wao, sehemu kama ya *TASAF* ili wawalishe wajukuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally. Serikali inaendelea kuwapatia huduma mbalimbali wale ambao wameathirika au hawana uwezo wa kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina vituo vyake vya kuwawezesha watoto hawa. Pia kuwapa elimu wale ambao wamepata changamoto ya mimba za utotoni ili waweze kuendelea na maisha na kuwapa vifaa ambavyo vitaweza kuwasaidia kujiwezesha na kuendelea kumudu maisha yao katika jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu majibu yake ya nyongeza, ameainisha kwamba, kuna nyumba salama ambazo zinahifadhi wahanga wa ukatili wa

kijinsia. Mkoa wa Mara hatuna kabisa hizi nyumba salama na hasa Wilaya ya Tarime ambapo kuna matukio mengi ya hivi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanajenga hii nyumba salama kule Wilaya ya Tarime?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther. Kuhusu nyumba salama Serikali kama ilivyoeleza, ina nyumba salama ambazo zinawahudumia watu hao.

Mheshimiwa Spika, tumeelekeza kwa wadau mbalimbali ambao wanaweza kujitokeza kujibu nyumba hizo. Serikali iko pamoja nao na tuna miongozo na taratibu zote za kuwawezesha kujenga nyumba hizo ili wananchi wetu wawe salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 656

**Kuyapatia Vitendea Kazi Madawati ya Jinsia Nchini**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuyapatia Madawati ya Jinsia nchini vitendea kazi ikiwemo magari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara inaratibu dawati la jinsia na taasisi za elimu ya juu na elimu ya kati na dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma, kwa mfano Sokoni.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji kazi, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatoa mafunzo na vitendea kazi vikiwemo mwongozo wa uzalishaji, uendeshaji na ufuatiliaji wa kazi za dawati na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, mathalan, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pikipiki 85 zilinunuliwa kwa ajili ya maafisa katika mikoa 13, halmashauri 13 na kata 65. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2024 Wizara inatarajia kununua pikipiki 100, na itaendelea kufanya uwezeshaji endelevu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninashukuru kwa vile vitendea kazi hivyo tayari wameshaanza kuvinunua. Tunategemea kama walivyosema, kwamba watavinunua, lakini tuhakikishe kwamba tunafanya haraka ili vitendea kazi hivyo vifike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sina swali la nyongeza, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika madawati ya jinsia, kweli kuna wataalamu pale, lakini kuna mambo mengine ambayo ni ya siri. Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga chumba mahususi ili wale wenye mambo ya siri waweze kuyaeleza kwa uwazi zaidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, katika madawati kwenye vituo vyote vya Polisi au sehemu mbalimbali ambazo zina madawati, tuna chumba maalumu hususan kwa wale hasa wanaotaka kujieleza kwa

uwazi na tuna wale watu ambao ni Askari, lakini tunaweka katika hali ya kuwa sio Maaskari, wawe watu wa kawaida ili wananchi waweze kujieleza kwa ufasaha, na fursa ili aweze kueleweka na kusaidiwa ili changamoto zake ziweze kutekelezwa na kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa mnayofanya ya kupeleka vifaa kwa ajili ya kusaidia utendaji kazi wa madawati haya, je, mmejipangaje kuwapa utaalamu wale wanaotoa huduma hii kwa sababu inaonekana wakienda wanaume mara nyingi hawahudumiwi sawasawa na wanawake, na hasa kupewa kauli za kashfa kama vile, "Mwanaume mzima unapigwa na mkeo!" Mmejipangaje kutoa elimu ili watoe huduma kwa usawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, kauli ya nani amepigwa na nani?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko kwamba wanaume wakienda kupata huduma kwenye madawati haya, mara nyingi hawajibiwi vizuri ikiwemo kuambiwa kwamba, yaani yule mtoa huduma anamjibu mteja mwanaume aliyekuja kulalamika kwamba, "wewe mwanaume mzima unakuja kushitaki unapigwa na mkeo, huoni aibu?" Sasa wanaume wanashindwa kwenda kwa uhuru. Wamejipangaje kuwapa elimu ili watoe kwa usawa huduma hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Jesca kwa kujali sana wanaume ambao wanapigwa na wake zao. Madawati haya yamewekwa kwa ajili ya watu kueleza shida zao, na kama kuna jamii yoyote au mtu yeyote amekwenda pale na akajibiwa sivyo inavyotakiwa, tunamtaka basi aripoti ili tuweze kulifanyia kazi jambo hili na yeye aweze kuhudumiwa inavyostahiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

Na. 657

**Hitaji la Miundombinu ya Kisasa Gereza la Sumbawanga**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA K.n.y. MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutengeneza miundombinu ya kisasa katika Gereza Sumbawanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Gereza la Mahabusu Sumbawanga ni miongoni mwa Magereza yaliyojengwa katika kipindi cha ukoloni katika mwaka 1927 hali iliyosababisha majengo na miundombinu ya Gereza kuwa chakavu. Serikali kupitia Jeshi la Magereza, inatekeleza mpango mkakati wa ukarabati wa Magereza nchini ambapo Gereza la Sumbawanga ni miongoni wa Magereza yatakayoingizwa kwenye awamu ya pili ya ukarabati kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa sasa Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na wadau wa Wilaya ya Sumbawanga, linaendelea na ukarabati wa gereza kwa kufanya upanuzi wa gereza kwa kujenga mabweni matatu na miundombinu ya kisasa yenye uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 200 kwa siku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali ambapo tayari imeanza mipango ya kukarabati hii miundombinu, lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri unaweza ukapanga muda wa kwenda kutembelea gereza hili ukajionea wewe mwenyewe kwa macho yako jinsi miundombinu inavyofanana?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Gereza la Wanawake Kingolwira ni gereza kongwe la muda mrefu, na majengo yake mengine yamechakaa. Je, kuna mpango gani wa kukarabati majengo haya ya wanawake ambayo ni gereza kongwe hapa Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza la kwenda kutembelea gereza ninamwomba awe miongoni mwa wale wanaotuombea turejee, na tunaamini wazi kwamba kwa kazi ambayo imechapwa na Mheshimiwa Rais nchini hapa, sisi Waheshimiwa Wabunge tunateleza tu kurudi majimboni kwa ajili ya kwenda kutekeleza wajibu wetu. Kwa hiyo, ninakuomba tu tuwe wavumilivu katika kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukarabati, mpango wa ujenzi wa magereza mapya ya kisasa katika wilaya karibia 50 zisizokuwa na magereza na zile ambazo zina magereza chakavu tayari umeandaliwa. Katika kipindi cha mpango wa fedha 2024/2025 zilitengwa karibu shilingi bilioni nne, na hili Gereza la Kingolwira ni miongoni mwa magereza yatakayopitiwa kwenye ukarabaji unaokuja. Kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Ishengoma tuvute subira kidogo tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, Gereza la Keko ndani ya Jimbo la Temeke ni gereza la muda mrefu sana na tunaombwa tulifanyie ukarabati. Tumekuwa tukiomba muda mrefu kufanyiwa ukarabati, lakini ukienda sasa hivi ni gereza ambalo hakika halipendezi tena pamoja na magereza waliopo huko ndani. Je, Serikali ina mkakati gani mkubwa hasa wa kutengeneza lile gereza au kuhamisha lile gereza kwenda mahali pengine kwa sababu lipo katikati ya watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa kwa haraka kusema tutalihamisha lile gereza kwa sababu ni la kimkakati, kwa kweli limekaa pale kwa ajili ya kuhifadhi mahabusu ambao wanakwenda kwenye mahakama ambazo zipo karibu na eneo lile. Kwa hiyo, tupokee hili jambo la ukarabati ambalo tunakwenda kuliangalia kwa umuhimu wa pekee na hasa kwa kuwa ni gereza ambalo lipo katikati ya mji, na uchakavu wake haupendezi kwenye macho ya watu. Kwa hiyo, tumelichukua hilo Mheshimiwa Kilave tunaenda kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 658

**Ujenzi wa Mnada wa Mifugo Kintinku – Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mnada wa Mifugo wa Kintinku katika Halmashauri ya Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina wajibu wa kuhakikisha kuwa biashara ya mifugo inafanyika katika mazingira yenye miundombinu muhimu ili kurahisisha biashara hiyo. Katika kufanikisha hilo, Serikali hujenga na kukarabati miundombinu hiyo ili kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 268.2 kwa ajili ya ujenzi wa uzio (ukuta) mzunguko wa meta za mraba 500 katika Mnada wa Kintinku uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Ujenzi wa mnada huo ambao ulihusisha ujenzi wa ukuta, umekamilika kwa 100% kwa mujibu wa mkataba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Katika Kata ya Manyoni na Kata ya Sanza tuna mifugo wengi na tuna minada ya mifugo, lakini hakuna uzio. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunajenga sasa uzio wa Minada ya Sanza na Manyoni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kata ya Makuru ipo umbali wa kilometa zaidi ya 70 kwenda kwenye mnada wa Manyoni na wafugaji wanapata shida sana kupeleka mifugo yao Manyoni. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaanzisha mnada wa mifugo katika Kata ya Makuru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, hili la kujenga uzio Sanza na Manyoni kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia jambo hili. Tumeshalichukua, tutaliingiza kwenye bajeti ijayo kwa ajili ya kujenga uzio katika minada hiyo mikubwa ambayo wananchi wetu wamekuwa wakinufaika nayo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu muhimu iliyobaki basi nimwombe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manyoni aangalie nini anachoweza kuanza nacho ili Serikali Kuu itakapokuja kukamilisha uzio, miundombinu mingine iwe imekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga mnada mwingine kule Makuru, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelichukua, tunakwenda kuliingiza kwenye Bajeti Kuu ili tuone tunajengaje mnada kule?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anakwenda kumalizia muda wake, na tuna uhakika atakwenda kushinda tena, basi kwenye Halmashauri yao, vikao vile vya Kamati ya Fedha waweke kama kipaumbele cha ujenzi wa mnada huo ili itakapokuja Wizarani tuweze kukamilisha ujenzi wa mnada huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang ni ya pili kwa ukubwa wa uuzaji wa mifugo katika Mkoa wa Manyara. Ina jumla ya minada 17. Halmashauri ya wilaya tayari imeshaomba fedha maalumu kwa ajili ya miradi ya Mnada wa Endasak, Endagaw pamoja na Katesh. Je, ni lini Serikali itaeleta fedha hizi ili minada hii ijengwe kwa kisasa hasa ukizingatia katika mkoa wetu ni wilaya ya pili kwa ukubwa wa uuzaji wa mifugo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Asia Halamga kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia jambo hili. Nimhakikishie, mara tu tutakapokuwa tumepata fedha Wizarani, tutakwenda kujenga minada hii katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba pia Halmashauri ya Wilaya ya Hanang waweke katika vipaumbele vyao kwamba hiki ndiyo kipaumbele chao wanakwenda kujenga minada hiyo ili na sisi Wizarani tutakapoona hiki ni kipaumbele chao, basi tuweze kujenga minada hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri ninadhani unajua Bunda tuna mnada mmoja tu wa Bitaraguru na bado haujawa mnada wa kisasa. Ni lini sasa mtatujengea mnada wa kisasa katika Mji wa Bunda ili tuwe na minada mingi na wafugaji wetu wawe wana uwezo wa kuuza mifugo yao kwa uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, pale Bunda ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge mnada ule ni mnada wa kawaida, lakini tutakwenda ku-*upgrade* sasa uingie kwenye viwango vya Kimataifa na uweze kutoa huduma kwa wafugaji wetu kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakachofanya, tutatuma wataalamu waende kuangalia na wafanye tathmini juu ya nini kinachoweza kufanyika pale ili kufanya mnada huo uwe mnada wa kisasa. Tofauti na hapo, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia jambo hili, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 659

**Ujenzi wa Miundombinu katika Visima vya Mpalu na Lochinu**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga miundombinu katika visima viwili vya maji Vijiji vya Mpalu na Lochinu ili kuondoa adha ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Wizara ya Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inapatikana kwa wananchi wote nchini ikiwemo wa Vijiiji vya Mpalu na Lochinu.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma hiyo, Serikali imekamilisha taratibu za kumpata fundi ujenzi na ununuzi wa mabomba yenye urefu wa kilometa 2.9 pamoja na matanki yenye ujazo wa lita 20,000. Ujenzi wa miundombinu katika visima vilivyopo vijiji vya Mpalu na Lochinu unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Septemba, 2025 na kunufaisha wananchi wapatao 2,663, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu ambayo wameyatoa yenye kuleta matumaini kwetu sisi Wananewala Vijijini. Pia niendelee kuishukuru kwa sababu imetutengea fedha shilingi bilioni 84.7 kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa Maji wa Makonde ambao chanzo kipo Newala Vijijini. Nina swali na ushauri. Nianze na ushauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu, ulianza kutekelezwa tangu 2023, ninaishauri Serikali ifanye hima ili

muda ambao imejipangia kukamilika wa Septemba, 2029 mradi ukamilike na wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali. Tunatambua kwamba Serikali ilitenga visima vitano kwa kila jimbo katika nchi kupata hivyo visima. Sasa ninataka kupata *status* ya visima vitano ambavyo vimetengwa kujengwa kwenye Jimbo la Newala Vijijini. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimwambie Mheshimiwa kwamba ushauri tumeupokea na tutakwenda kuufanyia kazi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri. Katika hili tumpongeze sana kwa ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Serikali ilipoona kwamba kuna haja sasa ya kufikisha majisafi na salama na ya uhakika katika vijiji vyote Tanzania nzima, iliahidi kwamba itajenga visima vitano kila jimbo. Katika hili, tayari kwa upande wa jimbo hili la Mheshimiwa Mbunge visima vitano hivi utaratibu wake umeshaanza na kisima kimoja tayari kimeshajengwa katika Kijiji cha Ukombozi. Vimebakia vijiji vinne ambavyo tayari utaratibu wa uanzwaji wa ujenzi wa visima hivi umeshaanza.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba utaratibu huu ama ujenzi huu unakwenda kukamilika hivi karibuni kama tulivyoeleza katika jibu la msingi ili sasa wananchi wa maeneo ya vijiji hivyo waweze kutumia majisafi na salama, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa nimewaona, lakini sasa huyu anajibu kwa niaba ya Wizara, siyo Wizara yake. Kwa hiyo, kama mnataka kumkabidhi atoke nayo, hilo ni suala moja; lakini kumtarajia yeye ajibu kwa mujibu wa Kanuni zetu zinavyotaka, hataweza kujibu hayo maswali kwa sababu yeye ni wa Wizara nyingine.

Kwa hiyo, nimewaona, kama vipi tafuteni swali lingine huku mbele nitawapa fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 660

**Ujenzi wa Barabara ya Maswa – Mwanza**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Maswa kupitia Shishiyu – Malya hadi Nyambiti Mwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Maswa (Nyalikungu) - Shishiyu – Malya – Nyambiti hadi Fulo kilometa 123.92; sehemu ya Malya – Nyambiti hadi Fulo kilometa 71 ikiwa ni maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kazi ya usanifu imefikia 50%. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu iliyobaki ya kutoka Maswa (Nyalikungu) – Shishiyu hadi Malya kilometa 53.92. Kazi hii ikikamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba Serikali imeanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kipande kile cha Malya – Nyambiti ambacho kipo Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ninataka kuuliza sasa, ni lini upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utaanza kwa kipande cha Maswa – Nyalikungu kwenda Malya kupitia Shishiyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa nini Serikali isitumie utaratibu wa *design and construction* badala ya utaratibu huu ambao inafanya sasa hivi ili kuharakisha ujenzi wa barabara hii unaenda kwa haraka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ninapokea pongezi za Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa jinsi ambavyo Serikali imeanza kuchukua hatua kwenye barabara zake.

Mheshimiwa Spika, pili, ninampongeza sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa jinsi anavyofuatilia miundombinu ndani ya jimbo lake na sehemu ya matunda tumeanza kuyaona Barabara ya Njiapanda kwenda Malampaka kilometa 21 imeshaanza kujengwa kiwango cha lami, na kama tulivyosema, na usanifu umeshaanza kwa Barabara Nyambiti – Malya ambapo upo kwa 50%.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa tumeshaanza kujenga barabara hii ambayo nimeshaitaja kilometa 21, na kwa kuwa kipande hiki cha juu tumeshaanza usanifu tuko 50%, atupe nafasi kama Serikali tutafute fedha. Tukishaanza kuzipata, tutakwenda kuanza utekelezaji wa kufanya usanifu na upembuzi yanikifu, na mara baada ya kukamilisha hatua hiyo, tutakwenda kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, alikuwa anatoa ushauri, kwa nini tusijenge kwa mfumo wa *design and construction?* Jukumu mojawapo la Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa nikiri kupokea ushauri alioutoa tutakwenda kuupeleka Serikalini, tutauchakata na kisha tutajua hatua bora ya kuendea ushauri wake, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 661

**Kuboresha Miundombinu ya Michezo Katika Chuo na Shule Maalum ya Patandi**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga upya kiwanja cha michezo katika Chuo na Shule ya mahitaji Maalum Patandi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Mkenda, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilikamilisha ujenzi wa shule mpya katika eneo lililokuwa uwanja wa mpira wa miguu wa Chuo cha Ualimu Patandi. Serikali imepanga kuboresha viwanja vya michezo vya Chuo cha Ualimu Patandi ikiwa ni pamoja na kujenga uwanja mpya wa mpira wa miguu ndani ya eneo la Chuo kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa michezo Chuoni hapo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tathmini ya gharama za ujenzi huo inaendelea kufanyika ili kujenga kiwanja kitakachokidhi mahitaji ya wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalum.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa mradi huu, na mikakati ambayo wanayo kuhakikisha wanajenga. Kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Pallangyo anauliza kwamba, wametenga eneo la Madira pale Arumeru Mashariki, wanaomba kama Serikali mngejenga viwanja vya michezo ili vijumuishe shule zote ambazo zinazunguka Jimbo na Wilaya kwa sababu eneo hilo ni eneo la kimkakati. Hilo ni ombi lao.

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni kwa ajili ya wananchi wa Makete. Mpango wa Mheshimiwa Waziri wa kujenga viwanja kwenye shule nchi nzima ni mpango mzuri. Sasa ni lini wanaweza kuanza kujenga angalau shule moja ndani ya Wilaya ya Makete iwe ni Iwawa au Tandala ili angalau shule iwe na viwanja ambavyo ni *complex* kusaidia wanafunzi wetu kufanya michezo kama UMISETA na shughuli nyingine za michezo mashuleni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa naomba tu shukrani zetu ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Pallangyo. Hili suala la viwanja vya michezo pale Arumeru amekuwa akilifuatilia muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lake hili tunalichukua kwa sababu tunahitaji wanafunzi washiriki sana kwenye michezo na tunajua kwamba moja ya sababu inayoweza ikachochea wanafunzi kuja shuleni na kukaa na kufurahia maisha shuleni ni kushiriki katika michezo.

Mheshimiwa Spika, katika hilo ombi lake la kuhakikisha kwamba viwanja vinaweza vikatumika na shule nyingine, tutalitilia maanani katika tathmini ambayo tunaifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi la Mheshimiwa Sanga kule Makete ambako nilikuwa mgeni wake, muda siyo mrefu sana, tutaangalia, kwa sababu tutafanya kazi na TAMISEMI, lakini mwelekeo wa Serikali sasa hivi katika kutoa elimu ni kwamba michezo ni sehemu ya masomo. Hatuchukulii kama michezo ni sehemu ya kupoteza muda, na ni muhimu sana wanafunzi wote washiriki katika michezo yote.

Mheshimiwa Spika, shule ambazo zina viwanja vya kutosha tutajitahidi kadri ya uwezo wetu na bajeti itakavyoruhusu kuhakikisha kwamba tunaweka viwanja vizuri vya michezo na kwa sababu tutakuwa na mkondo vilevile wa amali ambayo inazingatia masuala ya michezo, basi itabidi kwa kweli kwa wanafunzi hasa wa shule za msingi kuhakikisha kwamba wanashiriki vizuri kwenye michezo ili vipaji vionekane mapema wale ambao wanataka kuingia katika mkondo wa amali michezo watambulike na kupelekwa katika mkondo huo, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kuna utaratibu mpya wa ajira zinazotolewa sasa hivi kwa wanafunzi waliomaliza vyuo mbalimbali na kufanya mitihani mbalimbali ikiwemo ya *oral* pamoja na *practical,* wanapoenda tena kwenye ajira wanapewa mitihani mingine, na katika mitihani wanayopewa wako wanaofeli na wako wanaofaulu. Je, kwa nini huu utaratibu upo? Ni kwamba hawa wanaotoka vyuoni hawaaminiki, ni lazima wapewe tena mitihani mingine?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hili ni nje kabisa ya swali la msingi, ningependa tu kumweleza Mheshimiwa Cecilia Paresso kwamba utaratibu wa ajira umewekwa vizuri na Ofisi ya Rais, Utumishi kwa waajiriwa wote wa Serikali, na wanapoitwa kufanyiwa mtihani au kufanyiwa usaili,

wanakuwa vilevile tayari walishafaulu katika kozi ambazo walikuwa wamezifanya.

Mheshimiwa Spika, inafanyika hivyo kwa wanasheria, imekuwa ikidumu muda wote ipo, kwa wanaotaka kufanya *CPA* hata kama wana *Degree* ya *Account* wanafanya hivyo hivyo, kwa madaktari pamoja na kwamba wana *degree* za udaktari wanafanya hivyo hivyo. Kwa hiyo, ni utaratibu ambao uko chini ya utumishi. Kwa hiyo, ningeomba tu kwa kweli tulichukulie kama ambavyo lipo kisera.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani kwa Vyuo vile vya *FDC* kama kile Chuo cha Ufundi ambacho kiko pale Ifakara kuviboreshea viwanja vya michezo maana yake vimechoka sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Asenga. Ni kweli kwa suala la michezo siyo kwa shule tu, lakini hata kwa vyuo, tunahitaji sana kuchangamsha vijana wetu kwa sababu michezo inawasaidia kuwa na afya nzuri na kujenga mahusiano. Kama hivi, tulikuwa na mashindano yamehitimishwa kule Iringa; tunafanya hivyo hata katika vyuo vyetu vya *FDC*.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na ukarabati wa vyuo vya *FDC* na kuimarisha miundombinu. Hatujakamilisha, kwa hiyo, kadri tunavyokwenda, tutajitahidi kuhakikisha kwamba na tunaiongeza miundombinu kwa ajili ya michezo katika vyuo hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 654

**Ujenzi wa Kituo cha Kusambaza Umeme Nkangamo – Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha kusambaza Umeme Nkangamo – Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme cha Nkangamo - Momba ulianza mwezi Mei, 2024 ambapo utekelezaji wa mradi huo umefikia 30%. Aidha, ujenzi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Mei, 2026, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, tena napongeza majibu ya Serikali. Ombi langu, mchakato uharakishwe, utimie ndani ya huo muda. Pia nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwamba vijiji vyote 72 vimewashiwa umeme, lakini umeme tunaotumia kule Momba bado una nguvu ndogo, hivyo kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi kuzorota. Je, ni upi mkakati wa Serikali kutusaidia kwenye jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Vijiji hivyo 72 vyote ambavyo vimewashwa umeme ni kwenye vitongoji vya makao makuu. Ni upi mkakati wa Serikali kupeleka umeme kwenye vitongoji vilivyosalia kwa haraka ili wananchi wengine wasione kuachwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. Swali la kwanza kuhusiana na kuongeza nguvu ya umeme katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kuna tatizo hilo kwa sababu *lane* ambayo inalisha Jimbo la Momba ni *lane* ambayo inatokea umbali mrefu sana kutoka katika kituo cha kupoza umeme cha Mwakibete kilichopo Mkoani Mbeya. Ndiyo maana Serikali imeona umuhimu sasa, ndiyo maana tunatekeleza mradi huu wa kujenga kituo cha kupoza umeme pale Nkangamo ili sasa Momba iweze kulishwa kutokea pale.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi hatutasubiri mradi wote umalizike mpaka Rukwa ndipo tuwashe kituo cha kupoza umeme cha Nkangamo. Tunavyozungumza, Mkandarasi yuko *site* na tunamsimamia. Ni mkandarasi mzuri sana, tumekubaliana tutakapokamilisha *lane* kutoka Iringa kwenda Kisada hadi Nkangamo pamoja na kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme, basi tutawasha kituo kile cha kupooza umeme hata kabla ya Mei, 2026 kama mradi utakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake wavute Subira. Jambo hili linatekelezeka na tutawasha hata kabla ya kumaliza mradi ule kule mwishoni.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu vitongoji, sasa hivi Serikali imeanza mkakati wa kupeleka umeme katika vitongoji 20,000 na tumeshatangaza mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 9,000. Katika vitongoji hivi na vitongoji vya Jimbo la Momba vilevile vitanufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeahidi kwamba kuelekea 2030, tunaanza kazi hii ya kupeleka umeme kwenye vitongoji kwa kasi kubwa sana. Nimhakikishie, wananchi wote watafikiwa. Ni kwamba tu maendeleo ni hatua, nimhakikishie kwamba wananchi wote watafikiwa na umeme kwenye vitongoji hatua kwa hatua, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha ninyi kuuliza maswali na Serikali kutoa majibu. Ninalo tangazo la wageni hapa kabla hatujaendelea na ratiba yetu, lakini kabla ya tangazo la wageni kuna jambo moja ambalo linahitaji ufafanuzi kidogo, hili ni jambo linalohusu Waheshimiwa Wabunge maswali wanayouliza yanayohusu wananchi wanaowawakilisha hapa Bungeni, lakini pia wakati huo huo na michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaitoa hapa kulingana na hoja ambazo wanaziona ni za wananchi kutoka huko kwenye maeneo yao wanayowakilisha, pia nyingine ni hoja za Kitaifa kwa ujumla.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kumekuwepo na matumizi labda niseme ya mchango kwa namna ambavyo pengine Mbunge hakuwa amekusudia hilo jambo wakati akichangia wakati huo, maana siyo Bunge hili ambapo ametoa mchango huo, lakini wanauhusisha mchango wote anaoutoa Mheshimiwa Mbunge au swali analouliza Mheshimiwa Mbunge au hoja anayoitoa kwa niaba ya wananchi, hasa zile zinazohusu miundombinu, kama vile huwezi kuwa unaomba sasa miundombinu kwa ajili ya wananchi wakati Bunge hili ni la mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, uhalisia uko hivi, Serikali inaendelea. Bunge linapovunjwa linavunjwa kwa muda. Kwa hiyo, Bunge linavunjwa kwa muda, na Mbunge anapoleta hoja hiyo, haleti yeye binafsi, analeta hoja kwa niaba ya wananchi.

Kwa hiyo, uhitaji wa wananchi uko pale pale, haijalishi kwamba Bunge hili ni la wakati gani, maadam Bunge lipo, basi maswali ya Mbunge yanayohusu wananchi wake, ataendelea kuuliza; na maadam Bunge lipo, hoja zinazohusu wananchi zitaendelea kuletwa na Serikali itaendelea kuzichukua.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeona pia upande mwingine kwa sababu, sijui niite sasa kihoja ama nini? Kwa sababu ya hicho kihoja kinachozunguka kimeleta sura fulani hivi pia, na upande wa Serikali

majibu yanayotoka kwa namna moja ama nyingine yanaashiria kama vile lazima turejee halafu ndiyo kazi ianze, hapana. Majibu yanapotolewa hapa ndani, yanatolewa kwa niaba ya Serikali na kwa hiyo, Serikali inakuwa imetoa jibu.

Jibu likishatoka, kazi inaanza ya ufuatiliaji bila Bunge kuwepo. Yaani hata kabla ya hiyo Novemba kwamba *inshaallah*, watu watakaorejea humu ndani bado kazi itaendelea kwa sababu Serikali ipo, na ndiyo maana Bunge hili pia lilitunga sheria kwa ajili ya kuirejesha Tume ya Mipango ili iendelee kuweka hoja zinazoletwa na Wabunge kwenye mipango ya maendeleo ya Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nimeona nitoe huo ufafanuzi, maana nimeona hata kwenye maswali kidogo Wabunge kuna kujiuliza kidogo kama sasa hapa nikiuliza naweza nikawekewa kale ka-kihoja kwamba inakuwaje, lakini Mheshimiwa Mbunge wakati akichangia wakati huo, Mbunge aliyekuwa anachangia yeye walikuwa na utani naye. Kwa hiyo, alikuwa anamwambia hivyo kwamba, bwana we, hebu tulia kwanza, endelea na mambo mengine sasa. Naona watu wamechukulia hiyo kama ndiyo majibu yaani. Kwamba usiulize chochote sasa hivi Bunge, kama vile lisimame mpaka siku Rais atakapokuja kuhutubia, hapana.

Ndiyo maana shughuli zinaendelea, Wabunge wanaendelea kuchangia na maswali yanaendelea kupangwa kwenye ratiba, kwa sababu Serikali ipo na itaendelea kuwepo. Uchaguzi unahusu wanasiasa, Serikali ipo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo, wageni waliopo Bungeni Asubuhi hii, tutanza na wageni wangu ambao ni Klabu ya Wazee ya Mazoezi ya Jijini Dodoma kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la *AGING PLAN* wakiongozwa na Mkurugenzi, Ndugu Samwel Mwakatumbula. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni 24 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Jumuiya ya Wafanyabishara wa Kariakoo kutoka Wilaya na Mikoa mbalimbali ya Tanzania, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Severine Mushi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine watano wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Viongozi wa Chama cha Kulinda na Kutetea Haki za Walimu Tanzania (CHAKUHAWATA), karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 55 wa Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Hawa ni Jumuiya ya Bandi na *Classical Tour* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ambao ni Taasisi ya Pamoja Tutashinda kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mwantum Dau Haji ambaye ni Ndugu Shabani Yasin, ni mtoto wake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi kwa sababu hii ya watoto kidogo huwa inatuchanganya hapa mbele. Kuna watoto walezi, kwa hiyo sasa, wengine wasije wakaona kuna watoto wengine huwa wanatajwa kila mtoto halafu wengine hawatajwi. Hawa niliowataja hapa sijapewa taarifa maalum kama ni watoto wa Waheshimiwa Wabunge ili niweze kuwataja. Kwa hiyo, sina majina yao hapa mbele ili isilete hiyo hoja ya kwamba watoto wengine wanatajwa kwa majina.

Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ambaye ni Mchungaji Stanley Mwambepo kutoka Rungwe Mkoani Mbeya. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali ambao ni rafiki zake kutoka Mkoani Shinyanga, *(Makofi)*

Pia wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo ambao ni wapiga kura wake kutoka Mwanga Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ambao ni familia yake kutoka Mvomero wakiongozwa na Ndugu Maria Kuyu, Mama Mzazi wa Mheshimiwa. Mama wa Mheshimiwa Mbunge ndio yupi hapo? Hayupo! Haya. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Cecillia Daniel Paresso ambao ni wawakilishi wa wakulima wa zao la ngano kutoka Karatu Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Maimuna Ahmed Pathan ambao ni watoto na Ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo walimu 11 na wanafunzi 126 wa Darasa la Sita na la Saba wa Shule ya Msingi Amani kutoka Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha. Walimu 10 na wanafunzi 44 Shule ya Awali na Msingi ya *Destiny* Mkuranga Mkoani wa Pwani, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndiyo lilikuwa tangazo la wageni tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

## Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026
## na
## Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo orodha hapa ya Wabunge walioomba kuchangia. Pia Waheshimiwa Mawaziri ambao wameomba kuchangia, tutaanza na Wabunge na tutaanza na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kusema ninaunga mkono hoja, na kipekee itakuwa tofauti kidogo na miaka mingine ambayo nimekuwa nikichangia. Leo nitashauri maneno machache halafu baadaye nitakwenda kuwashukuru pia wananchi wa Jimbo la Geita Mjini.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa tukio la juzi, nilikuwa shuhuda kwenye uzinduzi wa Daraja la JP Magufuli. Mimi na wananchi wa Geita tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye uzinduzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, daraja hilo siyo tu ni suluhu kiuchumi kwenye Mikoa ya Geita, Kigoma, Kagera na nchi za Jirani, lakini pia ni daraja

ambalo limekwenda kujenga historia na kuweka maajabu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ni kivutio kipya cha utalii ambacho Serikali imeongeza. Katika nchi kama Ufaransa kuna mnara peke yake, watu wanasafiri kwenda kuangalia mnara. Sisi tuna daraja pale la zaidi ya kilomita tatu.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa kuongezeka pale ni kufanya *extension* kidogo, tukapata sehemu ya kufanya *sport fishing* na kufanya *diving,* tukafanya kama ilivyo kule Cahora Bassa ambako wanakwenda kufanya *diving* wanalipa dola, kwa sababu namna lilivyojengwa linahamasisha watu kwenda kutembea pale kusimama na kuangalia, siyo kurekodi kwaya peke yake kama Waziri alivyosema.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Mheshimiwa Waziri ninatamani sana kuona daraja hilo linatumika kiutalii, na kwa kweli ni kazi kubwa ambayo Serikali imefanya tunaishukuru na tunawapongeza wananchi wa Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka kusema, hivi karibuni wananchi wanaofanya shughuli za uchimbaji walipata leseni kwenye Pori la Kigosi ambalo zamani lilikuwa *National Park,* tukalibadilisha likawa *forest reserve* na watu wakapata leseni.

Mheshimiwa Spika, sasa utagundua kwamba kumekuwepo na kusuasua kwa waliopata leseni kwenda kufanya utafiti au kuchimba, lakini hii inatokana na uwepo wa sheria au hatua nyingi kabla ya kupata kibali cha kwenda kuchimba.

Mheshimiwa Spika, ili mtu aweze kuruhusiwa kuingia kwenda kwanza kutambua eneo lake, lazima apate kibali na kinalipiwa. Vilevile, huyo mtu akilipiwa, yeye atalipiwa kwa siku ambazo anaingia mle porini; atalipia kipande cha ardhi anachoenda kuchimba, atalipia miti atakayokata, atalipia udongo atakaotoa kuupeleka nje, na kule anakopeleka anakwenda kulipia anapokwenda kufanya *processing.* Sasa hizi gharama zote huyu mchimbaji mdogo hawezi kufanya.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitamani Serikali i-*harmonise* tuone kwa sababu wachimbaji hawa wamelipa leseni zaidi ya shilingi milioni moja, tu-*harmonise* hizi sheria, kwani Serikali ni ile ile. Huku mbele mchimbaji huyu anakuja kulipa *royalty,* kodi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna-*room* tayari ya kukusanya mapato ya Serikali baada ya uzalishaji kuanza, kuliko kuweka vizingiti ambavyo vinapunguza uwezo wa watu kwenda kuwekeza kwa kufikiri kwamba gharama hizi tukizikusanya mapema ndiyo tutapata pesa. Ninafikiri tuwekeze kwanza kwenye uzalishaji, halafu baadaye tutakuja kwenda kupata ushuru au na kodi zaidi huko siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nilitaka kuzungumza ni jambo la usambazaji wa gesi. Serikali imefanya kazi kubwa sana. Kupitia Wabunge peke yake karibu mitungi 100,000 imesambazwa. Kuna mitungi zaidi ya 400,000 huko kwenye mikoa inauzwa.

Mheshimiwa Spika, ninadhani kama ambavyo nilishauri kwenye Bunge lililopita, ili kuleta mapinduzi ya matumizi ya gesi, nia njema kabisa ya Mheshimiwa Rais tunapaswa tujue tabia na aina ya watu tunaowapelekea mitungi.

Mheshimiwa Spika, tumepeleka mitungi takribani 500,000 kule chini. Hivi tuna takwimu za wangapi wanaitumia sasa hivi? Kama takwimu hizo tunazo, hatujagundua kwamba wengi waliotumia baada ya kununua wameweka *store?* Kama wameweka *store,* maana yake tatizo letu limerudi *square zero. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu hapa, katika nchi ambazo zimefanya mapinduzi ya matumizi ya gesi, zimekwenda sambamba na kuweka ruzuku kwenye gesi yenyewe siyo kwenye mtungi. Yaani ni mara 100 uniuzie mtungi na gesi kwa bei ya soko halafu uweke ruzuku kwenye gesi ili nipate gesi kwa 50% au chini ya 50% inishawishi kutumia gesi kwenye matumizi ya nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunavyozungumza, wengi wameweka *store* na wengine wanakwenda kuuza kwa bei rahisi shilingi 5,000.00 au 10,000.00 na matokeo yake tumerudi kule kule tulikotoka. Kwa hiyo,

ni ushauri wangu kwamba itafutwe namna ya kupata ruzuku ili mitungi hii ya gesi inayoendelea kusambaa nchi nzima kwa nia njema kabisa na mingine iko mingi inakuja, Wizara imeweka mpango mzuri, iweze kutumika kwa sababu itakuwa ni gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, nilianza kwa kusema kwamba leo nitazungumza machache haya, lakini sasa ninataka nianze kutoa shukrani. Kwanza, ninataka nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuwa mlezi mzuri kwa miaka mitano kwenye hili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa sababu nimepata ushirikiano wa kutosha wakati wote, na kwa kweli niseme kwamba wananchi wa Jimbo la Geita Mjini ambao nimewatumikia kwa miaka mitano, yale yote waliyonituma kuhusu kero zao, nimefanikiwa kuyafikisha kwa sababu ya kazi nzuri inayofanywa na kiti chako. Ninaomba nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninaishukuru sana Serikali. Wakati ninakuja humu, miaka mitano iliyopita nilizungumza sana kuhusu maji na nikazungumza sana kwamba Mji wa Geita ambao ulikuwa ni mji, sasa ni Manispaa, ulikuwa una mahitaji ya maji ya zaidi ya lita milioni 18 lakini unazalisha lita milioni nne.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kubwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwamba sasa ninakwenda kukamilisha miaka mitano. Nina mradi ambao utanipa lita milioni 40 wakati mahitaji ya Mji wa Geita ni lita milioni 18 na sasa hivi uzalishaji umefika lita milioni nane.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitakuwa na uzalishaji wa lita milioni 48 wakati mahitaji ni lita milioni 18. Hivyo nitakuwa na *surplus* ya lita milioni 30. Tunaishukuru sana Serikali, na tunaombea mradi huo mkubwa wa maji ambao uko zaidi ya 70% uweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na mradi mkubwa wa maji, ninaishukuru Serikali kwa visima vingi ambavyo tumevichimba vikiwemo visima vitano ambavyo tulivipata mwaka huu ambavyo

vimechimbwa kwenye maeneo mbalimbali. Ninaiomba tu Serikali kwamba iendelee kusimamia mradi huo ili uweze kukamilika, lakini na usambazaji uweze kufanyika ili shida ya maji kwenye Manispaa ya Geita iweze kwisha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mwaka huu peke yake Manispaa ya Geita imepokea takribani shilingi bilioni 42. Shilingi bilioni 22 kwenye mradi wa barabara ambao unajengwa na *TACTICS* na shilingi bilioni 19 kwenye ujenzi wa stendi. Pia, ninamshukuru Mungu kwamba juzi tumesaini mkataba na kampuni ya *SINOTEC* kujenga Stendi ya Manispaa ya Geita.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa sababu kupata shilingi bilioni 40 kwenye mwaka mmoja wa fedha siyo jambo jepesi. Hata hivyo, ninaiomba sasa Serikali wakati huu tunakoelekea kwenye uchaguzi, ujenzi wa stendi uende kwa *speed* iliyokusudiwa kwenye mkataba na ujenzi wa barabara ambao tayari umeshaanza, uende kwa *speed* iliyokusudiwa kwenye mkataba kwa mantiki ile ambayo imekusudiwa kwenye Manispaa ya Mji wa Geita.

Mheshimiwa Spika, Geita kuwa Manispaa kuna faida yake kwamba tunaongezewa sasa bajeti ya miundombinu kama tulivyoona, lakini pia tunaongezewa bajeti ya fedha nyingine kwa ajili ya huduma za jamii. Ninaishukuru sana Serikali kwa hadhi hiyo ya Manispaa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, ninaishukuru sana Serikali. Nimekuwa Mbunge hapa, nimekuta vijiji vyote vya Jimbo la Geita Mjini havina umeme. Leo ninazungumzia Jimbo ambalo limepata vijiji vyote umeme na limepata mitaa yote umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikuwa jepesi kwa sababu sisi Manispaa ya Geita tulikuwa Geita Mjini, hatukuwa kwenye ruzuku. Kwa hiyo, ilibidi kupambana kwa miaka karibu sita hapa kuishawishi Serikali kutafuta fedha nje ya *REA* kupeleka umeme kwenye maeneo ambayo hayana ruzuku ya *REA*. Ninashukuru sana jambo hilo limefanikiwa. Tumekamilisha sasa usambazaji wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni moja hapa. Waliopata umeme kwenye vijiji ni wale waliokuwa kwenye orodha ya mradi wakati unafika. Kama ni 30 ni 30, na idadi ya nguzo zinaishia hapo. Mahitaji ya vijiji husika unakuta ni watu 300 au 400.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kuna mradi wa *densification* ambao tuliambiwa unaendelea. Pia, tuna mradi wa vitongoji ambao unaendelea, lakini bado haujagusa mitaa 65 na vijiji 15 ambavyo ni karibu ukiangalia vitongoji 15 unakuta maeneo mengine yote yanaweza kubaki zaidi ya mwaka mmoja hayana mpango.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu hapa kwa Mheshimiwa Waziri, umeme tunao na umeme huu utumike au usitumike gharama ya kuuzalisha iko pale pale. Serikali tayari imeshatuletea *megawatts* 4,000. Kwa hiyo, kama tunatumia *megawatts* 1,800 au 2,000, *installed capacity* ni *megawatts* 4,000. Maana yake tuna-*surplus* ya *megawatts* 2,000 ambayo haitumiki, lakini inazalishwa ambayo mitambo ya kuzalisha ipo na wataalamu wa kuzalisha wapo.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tu-*focus* kwenye kufikisha umeme huu kwa watumiaji ili Serikali ikusanye fedha zaidi na Serikali pia irahisishe maisha ya wananchi wale tuliowapelekea. Kuwa na umeme mwingi halafu tukawa na programu ambayo inasubiri miaka mingine 10 kuwafikishia watu umeme na anauona ule pale, hiyo nayo ni kero.

Mheshimiwa Spika, yaani kutokuwepo umeme zamani haikuwa kero, lakini kuuona kwa jirani ule umeme, halafu wewe kwako haupo ni kero nyingine ambayo unaitengeneza pale, na wapigakura wetu wanatabia moja. Hata kama zamani umeme haukuwepo, walikuwa hawazungumzii umeme, lakini akishauona umefika, anaigeuza kuwa kero kwa sababu yeye hajaupata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali, pale ambapo umeme umefika, na tatizo letu ni kwamba yule mkandarasi wa *REA* alishaondoka; tuje na *plan* ya haraka ya kuwafikishia wanaohitaji umeme tena kwa gharama ile ile kwenye maeneo yale yale ili wote wanaotaka umeme waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho amezungumza hapa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wakati akijibu swali kwamba wametangaza nafasi za walimu 11,000. Kuna nafasi zaidi ya 2,000 za masomo ya biashara na Wizara ilipotangaza, ilikosa watu wa kuomba zile kwa sababu hiyo kada kuna wakati ni kama watu waliacha kusoma kupata walimu wa masomo ya biashara, hivyo wakatoa nafasi kwa waliosoma *BBA* kuomba kwenda kufundisha. Ninadhani watawapeleka kozi kidogo labda ya *postgraduate diploma* ili waweze kuwa walimu.

Mheshimiwa Spika, sasa aliyesoma *BBA,* na aliyesoma *B. Com;* unaweza kusoma *B. Com in Accounts, B. Com in Marketing* au *Procurement* na kadhalika. Aliyesoma *BBA,* amesoma utawala kwenye biashara, lakini huku chini huwa tunaanza kusoma masomo, mfano, mimi nimesoma biashara; unaanza kusoma masomo yote na unapofika mwishoni ndiyo una-*specialise*. Kwa hiyo, ukimpa *loophole* aliyesoma *BBA* ni *the same* umpe aliyesoma *Bachelor of Accounts* kwa sababu alisoma masomo yote haya ya biashara wakati anaanza kusoma aka-*specialise accounts* au *procurement*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, sasa ninaona hawa waliosoma *BBA* wanapata hiyo *loophole,* lakini hao waliosoma *B. Com* na waliosoma *BA in Accounts* wanaonekana hawana hizo sifa. Nilitaka Wizara ilitazame hilo na nimeshazungumza na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, mfumo wetu...

**SPIKA:** Kengele ilishagongwa, yaani hapo nilishakupa muda wa nyongeza tayari.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, dakika moja tu.

**SPIKA:** Sasa hiyo moja ni ya mwenzio Mheshimiwa. Haya sekunde 30 malizia.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nilishauri hapa kwamba mfumo wetu ule wa *Ajira Portal* ukisha-*login* ukasema mimi ni *engineer,* ukienda kusoma kozi nyingine unaku-*reject;* na mfumo ulivyo sasa, vijana wengi wanakuwa na *multiple professions.* Nimemwomba Mheshimiwa Waziri sasa hivi, lakini ninaona *status* ni ile ile. Waurekebishe ili mtu mwenye kozi zaidi ya sita anapoona nafasi ya kazi aweze ku-*apply.*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba nichukue muda wako mchache tu kuchangia mambo machache na hasa kwa sababu bajeti hii ni miongoni mwa bajeti nzuri sana ambayo kwa miaka yangu michache, kwa kweli ni bajeti ambayo hata ukifanya tathmini nje huko unagundua kwamba kuna upendo na amani zaidi kwenye suala la bajeti hii. Ninaomba nishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu amegusa nyanja zote zinazohusu maisha ya wananchi wa kawaida. Bajeti hii imegusa kila nyanja, na ukitaka uthibitisho, hata wanaotumia *energy booster* pia wenyewe wameguswa. Ni kitu kidogo, lakini Mheshimiwa Rais ameweza kufika kuangalia maslahi ya watumiaji na maslahi ya wazalishaji. Ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye kila sekta: Sekta ya Elimu, Afya, Miundombinu (madaraja na barabara) zote Mheshimiwa Rais amegusa na kwa kweli ni kwa kiwango kizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mimi ningeomba kuwashukuru wataalamu wetu. Kwanza, ninaomba nimshukuru Waziri wa Mipango, lakini kubwa zaidi ninaomba nimshukuru Waziri wa Fedha kwa sababu

amefanya kazi kubwa sana kwani uchumi ni kitu kingine na *financing* ni kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukiangalia hapa Mheshimiwa Waziri ameingia kote; kwenye uchumi ameweza na kwenye *financing* ameweza. Sasa ninaomba nimpongeze sana na kwa kweli amefanya kazi yetu iwe nyepesi sana kwenye majimbo yetu katika kuwaelimisha au kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nigusie eneo dogo kabisa lakini ndiyo kiini cha bajeti yetu. Hapa nitakuwa na mashauri mawili. Ukienda kwenye ukurasa wa 168 ambapo inazungumza, imeanza 167, sura ya bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026, lakini ninaomba niguse kwenye *core*. Inasema kwamba, matarajio ya makusanyo kwa mwaka huu ni shilingi trilioni 56.49. Sasa ninaomba hapa kidogo wenzangu wanielewe, hasa wale wanao-*deal* na mambo ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo kila siku panatuletea kelele, lakini ninaomba nishukuru, mwaka huu kwa Mheshimiwa Waziri amefanya jambo kubwa sana. Wanasema kwamba kati ya shilingi trilioni 56.49, shilingi trilioni 40.47 haya ni mapato ya ndani, lakini shilingi trilioni 1.07 ni mikopo na hii mikopo imegawanywa kwenye mafungu mawili: kuna mikopo ya ndani na kuna mikopo ya nje. Mikopo ya ndani ni shilingi trilioni 6.27 lakini vyanzo vya nje ni shilingi trilioni 8.68. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *ratio;* sijajua Kiswahili cha *ratio* ni nini, lakini Waziri wa Fedha labda anaweza akatusaidia. Ukiangalia *ratio* ni 0:7, maana yake kati ya mikopo ya nje na ya ndani. Maana yake ni nini? Aliposema Mheshimiwa Waziri kwamba deni letu ni himilivu maana yake ni kwamba *ratio* ile ni 0:7.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba wenzangu hapa watuelewe hivi, kwamba wenzetu hawa wamefanya kazi kubwa na walipotuthibitishia kwamba deni ni himilivu, walikusudia kwa sababu uhimilivu unatokana na hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi kwenye hili niishauri Serikali, kwamba kwa sababu 6.27 na 8.68 maana yake ukiangalia upishano au ulingano ni mdogo sana. Sasa ukienda nane maana yake ni kwamba kati ya haya tunaweza kukopa, lakini vilevile yako maeneo katika shilingi trilioni 56.49, tutalipa madeni yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuweze kufanya kazi vizuri ninaomba tudhibiti sana kwenye suala la matumizi kwa sababu ukienda kwenye Taarifa ya CAG fedha nyingi inapotea kwenye matumizi yetu ambayo kwa kweli ku-*control* inakuwa tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana tukiweza kubanana hili kwenye mwaka huu, maana yake mwakani *ratio* ya mikopo yetu ya nje ukiangalia na mikopo ya ndani itakuwa ni ndogo sana. Kwa hiyo, ningeomba sana kwenye bajeti yetu ya mwaka huu tuangalie sana au tudhibiti sana uwezo wa wataalamu wetu kutupiga chenga kwenye matumizi, ndipo wanapotupiga. Kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, akodolee macho sana kwenye matumizi ili tuweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yake amegusa suala la vipimo. Wakala wa vipimo ukiangalia vizuri zaidi, nimeangalia baadhi ya nchi majirani, kama Kenya, Zanzibar, na wenzetu wa *South* Afrika, sisi kwenye Wakala wa Vipimo wana-*charge* meli kama ni kubwa au ndogo shilingi milioni saba. Sasa sijajua wametumia vigezo gani? Ninadhani hili tuliangalie vizuri, kwamba haiwezekani meli kubwa na meli ndogo zikalipa shilingi milioni saba. Hili halikai sawa. Tuangalie vigezo na tuangalie kwa nchi za majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo, ili tuweze kuimarisha wakala huu, Mheshimiwa Waziri amependekeza tuta-*charge* 0.15 kwa kila lita kama sikosei. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri hivi, lengo letu ni kuongeza mapato ya Serikali na pia kuimarisha wakala huu ili kile kinachoingia kiweze kuleta tija kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, inawezekana Mheshimiwa Waziri anajua zaidi kuliko mimi, lakini asilimia karibuni 50 ya mafuta

yanayoingizwa Tanzania yanapelekwa nje, na ndiyo takwimu zilizopo; ningeshauri, tuwaongezee kidogo kutoka 0.15 basi angalau iwe shilingi mbili ili kila lita wakala huyu apewe shilingi mbili ili aweze kuimarisha na kuhakiki kwamba hakika mafuta yanayoingia ndiyo yanayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa sababu *TRA* wanao mfumo wa kudhibiti mafuta yanayotoka, lakini ukiangalia taarifa ya *CAG,* amesema kwamba mafuta mengi yanayoandikwa kwamba yanatoka nje, kwa kweli yanakuwa *dumped* ndani, maana yake Serikali inakosa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwa na Wakala wa Vipimo, tukiwa na *TRA* ambao wana-*track* mafuta haya kwa kuwawezesha angalau wapate shilingi mbili, nina hakika kwamba Serikali itapata mapato mengi zaidi kwa sababu ya udhibiti. Maana yake ni kwamba mifumo ya *TRA* ya kuweza kudhibiti mafuta haya imeshindikana kwa ambavyo tunategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili tuweze kuwasaidia, ninaomba sana tuwawezeshe hawa wenzetu Wakala wa Vipimo ili waweze kudhibiti yanapoingia, lakini na kudhibiti yanapotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba niipongeze bajeti, niiunge mkono na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza, ninaunga mkono hoja iliyoko Mezani. Pia, natumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Momba. Jana tarehe 22 Juni, 2025 Wizara ya Ujenzi walikuwepo ndani ya Jimbo la Momba kwa ajili ya kusaini mkataba wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Barabara ya kutoka pale Momba kupitia Chitete, Makao Makuu, kutokea Momba –

Kamsamba – Chitete – Mlowo, kwenye Jimbo la Mbuzi, barabara yenye urefu wa zaidi ya kilomita 145.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, sisi kama wananchi wa Jimbo la Momba tunashukuru sana. Kiu kubwa ni kuona lami inakuja kwenye jimbo letu iwe kichocheo cha uchumi kwa sababu, kutoka kwenye eneo lile tunazalisha mpunga mwingi sana ambao unahudumia mikoa mingine mingi na kwenda nchi za jirani, kama Zambia na Congo. Pia, tunazalisha ufuta kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, umegundulika uwepo wa gesi ya *helium* na uwekezaji mkubwa sana umefanyika mahali pale. Kwa hiyo, barabara hii itakapokuwa imekamilika, bila kusahau kwamba, tuna Ziwa Rukwa samaki wengi wanatoka eneo lile, itakuwa ni chanzo kikubwa sana kwa halmashauri yetu, chanzo kikubwa sana kwa Mkoa wetu wa Songwe, kwa mikoa mingine ya jirani na kuongeza pato kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba Waziri wa Fedha pia, utakapofika wakati wake, kuendelea kutupatia fedha, maana tunaanza na kilomita 10, kilomita tano upande wa Kamsamba Jimbo la Momba na kilomita tano kule Mlowo, Jimbo la Mbozi. Tunaomba na kilometa nyingine zinazoendelea kufikia hizo 145 tupate fedha kwa wakati, ili barabara hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwenye hii Bajeti Kuu ya 2025/2026 mimi nitakuwa na maombi mawili, na muda ukiwa rafiki, basi matatu. Jambo la kwanza, nimewahi kuchangia hapa kwa nyakati tofauti na jambo hili ambalo nimekuwa nikilichangia, nashukuru Mheshimiwa Waziri huyu wa Fedha ameshawahi kupata nafasi ya kulitembelea Jimbo langu la Momba, mwaka 2021. Kwa kweli, alifanya ziara yenye tija sana na ninatumia nafasi hii kuendelea kumshukuru.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, kupitia Bunge hili Tukufu kwamba, lile eneo tulilofika kwa ajili ya kupata kituo kipya cha forodha, siyo kwamba, naomba tu kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Jimbo la Momba, lakini ni kwa maslahi mapana ya Taifa letu hili la Tanzania, kwa sababu, maeneo mengi

ambayo yameonekana kujengwa vituo vya forodha, wewe mwenyewe ni shahidi, ndipo mahali ambapo pia *TRA* inajikusanyia mapato ya kutosha, na jicho la Serikali huangalia maeneo hayo, kwa ajili ya kujikusanyia mapato.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo maeneo hayo ambayo yamekuwa na vituo vya forodha, yameonekana kuchachua sana uchumi wa maeneo hayo, na vijana wengi na akina mama kupata ajira, lakini taasisi za kifedha zimeonekana kuwa na mwitikio mkubwa sana kuweka taasisi zao hapo kwa sababu, shughuli nyingi zinazohusu uchumi zinakuwa zipo hapo.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wamekuwa wakivutiwa sana. Kwa mfano uwekezaji wa hoteli na shughuli mbalimbali. Mfano mzuri tunatolea eneo kama Namanga, kama Tunduma na maeneo mengine yote kama kule Sirari, ambayo yanavyo vituo vya forodha.

Mheshimiwa Spika, natolea mfano nchi nchi ya Kenya, ambayo tumepakananayo; kuna vituo vya forodha zaidi ya vitatu; Namanga hapo, Holili na hata kule Sirari. Kwa kweli, inashangaza kidogo kuonesha mpaka wa Tanzania na nchi ya Zambia ambayo nyuma yake imebeba nchi zaidi ya nne, tunasema ni lango kuu la *SADC*. Tafsiri yake ni kwamba tuna mpaka ambao unabeba mipaka mingine zaidi ya nchi tano.

Mheshimiwa Spika, Congo wanategemea kupita hapo kwenye kituo cha forodha, Zimbabwe wanategemea kupitia hapo, Namibia wanategemea kupita hapo, Botswana wanategemea kupita hapo na hata nchi ya *South Africa* ikitokea, kuna mtu yeyote amepokea mzigo kupitia Bahari ya Hindi ambao inabidi uende kwa barabara kupitia Zambia wanategemea kituo kimoja cha forodha cha Zambia.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo imesababisha kuonekana kuwa na mlundikano mkubwa sana wa magari pale Tunduma. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri ameshawahi kufika pale Jimbo la Momba na anafahamu, tulifika wote mpaka upande wa Zambia na wenzetu wa Zambia baada ya kuona tu kwamba, lile eneo ni fursa, wao tayari wameanza kujizatiti, wamejenga *gate toll.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, magari yote ambayo yanapita na kuingia kwenye nchi yao, kwa sababu, wanajua eneo lile ni la fursa pia, limeonekana ni la watu kupitishia magendo, kwa sababu, Zambia wao wamelitumia kama eneo la fursa ya kujiongezea kipato, wameshajikinga kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, kupitia Wizara hii ya Fedha ,ni kwa sababu, kituo hiki cha forodha kitakuwa na manufaa makubwa, lakini Serikali imeshaanza kuweka uwekezaji pale. Tumejenga Soko la Kimataifa la Mifugo na Mazao ambalo lipo kabisa mpakani mwa nchi ya Zambia na kwetu huku Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaamini baadhi ya miundombinu tayari imeshatangulia. Tunatamani kuona swali lile ambalo limejibiwa mara ya mwisho kwamba, tunaanza *feasibility study*. Tunaomba lifanyike kwa haraka na kwa upesi sana, ili Tanzania na mpaka wake wa Zambia angalau tupate kituo cha forodha ambacho kinafanana na hadhi ya Tunduma, kituo cha pili.

Mheshimiwa Spika, tunaomba, kwa kuwa, upande ule wa Jimbo la Momba unaonekana kuwa na barabara nzuri kufikia nchi ya *DRC,* basi angalau tuseme magari yote ambayo yatakuwa yanaingia na kutoka kwenda nchi ya *DRC,* yapitie kituo cha forodha kipya ambacho kiko ndani ya Jimbo la Momba. Tutachachua uchumi wa eneo lile, tutaongeza kipato na ajira zisizokuwa rasmi zitapatikana kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, nimechangia kwenye bajeti hii zaidi ya mara tatu. Naomba sana Wizara ya Fedha mchukue jambo hili kwa umuhimu kujua kwamba, ni jambo la muhimu, litakuwa ni chanzo kizuri sana cha mapato.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ni ombi, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana husika, jambo hili pia linahusiana na Wizara ya kilimo. Tunatambua nia njema ya Serikali kuweka mfumo wa stakabadhi ghalani ili wananchi waweze kupata bei kwa njia sahihi ambayo inatokana na Serikali, ili kuondoa urasimu wa wananchi

kuibiwa mazao yao na wafanyabiashara wasiokuwa na nia njema ya kumnyonya mkulima.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unapokuwa unatekelezwa, wakati mwingine kuna changamoto ambazo zinatokea ambazo zinaweza zisiwe za Serikali, lakini ni kulingana na hali halisi ya soko la dunia likoje. Sisi kule Momba na maeneo mengine tunalima ufuta ambao ni zao la biashara. Mwaka 2024 ndiyo tumeanza kutekeleza Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, ili halmashauri yetu na vyama vya ushirika, mfano *SORECU,* viweze kupata mapato na pia, ku-*control* yaweze kufika mpaka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajua kwamba, mazao haya yanapoonekana ni fursa duniani, na nchi nyingine zinajizatiti kwa ajili ya kulima na kujiongezea kipato. Tunajua katika mwaka huu, 2025, Brazili ilizalisha ufuta mwingi sana na ikauingiza sokoni. Hivyo, imesababisha ufuta ambao umelimwa katika maeneo yetu kushuka bei. Tafsiri yake ni wananchi wameona kwamba, mfumo wa stakabadhi ghalani ni kitu ambacho siyo sahihi ilhali tunajua *demand and supply* iliyoko duniani imechagizwa na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, kama ambavyo huwa tunafanya kwa mazao mengine kama mahindi, inapoonekana kwamba *demand* inakuwa *high* huko duniani na *supply* imekuwa *limited* kwamba, sisi huku Tanzania tumezalisha kwa kiwango kikubwa, lakini nchi nyingine hazijazalisha, mahindi huwa yanapanda bei na wananchi wetu kujipatia kipato. Inapoonekana nchi nyingine pia, zilizalisha kwa wingi na sisi Tanzania tulizalisha kwa wingi na bei inashuka, Serikali huwa inachukua jukumu la kuyanunua mahindi hayo na kuyatunza ili kuwaondolea maumivu Watanzania ambao wamelima kwa shida.

*Mheshimiwa Spika, naomba pia, katika hili tunajua Serikali inazo njia na milango mingi ya kusaidia, siyo muda wote Brazil ataingia sokoni kimabavu ku-control soko la dunia.*

**[MANENO HAYA SIYO SEHEMU YA TAARIFA RASMI ZA BUNGE]**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Tunaomba vile ambavyo huwa tunafanya kwenye zao la mahindi, tufanye hivyo hivyo pia kwenye zao hili la ufuta. Ufuta umeshuka bei sana na wananchi wakati mwingine wanafikiri Mfumo wa Stakabadhi Ghalani siyo kitu sahihi au kwa kuwa, wananchi waliwekeza nguvu nyingi na tuliwahamasisha kwamba, mazao mengi ambayo yanauzwa kwa Stakabadhi Ghalani yataenda kumsaidia mkulima bila kumnyonya.

Mheshimiwa Spika, basi tuombe turuhusu soko huria, wafanyabiashara waingie kununua ufuta kwa wananchi. Inaweza ikasaidia soko kutokuonekana kuwa *monopoly* kwa sababu, wote wanapaswa kwenda kuuza kwa Stakabadhi Ghalani, ili wananchi waondoe yale machungu, kwa sababu, mwaka 2024 tumeuza ufuta kilo moja zaidi ya shilingi 4,500.00, lakini muda huu tunavyoongea mnada wa mwisho bei ilikuwa chini ya shilingi 2,500.00 kidogo inawaumiza wananchi kwa sababu, waliwekeza nguvu nyingi. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tunaomba maombi haya muweze kuyachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester, wakati unajenga hoja yako, umezungumza hapo kuhusu Brazil kuingia sokoni kimabavu? Sijaelewa vizuri hili.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninamaanisha kwamba…

**SPIKA:** Nataka nikishaelewa ndiyo nijue kama hayo maneno yafutwe ama vipi.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, wamezalisha kwa kiwango kikubwa ufuta, hivyo wamefanya ufuta uwe mwingi sokoni na bei kushuka kwenye hizi nchi nyingine kwa sababu, ufuta umekuwa mwingi, lakini nina-*withdraw* hiyo kauli. Maana wamezalisha kwa kiwango kikubwa, wameonekana kwamba, wao wamekuwa *tough* sokoni.

**SPIKA:** Sasa kama wamezalisha kwa wingi, ni haki yao. Hawawezi kuzuiwa kuzalisha, na sisi tuzalishe ili tuwazidi.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli.

**SPIKA:** Kwa hiyo, inabidi hii kauli ya kusema, "Brazil kuingia sokoni kimabavu," iondoke, ili mchango wako huo…

**MHE. CONDESTER M. SICHAKWE:** Mheshimiwa Spika, nimeiondoa.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stella Martini Manyanya. Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Bajeti ya Mwaka 2025/2026, Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza, natumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya ambayo ametujalia mpaka leo tunasimama kuhakikisha tunaendelea kuwatumikia Watanzania kwa kuja kuwawakilisha humu ndani.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kuendelea kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambazo anazifanya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza na kukushukuru kwa namna ya pekee kabisa kwa kutulea sisi vijana ndani ya Bunge hili hadi leo ninaposimama hapa. Tumeiva, tupo imara kwa sababu, Spika wakati wote umetulea na tumeweza kuwa wawakilishi wazuri ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakishukuru sana Chama cha Mapinduzi pamoja na jumuiya zake kwa kuendelea kuwalea vijana wa Kitanzania katika misingi mizuri ya uongozi, utaifa, uzalendo na kuipenda nchi yao. Natumia nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambazo amezifanya. Kazi za Kitaifa alizozifanya Mheshimiwa Rais pamoja na kwenye maeneo yetu, ni ndani ya Taifa letu hili la Tanzania, kule ambapo tunapotoka.

Mheshimiwa Spika, tumpongeze Rais kwa kazi kubwa ya ukamilishaji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kwani imeleta tija kwenye maeneo tunayotoka kwa sababu, miundombinu ya umeme imeendelea kukamilika. Wote tunafahamu umeme ni chanzo kikubwa cha maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, napongeza miradi mikubwa kama *SGR,* ambapo sasa hivi imerahisisha maisha, Watanzania wanasafiri na kufika kwenye maeneo yao kwa wakati. Wagonjwa wanafika hospitali kwa wakati na wanapata huduma, tunaendelea kupunguza vifo.

Hakika Mama Samia kila la heri, Oktoba, 2025 Watanzania tunasubiri kukupigia kura za "Ndiyo," kura za kishindo. Kazi umeifanya mama, Watanzania wameiona.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa Daraja la Busisi na madaraja mengine makubwa katika nchi yetu. Hakika angaweza kuacha kazi hizi ambazo zilikuwa zimeshaanza, lakini Mheshimiwa Rais toka ameingia madarakani amezishika kazi ambazo zilikuwa zimeachwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, amezifanya na kuzikamilisha, kazi imeonekana.

Mheshimiwa Spika, wote tunaingia mitaondoni sasa tunaona. Boti la kisasa kabisa ambalo limetoka Mtwara, hata mimi mwenyewe jana nilisimama, ili niweze kupiga picha niwe miongoni mwa watu wa Mwanza, japo nilikuwa hapa Dodoma. Tunaendelea Kumshukuru sana na kumpongeza Rais kwa kazi kubwa ambayo anatufanyia sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi kama kijana, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba, ameendelea kutoa mikopo katika vyuo vikuu, vyuo vya kati na pia, kuendeleza kujengwa kwa vyuo mbalimbali ndani ya nchi yetu, vikiwemo vyuo vya kati, kama *VETA*. Hii yote ni Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan na Serikali yake ya Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba, anatoa fursa mbalimbali za elimu na ujuzi kwa vijana wa Kitanzania, ili kuendelea kutengeneza maisha yao. Ni nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan katika nchi yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, sisi vijana tuna kila sababu ya kujivunia. Hivi juzi tu katika bajeti hii tumeona punguzo la faini kwa vijana wa bodaboda na bajaji, faini ya kutoka shilingi 30,000.00 mpaka shilingi 10,000.00. Hii yote ni kuhakikisha kwamba, kijana wa Kitanzania anaendelea kujiimarisha kiuchumi, kujikuza kiuchumi na kukuza pato lake binafsi pamoja, la jamii na la nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Waziri wa Fedha na Mipango kwa sababu, leseni zimeondolewa, faini kutoka shilingi 70,000.00 mpaka 30,000.00. Hii yote ni kuendelea kuhakikisha kwamba, kijana wa Kitanzania, kile kipato anachopata kinaenda kuwa chenye tija kwake na kwa jamii yake.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mapato ilikuwa ni shilingi 65,000.00, lakini leo tunavyoongea, kodi hiyo imetolewa, ni shilingi sifuri katika bajeti hii. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kumsaidia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba, anaendelea kutatua matatizo kwa vijana, kwa Watanzania, kukuza uchumi, pamoja na kuhakikisha kwamba, nchi inaendelea kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, siyo bajaji peke yake, tuna kundi kubwa la vijana ambalo limeajiri. Kundi la bajaji hili, faini zake zimetolewa kutoka shilingi 120,000.00 mpaka shilingi sifuri. Ni nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutengeneza mazingira mazuri ya vijana, hasa katika miradi ya *BBT* pamoja na akinamama. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba katika bajeti hii tumeona bado Serikali ina nia

njema, dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba, vijana pamoja na akinamama wa Kitanzania wanatengenezewa mazingira mazuri ya kupata ajira na kipato, kwa ajili ya familia zao na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, binafsi katika kuwawakilisha vijana wenzengu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatokea Mkoa wa Manyara, hususan Wilaya ya Hanang, mwaka 2024. Tulipata maafa ya mafuriko ndani ya Wilaya yetu ya Hanang, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa ziara nje ya nchi, lakini alisitisha ziara na kuja kutukimbilia Wanahanang. Alikuja kusimama na sisi, wananchi wetu walikosa makazi, lakini hivi leo tunavyoongea, Mheshimiwa Rais ametuletea fedha, makazi yamejengwa na wananchi wako kwenye makazi zaidi ya nyumba 108. Ahsante sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mungu aendelee kukutunza Mama, Mungu akupe afya njema, tunakusubiri Oktoba tuweze kukupa kura zetu za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninatokea Hanang. Tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea mradi mkubwa wa stendi mpya na ya kisasa iliyochukua zaidi ya shilingi bilioni tano. Stendi imetatua ajira kwa akina mama, stendi itatoa ajira kwa vijana, stendi italeta fedha kwa Watanzania pamoja na nchi yetu kupata mapato kwa kupitia stendi ile. Ahsante sana mama Samia kwa kuung'arisha Mji wa Katesh kwa kuing'arisha Wilaya ya Hanang.

Mheshimiwa Spika, kazi hii kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya ninajua katika mkoa wetu wa Manyara, hajaifanya Hanang, amefanya katika wilaya zote kwa kada tofauti tofauti. Tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia, kwani katika mafuriko yale, tuliondokewa mpaka na soko. Mheshimiwa Rais ametuletea zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga soko la kisasa katika Wilaya ya Hanang. Ahsante Mheshimiwa Dkt. Samia, Wanahanang tuna deni na wewe na kazi yetu ni kulilipa Oktoba.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii sasa kusema, ndani ya Wilaya ya Hanang katika Mkoa wa Manyara tuna fursa kubwa sana

ambayo katika bajeti zote nimeweza kujaribu kuiongelea. Tunayo chumvi ya kutosha, tunayo madini ya kutosha, na tunayo miundombinu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kilichobakia ni kuona kwamba Serikali wanatuweka kwenye mpango ili kuona kwamba Wilaya ya Hanang inakwenda kuwa wilaya ya viwanda ili chumvi ile ambayo ni dhahabu na lulu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, baraka ile tuliyopewa na Mwenyezi Mungu tuone sasa wananchi wanaanza kupata uchumi na kwamba uchumi ule wa Hanang unaleta tija kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, wapo wenzetu wa nchi nyingine wanakuja pale wanachukua chumvi ile na inakwenda kuwa na tija kwenye nchi zao wakati sisi wananchi tuko pale. Nina imani kubwa na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, na ndiyo maana ina mikakati na mipango thabiti. Ndiyo maana hivi karibuni tumepitisha Ilani ya Uchaguzi ambayo ni dira na mwelekeo wa nini kitafanya katika mwaka 2025/2030.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo ukubwa wa Chama cha Mapinduzi, na huu ndiyo ukubwa wa CCM. Hauongei maneno maneno, unaongea kwa mipango, na mipango ile ya kwenye Ilani tunaona sambamba iko humu Serikalini, kwa maana ya bajeti hii ya 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, Wilaya ya Hanang ipo *cement* ya kutosha. Tunahitaji viwanda Mogitu. *Cement* ile, na baraka ile tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, tunaomba sasa ikawe na tija kwetu sisi, kwa wananchi wetu na pia iwe na tija kwa Taifa letu. Iweze kuleta fedha za ndani pamoja na fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa uzima na afya, kama ambavyo nilitangulia kusema. Ninawashukuru sana Mkuu wetu wa Mkoa wa Manyara, Kamati ya Ulinzi na Usalama, Kamati ya Siasa ya Mkoa, Kamati za Siasa za Wilaya, na Kamati za Ulinzi na Usalama za

Wilaya. Nichuke nafasi hii kuwashukuru sana kwa kuendelea kuzisimamia fedha hizi ambazo tunaziomba hapa.

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru watendaji wote wa Serikali ngazi ya halmashauri, watendaji wa kata, watendaji wa vijiji, na watendaji wa vitongoji. Wenyeviti wa vijiji wameifanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuendelea kuwashukuru Wenyeviti wa Chama cha Mapinduzi kwa ngazi zote kuanzia kata, mashina, mpaka matawi. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana mabalozi kwa kazi wanazozifanya za kuendelea kusimamia miradi hii na kuibua miradi mipya ambayo sisi tunakuja kuiombea fedha humu ndani, wamenikuza.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuwashukuru wazazi wangu, nyumbani ni Hanang; nimekua, nimekomaa, nimeiva. Hivi viwanda nilivyokuja kuviomba, nitakuja kumdai Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, nitakuja kumwuliza tena, awe amevikamilisha ili viweze kwenda kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninakuombea heri katika uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa Watanzania, Mheshimiwa Rais ameifanya kazi kubwa sana. Kurukaruka kwa mahindi ya bisi ndiyo kuiva kwake. Kwa hiyo, hawa wanaorukaruka, tuwaache waruke lakini Mheshimiwa Dkt. Samia ndio mpango wa Watanzania, ndio mpango wa maendeleo na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mimi najua Watanzania wanawaona watu majukwaani, hakuna mtu anayemwona mwenye kitabu cha ilani, kitabu cha ilani chenye mipango ya Watanzania kipo kwa Chama cha Mapinduzi na kiliwekwa wazi kwenye mitandao ya kijamii. Mkutano ulikuwa wa wazi kwa sababu tuna mipango na Watanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana…

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutuweka kuwa salama mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru pia wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umeliongoza Bunge letu katika kipindi chote hiki. Hakika tunaamini kabisa Wanambeya hasa kule Uyole, watatenda haki na watakurudisha bila usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyasa kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi chake cha Urais hiki ambacho tunakimaliza. Wananyasa wanapenda kumthibitishia kwamba wako naye na watakuwanaye bega kwa bega mpaka dakika ya mwisho, na wanaamini atapata ushindi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitaongea mchango wangu. Ninafahamu mchango huu ni wa Bajeti Kuu, kwa hiyo, kimsingi ni mchango ambao ni wa Kitaifa. Kwa kuanzia, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwa jinsi ambavyo wameitendea haki nchi yetu katika kipindi walichokua madarakani; na pengine Mwenyezi Mungu atawaendeleza tena, lakini pia Manaibu wao na timu yao yote ya uongozi ambayo wanafanyanayo kazi katika Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza pia Kamati ya Bajeti kwa upande wa Bunge, pia na wenyewe wameifanyakazi kubwa katika

kuhakikisha kwamba bajeti inawekwa kiasi cha kusaidia Watanzania kufikia malengo ya hali bora ya maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitaulilia kwanza mradi wa reli kutoka Mtwara – Mchuchuma – *Mbamba Bay*. Ninaomba mradi huu sasa ufikie mahali uanze. Wananchi wana hamu na wana kiu kubwa, na hasa baada ya kuonja reli hii ya *SGR* kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na inavyoendelea. Kwa hiyo, wanaona huo ni ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania imeishaamua kuthubutu, imejaribu kuthubutu na imeweza kuthubutu, basi tunaamini kwamba na reli hiyo itaweza kujengwa kama ambavyo inatarajiwa ili kuweza kutoa mizigo kutoka Mtwara na kupeleka mpaka pale *Mbamba Bay,* mingine iweze kuvuka kwenda nchi jirani kama Malawi na Msumbuji kama ambavyo tumejiona boti sasa ikitokea Mtwara kwenda mpaka Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hali hiyo ni kwamba hizi bandari zetu zinapokuwa imara na miundombinu ya reli ikawa imara hali ya maisha ya Watanzania itazidi kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ninashukuru sana kwa bandari inayoendelea kujengwa pale *Mbamba Bay* ambayo ni bandari ya kisasa kabisa, haijakwama, inaendelea kila siku na ujenzi wake; pamoja na barabara ile itakayokuwa inaingiza mizigo mpaka kule bandarini, barabara ambayo ni pana, ya njia mbili kwa mbili kulia na kushoto. Kwa kweli kwa Mkoa wa Ruvuma ndiyo itakayokuwa barabara ya kwanza kwa upana. Kwa hiyo, hayo ni maendeleo makubwa ambayo yameenda kule wilayani kwangu Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa leo ninaomba niongelee jambo moja. Hili naomba kuliongea kwa sauti kubwa zaidi kidogo. Ni jambo linaonekana kuwa la kawaida, lakini ni jambo la msingi sana. Tumeshuhudia Mheshimiwa Rais alipoamua fedha za *UVICO* ziende zikajenge madarasa, mabadiliko makubwa yalitokea. Ni maeneo ambayo tuliyasahau.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, changamoto ambayo ninaiona bado ipo kubwa sana ni ukosefu wa vyoo bora, nikimaanisha kuwa na maji ya kutosha katika maeneo hayo ya shule zetu za msingi na sekondari. Kwa kweli ni jambo ambalo linatia simanzi.

Mheshimiwa Spika, nimefanya ziara katika maeneo mbalimbali hususan kwenye jimbo langu, nikaona kuna changamoto kubwa sana ya vyoo bora hasa maji. Maji ni tatizo kabisa. Unaweza ukajenga vile vyoo ambavyo sasa hivi kuna huu mradi mpango wa *SWASHI* unatusaidia kupeleka vyoo kule, lakini baada ya kuvijenga vile vyoo unakuta hakuna maji. Inaleta simanzi kubwa kwa watoto namna ya kutumia vyoo vile. Vilevile inaweza ikawa ni chanzo cha magonjwa.

Mheshimiwa Spika, ni vitu vya kawaida, vidogo lakini mimi ninadhani kwa hatua tuliyofikia Watanzania, ya kuona kwamba iko haja ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia hususan kwa upande wa vyoo, niwaombe sana, yawezekana kwenye bajeti hii hatuweka maalumu kwa ajili hiyo, lakini iwepo kwenye mpango kwamba sasa tujihakikishie kila shule iwe na vyoo bora na iwe na maji ya kutosha ili kuona kunakuwa na usalama kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, ninaomba sana Bajeti ya Wizara ya Maji iangaliwe kwa umakini. Wizara ya Maji ihakikishe kwamba kila shule inapata maji. Iwe ni ya kutoka kwenye vyanzo vingine au visima, lakini shule zipate maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepata simanzi sana wakati ninatembelea na kuona hiyo changamoto, nikajua ahaa, kwa sababu mimi nimeshazoea kuwa kama *whistle blower* kwa Serikali yangu, basi hili nilifikishe kwa sauti hiyo. Ninawaomba sana Wizara tufanyie kazi suala hilo ili watoto wetu waanze kuwa na ustarabu tangu wakiwa wadogo mpaka wanapondelea katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, safari hii kuna shule nilitembelea pale ya *Eng.* Manyanya, na shule nyingine kama Mitumbitumbi, shule kama Malamala; zote hizo zina changamoto ya maji. Kwa hiyo, najua tatizo hilo sasa, kwa sababu nimecheki kata zangu zote nikajua siyo la

Wilaya ya Nyasa tu, ni la Taifa zima. Basi tulipatie kipaumbele suala la vyoo na maji shuleni.

Mheshimiwa Spika, pia maji hayo yatawaisaidia hata kupata majisafi ya kunywa. Kwa hiyo, niombe sana sana, pale pana kijiji na kwa hiyo, hapatakiwi pakatokee milipuko. Hilo ndilo suala langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ni kuhusiana na maliasili na utalii. Ninashukuru kwa jitihada kubwa zilizofanyika za kuendeleza utalii katika Wilaya ya Nyasa. Kwa hiyo, na sisi tunaanza kuwa kwenye mfumo wa kuchangia uchumi kupitia utalii, na kwa kweli tumesogea sana kiutalii.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo limefanyika. Baada ya kuona kwamba namna gani tunasogeza hayo masuala ya kiutalii, taasisi ipi itusaidie? Tuliamua kuwapa mlima ya *Mbamba Bay* pamoja na kisiwa cha Lundo pale *Mbamba Bay* wenzetu wa *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, sasa kilichotokea ni kwamba wanawazuia wananchi wasiende kufanya matambiko yao kule kwenye Mlima wa *Mbamba Bay*. Kwa hiyo, hilo nalileta kwenu. Utalii ni pamoja na kuheshimu mila na desturi za watu. Kwa hiyo, naomba hilo katazo kama lipo lifanyiwe kazi mara moja ili wale wazee wasikasirike juu ya matambiko yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ninaomba bajeti ya *TARURA* isaidiwe, kwa sababu kuna barabara nyingi za vijijini ambazo tulikuwa tumezianzisha, na barabara hizo hazijakamilika, na ni mategemeo makubwa kwa wananchi. Kwa mfano, kuna Daraja la Mto Luhekea pale linalotakiwa kuunganisha Likwilu na Mtipwili katika Wilaya ya Nyasa. Ninaomba lisaidiwe ili liweze kukamilika. Lilikuwa limeondolewa na mvua, kwa hiyo, liweze kujengwa upya.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hizi barabara kuu, barabara ya Rwanda – Ndumbi ambayo tayari imeshasainiwa. Kinachotakiwa ni kuipatia fedha tu ya kuanzia. Ninaomba hizo fedha zitolewe ili sasa kazi hiyo iweze kuanza mara moja. Pia mtufikirie, sasa katika hiyo

barabara ya Ndumbi – *Mbamba Bay* mpaka Chiwindi – Nanyoni mpaka Mitomoni hizo ni barabara kuu za kufungua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa bei ya zao la kahawa. Kahawa sasa bei yake imekuwa nzuri. Tulikuwa tunauza kwa shilingi 3,000.00 mpaka 4,000.00, lakini sasa hivi tunauza kwa shilingi 10,000.00 mpaka 14,000.00 kwa kilo, jambo ambalo limewafariji sana wananchi. Wanaishukuru sana Serikali yao, wanampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, tunachoomba sasa, watuangalie katika ruzuku ya madawa ili tuweze kupata kahawa nyingi zaidi na ambayo ni bora. Katika eneo hilo, tumekuwa hatutoi ruzuku ya madawa kama ilivyo kwenye korosho na mazao mengine. Kwa hiyo, ninawaomba, kama labda ilisahaulika, pamoja na kutupatia miche, lakini ni vyema mkatupatia na pembejeo hizo za dawa ili kuweza kupata zao bora na kuweza kupata faida kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hayo, ninaona kama nakaribia mwisho sasa, nizidi kusema kwamba kazi kubwa imefanyika na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na sisi Wabunge. Ninapenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Nyasa kwa wema wao, kwa upendo wao, kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote nilichohudumu katika Jimbo la Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia kwa kunitia moyo. Akina mama wamekuwa mstari wa mbele kunitia moyo, akina baba wamekuwa hivyo hivyo bega kwa bega na sisi, hata wazee, na wote. Mimi ninaamini, kama haki itatendeka inavyotakiwa, bado nitaendelea kuwa Mbunge wao wa Jimbo la Nyasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa hilo ninashukuru sana na kwa sababu ninakiamini sana Chama change, Chama cha Mapinduzi katika ngazi ya kura za maoni, ninaiamini sana Serikali yangu katika hatua ya pili ya Uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo, ninaamini mambo yote katika majimbo yote yatakuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, ninazidi kushukuru na kupongeza jitihada za Daraja la Mitomoni. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ulega, nimshukuru sana Mheshimiwa aliyetangulia, Mheshimiwa Bashungwa kwa lile Daraja la Mitomoni na Daraja la Mkili. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, hatuwasemi sana Mawaziri hawa kwa sababu kazi ya Wizara ni kutema fedha. Basi waendelee kutema hizo fedha ili mambo ya Watanzania yaendelee kuwa mazuri. Hongera sana kwa Waheshimiwa Mawaziri wote na timu yao, Mwenyezi Mungu awabariki sana. Ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba tunapoelekea katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka mingine 25 ya Taifa 2050, ninatoa ushauri ufuatao: -

(i) Kuhakikisha suala la afya ya akili nchini linashughulikiwa kikamilifu ili kuwa na Taifa la watu wenye uwezo wa kuzalisha kwa tija, kujitambua, kupambana na changamoto na wenye uwezo wa kuchangia kwenye maendeleo ya Taifa kupitia jamii yetu. Hivyo, ni muhimu sana Baraza la Afya ya Akili nchini lianzishwe kwa mujibu wa sheria yetu tuliyojitungia wenyewe.

(ii) Kuimarisha utalii Kusini ili kuhakikisha vivutio vilivyoko Kusini mwa Tanzania vinachangia katika kuongeza pato la Taifa, hasa fedha za kigeni. Hivyo, ni muhimu sana mipango yetu kama Taifa iangalie namna ya kuufanya Mji wa Iringa kama lango la utalii unaboreshwa ili kuwa sehemu ya kivutio cha utalii kusini.

(iii) Elimu yetu izingatie mahitaji ya soko kama ilivyo kwamba bajeti yetu inazingatia mahitaji ya jamii na siyo kuzingatia bajeti zilizopita. Hivyo, ni muhimu sana kuhakikisha elimu ya ujasiriamali ambayo ndani yake inahusisha *creativity* na *innovations* na utafiti. Hii

itasaidia sana kuwa msingi wa kufanya mapinduzi ya maendeleo ya nchi yetu.

(iv) Usawa wa binadamu ni muhimu sana. Dhana ya usawa iwe asilimia 50 kwa 50 kwa jinsi zote mbili kwa wanawake na wanaume. Mipango yetu izingatie jinsia zote mbili. Tunapojenga mabweni ya watoto wa kike, basi tujenge na ya kiume pia. Fursa zozote zitolewe kwa usawa.

(v) Upo msemo unaosema Taifa lisilo na utamaduni hilo ni Taifa lililo duni, haliwezi kutambuliwa popote duniani. Hivyo ni muhimu tamaduni zetu zilizo nzuri zifuatwe ili kujiepusha na mila potofu, kama ndoa za jinsia moja, ushoga na usagaji na ndoa za utoto na ufamilia. Hili liende sambamba na kupambana na mila na desturi potofu ikiwemo imani potofu. Tuimarishe Taifa letu kwa kulinda maadili mema ndani ya nchi yetu.

(vi) Serikali ifanye uwekezaji mkubwa kwa vijana katika kuwawezesha kiuchumi. Tuwekeze tu kwa vijana katika shughuli zao, kwani hawa wakiwa *busy* zaidi ya kuongeza pato la Taifa itapunguza sana uovu nchini.

(vii) Ulinzi na usalama wa Taifa letu kama ajenda ya kudumu, basi tuweke miundombinu ya ulinzi wetu uwe wa kisasa na wa teknolojia ya juu. Hii itapunguza sana sintofahamu zisizo za msingi ikiwemo hizi za utekaji, uuaji au kupotea kwa binadamu. Miji mikubwa ilindwe na mifumo ya kisasa ya kiteknolojia ikiwemo kufunga vyombo vya kisasa katika miji ya ulinzi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninampongeza sana Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge na Naibu wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge; Katibu Mkuu, Ndugu Natu El-Maamry Mwamba; Naibu Makatibu Wakuu, Ndugu Jenifa C. Omolo, Ndugu Amina K. Shaaban na Ndugu Elijah G. Mwandumbya; na wataalamu wa Wizara na taasisi zilizoko chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza majukumu yao ya kusimamia ukusanyaji wa mapato na kusimamia sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, pia ninampongeza sana Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na Naibu Waziri, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo; Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na Dkt. Fred Matola Msemwa, Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango, kwa kazi kubwa za kutengeneza mipango ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye umuhimu wa Watanzania kulipa kodi na changamoto kubwa zinazoikabili nchi yetu na mapendekezo ya namna ya kuzitatua.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kishujaa, Waziri wetu wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ametoa hotuba ya viwango ambapo bajeti ya Taifa imeongezeka kutoka shilingi trilioni 50.29 na kufikisha shilingi trilioni 56.46 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya shilingi trilioni 6.2, ongezeko la 12.3%, bajeti ambayo ni kubwa zaidi katika historia ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze na kumsifia Waziri kwa kusimamia vizuri ukusanyaji wa kodi na Sekta ya Fedha. Vicheko vya Wabunge na mafanikio ya Serikali ni kutokana na usimamizi mzuri wa Waziri wa Fedha na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha malengo ya bajeti pendekezwa, niwaombe Watanzania wote na walipa kodi wote kulipa kodi ili fedha ya kuiendesha Serikali na kuijenga nchi yetu ipatikane. Wahisani wetu wa maendeleo wanaonekana kutuchoka, na hii inatokana na matamko mbalimbali yaliyotoka hivi karibuni kusitisha misaada. Hivyo basi, ni vyema tuchangie wenyewe kupitia kodi zetu ili kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata neno la Mungu katika Bibilia Takatifu kuhusu kulipa kodi linatuelekeza kulipa kodi (Mathayo 22:17-21); 17 Basi tuambie, wewe unaonaje? Ni halali, au si halali kulipa kodi kwa Kaisari?" 18 Yesu alifahamu hila yao, kwa hiyo, akawaambia, "Ninyi wanafiki, kwa nini mnajaribu kunitega? 19 Nionyesheni sarafu mnayolipia kodi." Wakamletea sarafu. 20 Yesu akawauliza, "Picha hii

na sahihi hii ni za nani?" 21 Wakamjibu, "Ni za Kaisari." Basi Yesu akawaambia, "Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari; na ya Mungu mpeni Mungu."

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, ni vyema Watanzania wakalipa kodi kama ilivyoekezwa kwenye kitabu kitakatifu.

Mheshimiwa Spika, maisha ya Watanzania yanakumbwa na changamoto nyingi zinazotokana na masuala ya kijamii, kiuchumi na mazingira. Changamoto hizi zinaathiri kwa kiasi kikubwa hali ya maisha, upatikanaji wa huduma za msingi na uwezo wa wananchi kufikia malengo yao binafsi na Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, licha ya juhudi mbalimbali za Serikali na wadau wengine wa maendeleo kusaidia katika kupunguza changamoto hizi, bado kuna maeneo ambayo yanahitaji juhudi za ziada ili kuleta mabadiliko chanya kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni baadhi ya changamoto za maisha kwa Tanzania ambazo zinakwamisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya kwanza inayolikabili Taifa letu ni ile ya ukosefu wa ajira na hususan kwa vijana ambao wanajikuta wakimaliza masomo bila kuwa na ajira zinazolingana na ujuzi wao. Kukosekana kwa ajira kunasababisha kuongezeka kwa umaskini na kuathiri ustawi wa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi hujikuta katika ajira zisizo rasmi ambazo mara nyingi hazina usalama wa kazi wala kipato kinachoweza kukidhi mahitaji yao ya msingi. Hali hii ya ukosefu wa ajira, pia husababisha kushuka kwa kiwango cha maisha na kutokuwepo kwa usawa wa kiuchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri iliyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026, bado ninaishauri Serikali iwekeze katika elimu na ajira. Katika hili, Serikali na wadau wa maendeleo wanapaswa kuongeza juhudi za kutoa elimu bora na nafasi za ajira

kwa vijana. Hii inaweza kufanyika kwa kuboresha elimu ya ufundi, kushirikiana na sekta binafsi katika kutoa mafunzo ya kazi na kuanzisha mipango ya kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inapaswa kuwekeza katika miradi ya ajira kwa vijana kama vile miradi ya kilimo, ufundi stadi na ujasiriamali. Tunaishauri Serikali ipanue wigo na kushirikisha vijana wengi katika mradi wa *BBT* (kilimo, mifugo, uvuvi, madini).

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikafanya uboreshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ili uongeze uwezekano wa vijana kujiendeleza kiuchumi. Aidha, ni muhimu kuimarisha vyuo vya ufundi na mafunzo ya ujasiriamali ili kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri na kukuza uchumi wao binafsi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili inayowakabili Watanzania ni ukosefu wa huduma bora za afya hapa nchini hasa katika baadhi ya maeneo ya vijijini. Changamoto za maisha zinajidhihirisha sana katika sekta ya afya ambapo upatikanaji wa huduma bora za afya ni changamoto kwa watu wengi hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, hospitali nyingi zinakosa vifaa vya kisasa; dawa muhimu na wahudumu wa afya wa kutosha, hali inayowafanya wananchi wengi kutopata huduma zinazostahili. Hii inasababisha vifo vinavyoweza kuzuilika na kuathiri uzalishaji wa Kitaifa kwa sababu watu wengi hutumia muda mwingi wakitafuta huduma za afya au wanashindwa kufanya kazi kutokana na kuwa na magonjwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye sekta ya afya, bado ninashauri Serikali kuboresha huduma za afya vijijini na mijini. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa hospitali zinapatiwa vifaa vya kutosha na wataalamu wa afya wanaoendana na mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia huduma za afya ya msingi zinapaswa kupatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu ili wananchi wengi waweze kufaidika, hasa wale wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuimarisha huduma za afya kwa wote. Huduma bora za afya ni muhimu kwa ustawi wa jamii. Serikali inaweza kuongeza uwekezaji katika sekta ya afya kwa kuimarisha hospitali, kutoa vifaa na dawa za kutosha, na kuongeza idadi ya wahudumu wa afya.

Mheshimiwa Spika, pia kuhakikisha Watanzania wote wanajiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote, hapa ninaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko Maalum wa Bima ya Afya kwa Wote. Ninashauri katika mfuko huu, kiasi kikubwa kielekezwe kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iwekeze kwenye kutoa elimu ya afya ili isaidie wananchi kuwa na uwezo wa kuzuia magonjwa yanayoweza kuzuilika kwa kuzingatia usafi na lishe bora.

Mheshimiwa Spika, changamoto za afya zinaweza kuwa na fursa ya uboreshaji wa huduma za afya. Changamoto za afya kama vile upungufu wa huduma za afya vijijini na magonjwa yanayoathiri jamii, zinaweza kuwa fursa kwa Tanzania kujenga mfumo wa afya wenye nguvu zaidi. Uwekezaji katika sekta ya afya hasa kwa kutumia teknolojia kama *telemedicine* (matibabu kwa njia ya mtandao) unaweza kusaidia kufikisha huduma za afya kwa watu wa vijijini na kupunguza msongamano katika hospitali.

Mheshimiwa Spika, pia kuanzisha viwanda vya dawa na vifaatiba ndani ya nchi kutasaidia kupunguza gharama za matibabu, kukuza ajira na kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu kama zile za kupambana na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu inayoikabili nchi yetu ni ile ya ukuaji wa kusuasua wa sekta ya utalii. Sekta ya utalii ni mojawapo ya vyanzo vikubwa vya mapato ya Tanzania, lakini changamoto kama vile ukosefu wa miundombinu bora na utangazaji

mdogo wa vivutio vya asili zinazuia maendeleo yake. Hata hivyo, sekta hii ni fursa kubwa ikiwa miundombinu ya barabara, hoteli na huduma za usafiri zitaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuongeza miundombinu hiyo, Tanzania itaweza kuvutia watalii wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi. Pia utangazaji bora wa vivutio vya asili na kitamaduni utasaidia kuongeza idadi ya watalii na kuongeza mapato ya Serikali na ajira kwa wananchi, hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi kupitia matangazo katika ligi kuu za michezo mashuhuri duniani, mashindano ya Kimataifa, mashirika ya ndege, misafara ya utalii, matamasha ya Kimataifa na mitandao mbalimbali ya Kimataifa na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza Sekta ya Utalii, ninaishauri Serikali ya Tanzania ijitahidi kuhakikisha kuwa utalii unakuwa endelevu kwa kuboresha miundombinu, kuboresha huduma za utalii na ukarimu, kutoa mafunzo kwa wenyeji kuhusu utalii wa kitamaduni, kukuza utunzaji wa mazingira, kuimarisha masoko na uhamasishaji wa utalii, kuimarisha sera na sheria za kukuza na kuwekeza kwenye utalii na kuwekeza kwenye utafiti, ubunifu na uvumbuzi wa maeneo mapya ya kitalii.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya nne inayowakabili Watanzania wengi ni ukosefu wa majisafi na salama na huduma za majitaka. Upatikanaji wa majisafi ni changamoto kubwa kwa Watanzania ambapo sehemu kubwa ya wananchi wapo vijijini.

Mheshimiwa Spika, changamoto hii hupelekea magonjwa yanayotokana na maji machafu kama vile kipindupindu na kuhara na hivyo kuathiri afya na maisha ya wananchi, pia upungufu wa huduma za majitaka unasababisha uchafuzi wa mazingira, hali inayozidi kuzorotesha ubora wa maisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwekezaji mkubwa katika sekta ya maji bado ninaishauri Serikali iendelee kuwekeza kikamilifu kwenye miradi ya majisafi kama vile kuchimba visima, mabwawa na kusambaza maji kupitia mifumo ya usafirishaji ya kisasa ikiwemo kuyatibu maji kabla ya kumfikia mtumiaji. Hili likifanikiwa inaweza kuboresha afya na usafi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Majiji, Miji, Manispaa na Halmashauri zinatakiwa kuwekeza katika usafi wa mazingira, jambo litakalosaidia kuboresha maisha ya wananchi na kupunguza magonjwa yanayotokana na uchafuzi wa mazingira na maji. Fursa hii pia itasaidia kuboresha sekta ya afya na kuongeza maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tabia ya wateja kutokulipa bili za maji, ni vyema Serikali ikaweka *pre-paid meters* kwa wateja wote.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tano ni kukosekana kwa huduma bora za ustawi wa jamii. Huduma za ustawi wa jamii, kama vile msaada kwa watu wenye ulemavu, wazee na watoto yatima, zinakosa ufadhili na mipango madhubuti. Watu hawa wanakosa msaada muhimu na kubaki katika hali ngumu ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa huduma hizi za kijamii kunaongeza changamoto za maisha kwa watu walio katika mazingira magumu na kunazidi kudhoofisha ustawi wa jamii kwa ujumla. Huduma za ustawi wa jamii ni muhimu kwa kuimarisha usawa na kuwasaidia watu wote kufikia malengo ya maisha, lakini upungufu wake unazuia maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa, Spika, kwenye kutoa huduma bora za ustawi wa jamii, Serikali na mashirika ya kijamii yanaweza kutoa msaada kwa makundi maalum kama wazee, watu wenye ulemavu na watoto yatima ili kupunguza changamoto za maisha kwa makundi haya yaliyo katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika vituo vya ustawi wa jamii na utoaji wa msaada wa kisaikolojia na kiuchumi kwa watu hawa utasaidia katika kuhakikisha wanapata msaada wanaohitaji kwa ajili ya maisha bora.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa kuongeza pensheni kwa wastaafu wanaolipwa kupitia Hazina kutoka shilingi 100,125.90 hadi shilingi 250,125.90. Ninaishauri Serikali itafakari ili iwalipe pensheni wazee wa Kitanzania ambao hawakuwa kwenye ajira rasmi za Serikalini kama inavyofanyika kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya sita inayowakabili Watanzania katika maeneo mbalimbali ni ubovu wa miundombinu ya barabara. Miundombinu, hususan barabara, ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi kwa sababu inawezesha biashara na kusafirisha bidhaa kutoka mashambani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, changamoto za maisha zinaongezeka kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara, hasa maeneo ya vijijini. Barabara nyingi ni mbovu, hazipitiki wakati wa mvua na hivyo kuwafanya wakulima kushindwa kufikia masoko na kupeleka bidhaa zao. Hali hii hupunguza mapato ya wakulima na biashara za vijijini na hivyo kudumaza uchumi wa wananchi wa vijijini na ule wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuimarisha miundombinu ya barabara ili kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma hizi muhimu. Hii itasaidia kuboresha biashara, kilimo na maisha ya watu, hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyowasilishwa, Serikali imeonesha dhamira ya kuisaidia kimkakati sekta ya kilimo na itatekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ili kuongeza uwezo wa uzalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na ukweli kwamba uduni wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ni mojawapo ya changamoto kubwa ya saba inayowakabili wananchi wa Tanzania. Ingawa kilimo ni uti wa

mgongo wa uchumi wa Tanzania, sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi kama vile ukosefu wa vifaa vya kisasa, upungufu wa pembejeo bora na ukosefu wa masoko yenye uhakika.

Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto ambayo pia ni fursa kwa kubadilisha sekta ya kilimo kuwa kilimo biashara. Kwa kutumia teknolojia za kisasa na mbinu za kilimo endelevu, Tanzania inaweza kuongeza uzalishaji wa mazao na kukuza uchumi wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, programu za kilimo biashara na matumizi ya teknolojia za kisasa kama zile za umwagiliaji, kilimo cha *greenhouse*, matumizi ya mbolea na mbegu bora zinaweza kusaidia wakulima kuongeza tija na kupata masoko ya Kimataifa, hivyo kuongeza pato la Taifa na maisha ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto katika sekta ya kilimo, ninaishauri Serikali kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na kujenga viwanda vidogo kuongeza thamani ya mazao ya wakulima, wafugaji na wavuvi. Ili kuongeza nafasi za ajira na kupunguza umaskini, Serikali inaweza kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kutoa mafunzo na vifaa vya kisasa kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inaweza kutoa mikopo nafuu kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wajasiriamali wadogo ili kusaidia kuongeza uzalishaji. Kukuza kilimo, ufugaji na uvuvi na kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika mazao ya sekta hizi itasaidia kuongeza kipato kwa wakulima, wafugaji na wavuvi na kuinua uchumi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya nane inahusu mabadiliko ya tabianchi na athari za mazingira. Mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kubwa inayowakabili Watanzania kwa sababu inaathiri kilimo, ufugaji na uvuvi ambavyo ni tegemeo kuu la maisha kwa watu wengi.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yameleta athari kama vile ukame, mafuriko na upungufu wa mvua, hali inayosababisha hasara kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Mabadiliko ya tabianchi pia

yanaathiri vyanzo vya maji na kusababisha uharibifu wa mazingira hali ambayo inawafanya wananchi kukosa kipato cha uhakika. Matokeo yake ni kuongezeka kwa umaskini na changamoto nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali inapaswa kushirikiana na mashirika ya Kimataifa ili kuimarisha mipango ya kuhifadhi mazingira na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Hii itasaidia kupunguza athari za ukame, mafuriko na uhaba wa maji ambao huathiri sana sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi pamoja na uchumi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali inashauriwa iongeze kushirikiana na mashirika ya mazingira na jamii katika kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda miti na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira, pia kuhimiza kilimo, ufugaji na uvuvi wa kisasa. Hivyo basi, ni muhimu kusaidia makundi haya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha uhakika wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tisa ni ile ya mila na desturi potofu za kijadi na unyanyasaji na dhuluma za kijinsia kwa wanawake. Mila na desturi za kijadi zimekuwa changamoto kubwa kwa usawa wa kijinsia katika makabila mengi hapa nchini. Mila hizi mara nyingi zinampa mwanaume nafasi ya juu zaidi kuliko mwanamke na hivyo kumnyima mwanamke haki ya kushiriki katika maamuzi ya kifamilia na kijamii.

Mheshimiwa Spika, desturi hizi pia zinahamasisha vitendo vya unyanyasaji kama ndoa za utotoni, ukeketaji, ubaguzi wa kijinsia, ukatili wa nyumbani, ubakaji na unyanyasaji wa kingono mambo ambayo huzuia wanawake na wasichana kupata fursa sawa, kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kuwafanya kuishi kwa uwoga na huwafanya wanawake kukubaliana na nafasi duni katika jamii.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi pia huathiri afya ya akili na kimwili za waathirika na huzuia juhudi za kufikia usawa wa kijinsia.

Ninaishauri Serikali iendelee kuimarisha elimu ya haki za kijinsia na uhamasishaji katika jamii kwa kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa usawa wa kijinsia na kuondoa mitazamo hasi kuhusu nafasi za jinsia. Uhamasishaji wa kijamii utasaidia kubadili mawazo ya jadi na kuondoa desturi zinazokandamiza wanawake.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni vyema Serikali iweke sera na sheria zitakazosaidia kufikia usawa wa kijinsia hasa katika ajira, elimu na afya. Sheria kandamizi dhidi ya wanawake zinapaswa kubadilishwa ili kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wana haki sawa katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuwashirikisha wanaume katika juhudi na hatua zote za kukuza usawa wa kijinsia. Katika hili, wanaume wanapaswa kushirikiana na wadau wahusika katika juhudi za kufikia usawa wa kijinsia. Wanaume wanapaswa kuhamasishwa kuhusu haki za kijinsia na kushiriki katika kubadili mtazamo wa kijamii ili kusaidia kuondoa ubaguzi wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe kwa kusema kwamba ulipaji kodi ni muhimu ili kulijenga Taifa letu. Vilevile changamoto za maisha kwa Watanzania ni nyingi na zinahitaji hatua za makusudi na ushirikiano wa Serikali na wadau wote wa maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana, Serikali, sekta binafsi, wadau wengine wa maendeleo na jamii wanaweza kutumia changamoto hizi kama njia ya kuboresha maisha ya wananchi na kukuza uchumi wao na ule wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, ninaunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji wa Ilani ya

Uchaguzi kwa kiwango cha juu. Pia, ninawapongeza Mheshimiwa Waziri Fedha na Naibu wake kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kusimamia Wizara kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia, ninaipongeza sana Serikali yetu ya CCM kwa maendeleo makubwa sana yaliyofanyika kwa sekta zote. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuongeza bajeti katika sekta za uzalishaji, sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo imekua na zinaleta tija. Ninaipongeza sana Serikali yetu kwa kusamehe kodi na tozo mbalimbali zitakazokwenda kumsaidia mwananchi wa chini kuongeza kipato chake kupitia shughuli anazozifanya za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, wananchi tunajionea mabadiliko makubwa katika sekta za miundombinu, afya, elimu, maji mawasiliano, usafiri, michezo, utamaduni na kadhalika. Watanzania tuna kila sababu ya kumchagua kwa kishindo kikubwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Oktoba 2025. Mama Samia mitano tena. Mwenyezi Mungu ampe afya njema na maisha marefu, amini na ahsante.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Mungu kwa wema wake kwa miaka mitano niliyokaa Bungeni na kunipa uwezo wa kufanya kazi na wananchi wa Jimboni Temeke, pia kuniwezesha kushirikiana na Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana wewe na wasaidizi wako wote kwa kazi nzuri kwa muda wote wa Bunge hili. Pia, ninapenda kumshukuru Mungu sana kwa ajili ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana katika nchi yetu nzima, kazi nzuri yenye tija kwa nchi yetu. Mungu ambariki sana. Ninaomba nimshukuru Rais kwa kazi kubwa ndani ya jimbo langu la Temeke.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, nimepata vituo vitatu vya afya. Kabla ya hapo, tulikuwa hatuna zahanati, zimeongeza zaidi ya nne, na tayari zahanati mbili zinaendelea. Nikiri, vifaa vyote vya kitabibu vimeingia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, ninamshukuru Rais kwa shule za msingi na madarasa lukuki yameongezeka. Hakuna mtoto wa Temeke ambaye haendi shule. Hii kwa Wanatemeke imetufanya kuhakikisha tunahimizana kupeleka watoto wetu shuleni. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa shule za sekondari, zimeongezeka. Kila kata imepata shule ya sekondari, kata 13; mbili zilikuwa bado, lakini mwezi wa Mei, 2025 tumepokea fedha ya sekondari ya Kata ya Makangarawe na Sekondari ya Chang'ombe na zote hizi ni majengo ya ghorofa. Pia, sekondari yetu ya Yombo Vituka tayari tunayo shule ya ghorofa, madarasa 32). Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, tunashukuru sana, tunasema ahsante Rais Samia. Barabara za *TARURA* tumepata nyingi na tunasema ni barabara kama mgongo wa ngisi, zinateleza. Mradi wa *DMDP* umetufikia na barabara zimeanza kutengenezwa pamoja na vivuko kutoka kata moja kwenda kata nyingine. Hakika tunasema tumefaidika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko, tunashukuru masoko yetu ya Sterio na Tandika, tumepata fedha za kuyakarabati na mengine yako katika michakato ya kuyaendeleza katika kuyakarabati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umeme, Temeke mwanzoni tulikuwa na shida, lakini nimeshukuru kwa sasa umeme kukatika Temeke ni kwa nadra, na ni pale nguzo zinapobadilishwa kwa kuimarisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, tumetokea 55% na kwa sasa tuko 89%. Hakika tunashukuru sana kwa Serikali iliyoko chini ya Rais Samia. Deni kubwa anatudai Wanatemeke Oktoba ni kutia tiki kubwa.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri wote walioshiriki kutengeneza bajeti ya wananchi. Hongereni sana kwani imegusa kila kona ya mwananchi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaenda sasa kwenye orodha ambayo imeletwa na upande wa Serikali ili nao waanze kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi ambaye ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Dennis Londo ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja za Serikali kuhusu mpango wa Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ikiakisi Ilani ya Chama Tawala ya Mwaka 2025 pamoja na mikakati ya muda mfupi iliyowekwa katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutuamini mimi na Mheshimiwa Waziri Dkt. Dorothy Gwajima katika kusimamia utekelezaji wa mipango iliyo katika lengo la kuimarisha ustawi wa maendeleo ya jamii. Ninasema Oktoba tunasonga mbele kwa kutiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu, nitumie fursa hii kukupongeza wewe kwa kuendelea kutulinda, kutuongoza pamoja na Naibu wako na Wenyeviti wako ambao wanasimamia Bunge hili katika kuhakikisha linakwenda, linaimarika kwa ajili ya ustawi wa jamii na pia linaimarika kwa ajili ya wananchi wote; katika kusikiliza yale yote ambayo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hakika Mheshimiwa Rais alikuwa ana maono mapana, kwani alikuwa na maamuzi haya ya kuiwezesha Wizara kupambana kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio ili kuimarisha maendeleo ya ustawi wa jamii pamoja na kupelekea kupata ufanisi katika utekelezaji wa afua mbalimbali za kuimarisha ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii mwanzo ilikuwa katika Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Wizara hii hapo mwanzo ilikuwa haisikiki, kwa sababu Wizara hii iko ndani ya nafsi za watu. Hivyo ni lazima mtu

lile suala limfike ndipo ataona umuhimu wa Wizara hii. Kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake.

Mheshimiwa Spika, hapo mwanzo tulikuwa tunapata fedha. Kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 tulikuwa tunapata takribani shilingi bilioni 43.6, lakini baada ya Mheshimiwa Rais kuuona umuhimu wa Wizara hii, hivi sasa bajeti hii imeongezeka, ambapo tunapata fedha takribani shilingi bilioni 76.57 iliyotengwa na kupitishwa na Bunge lako hili Tukufu, kwa mwaka huu wa 2025/2026, ambayo ni sawa na 74%. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu sasa hivi wananchi wameanza kuelewa Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni nini?

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kufikia mafanikio mengi ambayo ni pamoja na kuundwa na kitengo maalumu kinachoratibu na kusimamia wafanyabiashara ndogo ndogo; mama lishe, mama ntilie na wanaoshona. Mheshimiwa Rais alitoa fursa hii kwa wananchi mbalimbali ambao hawana uwezo wa kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 10.1 kwa ajili ya wafanyabishara ndogo ndogo kuhakikisha wananchi wake wanapata uwezo na kujiendesha kimaisha. Mheshimiwa Rais akaona sivyo, kila mkoa akatoa fedha shilingi milioni 10 kwa ajili ya Ofisi ya Wafanyabiashara Ndogo ndogo katika nchi hii. Tumpongezeni sana Mheshimiwa Rais kwa kujali sana wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Mheshimiwa Rais kaunda majukwaa ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi lenye lengo la kuwawezesha kupata mitaji mbalimbali katika elimu na kutoa masoko, kujengea uwezo wanawake katika nyanja mbalimbali za ujasiriamali, kuratibu uongozi, na kufuatilia tathmini ya jitihada za uwezeshaji kiuchumi na wanawake; kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika uchumi wa Taifa na kuimarisha majukwaa kwa Wizara na ameunda kamati za uhamasishaji waundaji wa majukwaa hayo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameona umuhimu wa Wizara hii na wanatakiwa watoe maoni yao ili yaweze kufanyiwa kazi katika Wizara hii ili malengo yao ambayo wamekusudia katika mioyo yao na katika maisha yao, basi yaweze kufanyiwa kazi kutokana na

majukwaa haya ya uwezeshaji ambayo Mheshimiwa Rais ametuwezesha na kutuelekeza kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kuimarisha ulinzi wa wanawake watoto kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Kupitia utekelezaji wa mpango huu, uwezeshaji wa kupungua vitendo vya ukatili; tulikuwa tuna vitendo vingi sana vya ukatili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anaposimama majukwaani anasikitika kuona vitendo hivi vya ukatili vikiendelea, lakini kutokana na jitihada zake na Serikali hii ya Awamu ya Sita anayoiongoza, jitihada hizo zimefanyika kupitia Maafisa wetu wa Jamii, ambao Mheshimiwa Rais katika mwaka wa fedha huu 2024/2025 ametuwezesha kuwaajiri 178, wasaidizi 176 na kwa jumla Maafisa wa Ustawi wa Jamii wote Tanzania nzima kwa hivi sasa tunao 2,328. Kwa maana hiyo vitendo hivi vya ukatili vimeanza kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukatili wa kimwili kwa wanawake umepungua kutoka 40% kwa mwaka 2015/2016 hadi 27% kwa mwaka 2022. Kwa watoto wa kike, ukatili wa kingono umepungua kutoka 33% kwa mwaka 2009 kwa 11% kwa mwaka 2024. Kwa ukatili wa kimwili umepungua kutoka 76% kwa mwaka 2009 hadi 24% kwa mwaka 2024. Kwa upande wa watoto wa kiume, ukatili wa kingono umepungua kutoka 21% kwa mwaka 2009 hadi asilimia tano; na ukatili wa kimwili umepungua kutoka 74% kwa mwaka 2009 hadi 21% kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, hizi zote ni jitihada za Mheshimiwa Rais kuwaongeza Maafisa Ustawi wa Jamii hawa na kufanya kazi hii kwa juhudi zao kuhakikisha wananchi wa Tanzania wote wanakuwa salama na wanaondokana na changamoto zote za ukatili wa kijinsia katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni mengi na matokeo ya uwekezaji wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan siyo ya kisekta tu, bali ni kati ya sekta nyingi kama za huduma za kijamii za uzalishaji ikiwemo fursa za kifedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imetengewa shilingi bilioni 76.57 kutekeleza vipaumbele mbalimbali kama Wizara, kwa ajili ya kukuza ari za jamiii, kuratibu, kuimarisha ngazi za misingi na kutambua na kuratibu maendeleo ya ustawi na makundi maalumu. Kuboresha mazingira ya maendeleo ya ufundishaji na taasisi mbalimbali, pia, kuimarisha ushiriki wa mchango wa mashirika yasiyo ya Serikali katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha mchango wangu huu ninapenda nitoe rai kwa wananchi wote kujitokeza kutumia fursa hizi ambazo Mheshimiwa Rais ameziweka na kuzifanyia kazi. Mheshimiwa Rais katika upande wa wazee anajali sana wazee na anataka kuhakikisha kwamba wazee wote wanakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anatoa fedha, shilingi milioni 118 kila mwezi kwa ajili ya huduma za msingi za wazee ambao wapo katika vituo vyetu vya malezi na makuzi ya wazee na anahakikisha kwamba wanapata huduma mbalimbali. Kwa mwaka, fedha hizo ni sawasawa na shilingi 1,416,000,000.00. Wazee hawa wapo vizuri, wanapata ulinzi na usalama, maisha yao yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwasisitize wananchi wote kulinda wazee. Huduma za wazee siyo za Serikali peke yake, kila mmoja ana mzee na mzee ndio aliyemlea. Kwa hiyo, niwaombe Wabunge wenzangu tunapotoka hapa kutoa elimu kwa wananchi wote kuhakikisha wazee wao wanawalea na wanakuwa salama, wanaondokana na changamoto.

Mheshimiwa Spika, kumpeleka mzee katika kituo cha wazee, ile inakuwa ni hatua kubwa sana ambayo mzee yule hana mtu wa kumlea wala mtu wa kumwelekeza na kumpatia huduma za ustawi. Mheshimiwa Rais analifanya hilo na tunamwona ni hodari wa kuwatembelea wazee, hasa wale ambao wametokana na siasa.

Mheshimiwa Spika, wale ambao wamefiwa na viongozi wetu mbalimbali, ikifika muda Mheshimiwa Rais anapopata nafasi, basi yeye anachukua fursa hii kuwatembelea na kuwafariji. Sisi basi tukiwa

kama wananchi, tuhakikishe tunafanya kazi hiyo ili wazee wetu wapate kuimarika na kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mikopo ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais kupitia Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii. Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa uratibu mbalimbali ambao unatolewa kwa kupitia wananchi, tulikuwa tunatoa fedha hizi kwa ajili ya kuwakopesha wananchi, lakini sasa tumeweka miongozo mizuri ambayo inawafanya wananchi kupata fedha zile kupitia mikoa na halmashauri zao ambapo elimu hii inatolewa na Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na 2024/2025 Wizara imetoa mikopo ya shilingi 700,500,000,000.00. Wizara inawasisitiza wananchi kwamba, wanapopata mikopo hii waweze kuirejesha ili wananchi wengine waweze kupata fursa hii kwa sababu wasiporejesha kwa wakati, mikopo ile basi wananchi wengine wanakosa fursa ambazo amezitoa Mheshimiwa Rais. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais ametuelekeza fedha hizi sasa, mikopo hii tuelekeze katika sekta za taasisi za benki. Mikopo hii taratibu zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, niwaombe wananchi waende katika halmashauri zao kupata elimu hii na kupata fursa ambazo anazitoa Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais anajali sana wananchi wake, anawapenda sana wananchi wake kuhakikisha kila mmoja anapata fursa muhimu ambayo inamwezesha katika maisha yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, ninapenda kukushukuru na kukupongeza wewe na Waheshimiwa Wabunge wote ambao nilianza nao kutoka 2020 hadi leo 2025 kwa kunipatia upendo, kunionesha imani na fursa mbalimbali za kuniwezesha. Ninawashukuru sana maana nilikuja hapa nikiwa mgeni wa Bunge hili, lakini sasa nimeshakuwa mwenyeji.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wote ambao labda nimewakosea, ninaomba basi wanisamehe katika mwaka huu ili tunapokwenda tuweze kupata fursa na kuweza kurejea tena katika uchaguzi ambao tunauendea. Niwaombee heri Wabunge wote ambao wanaenda

kutafuta fursa nyingine ya kurejea kwenye Bunge hili, basi warudi kwa salama na amani na tukutane tena 2025 – 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwatakie kila la heri katika uchaguzi ambao unakwenda. Ninaamini Oktoba, 2025 tunaenda kumpatia tiki Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hakuna Rais mwingine kama sio Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Rais huyu ni mwanamke na wanawake tunaweza.

Mheshimiwa Spika, mwanamke huyu ameleta maendeleo mengi sana katika nchi hii. Hakuna mwaka wowote uliopita maendeleo yalifanyika kama kipindi hiki cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mama huyu ni shupavu, mahiri, mzalendo, mnyenyekevu na mwenye imani na pia msikivu kwa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mama huyu ukimwendea kwa maendeleo, basi yeye yupo mbele katika kuleta maendeleo hasa katika ustawi wa jamii. Kwa hiyo, wananchi wote tukahakikishe kwamba Oktoba, 2025 tunatiki kumchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atatuongoza na kutuletea maendeleo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaona muda unakwenda na kengele zinaanza kugonga. Baada ya kusema hayo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Umeshaisha Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Ninawapenda sana, ninawajali sana, tutakiane kila la heri ikiwa hii leo ni hitimisho letu kwa upande wa Wizara, basi tuna imani wananchi na Wabunge wote Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii ipo milango wazi kuhakikisha ustawi na huduma zenu. Wizara inafanya yale yote ambayo Mheshimiwa Rais ametuelekeza ili kuleta ustawi, umuhimu na uongozi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana kwa upendo na kujali. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea kuchangia, maana orodha ni ndefu kidogo na tuna leo, kesho ni wachache sana watakaopata nafasi ya kuchangia. Niwaombe tuisikilize kengele kwa sababu pia haitakuwa busara kwa Spika kukukatisha wakati unazungumza habari za Mheshimiwa Rais.

Aidha, panga mchango wako; ya Rais sema mwanzo ili mwishoni unirahisishie kukukatisha. Sasa ukiyachukua ukayaweka mwisho, unanipatia wakati mgumu kidogo. Kwa hiyo, niwaombe wale mnaochangia sikilizeni kengele. *(Makofi/Kicheko)*

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dustan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Londo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim, ambaye ameturuzuku uhai.

Mheshimiwa Spika, pili, nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa uongozi wake madhubuti, maono yake na dhamira ya dhati katika kuhakikisha sekta ya maliasili na utalii inaimarika, maliasili zinatunzwa ili ziweze kunufaisha kizazi cha sasa na kifuatacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nielezee kwa ufupi mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kupitia hii Serikali ya Awamu ya Sita. Wote ni mashahidi katika kipindi cha uongozi wa Awamu ya Sita tumeshuhudia mafanikio makubwa. Tumeshuhudia ongezeko kubwa la watalii waliotembelea nchi yetu. Tumeona idadi ya watalii ikipanda kutoka watalii milioni 1.7 mwaka 2021 hadi kufikia watalii milioni 5.3

mwaka 2024. Ikiwa ni ongezekola 117.2% zaidi ya matakwa ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ongezeko hili wenzetu duniani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii limeitambua Tanzania kwamba ni kinara wa utalii katika Afrika kwa ongezeko la idadi ya watalii. Ukuaji ambao umepatikana ni 48% ikilinganishwa na idadi ya watalii waliokuwa wanaingia nchini wakati wa kipindi kile cha UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ongezeko hili la watalii tumeshuhudia ongezeko la mapato yanayotokana na shughuli za utalii. Mwaka 2021 mapato yetu yalikuwa dola bilioni 1.3. mwaka 2024 kwa kazi kubwa iliyofanyika na Serikali ya Awamu ya Sita mapato yameongezeka kufikia dola bilioni 3.9 sawa na ongezeko la 200% kwa watalii wanaotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa watalii wa ndani, na hapa ninataka nitumie fursa hii kuwapongeza sana Watanzania kwa mwitikio mkubwa wa utalii wa ndani. Mwaka 2021 mapato yetu yanayotokana na utalii wa ndani yalikuwa shilingi bilioni 46.3.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024 mapato ya utalii wa ndani yameongezeka kufikia shilingi bilioni 209.8 sawa na ongezeko la 353.1%. Hongera sana kwa Watanzania kwa kuitikia wito huu. Mafanikio haya ya ongezeko la utalii yameifanya Tanzania kushika nafasi ya tisa duniani na nafasi ya tatu katika Bara la Afrika kwa ongezeko la mapato katika sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya na kazi kubwa iliyofanyika imeifanya Tanzania kung'ara Kimataifa. Leo hii tunapozungumza, mwaka 2024 Tanzania ilipewa tuzo ya kuwa ni eneo linaoongoza kwa Utalii wa Safari Duniani *(World Leading Safari Destination 2024)*.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, Tanzania ikapata *award* nyingine ya kuwa eneo linalovutia zaidi kiutalii katika Afrika. Hifadhi yetu ya Serengeti ikapata tuzo ya kuwa Hifadhi Bora Duniani na hii imekwenda kwa miaka sita mfululizo. Mlima Kilimanjaro umepata tuzo ya kuwa kivutio bora cha utalii Barani Afrika. Kama haitoshi, Bodi yetu

ya Utalii imepata tuzo ya kuwa Bodi Bora katika sekta ya utalii katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na tuzo hizo, *TANAPA* imepata tuzo kwa miaka sita mfululizo ya kutoa huduma kwa kiwango cha Kimataifa. Tuzo hii inatolewa na Taasisi ya *European Society for Quality Research* ambayo ipo kule Bara la Ulaya.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi na mafanikio haya yamekuwa chachu ya kuifanya Tanzania kupewa heshima ya kuandaa Tuzo za *World Tours Travel Award* kwa Ukanda wa Afrika. Tuzo ambazo zinafanyika Dar es Salaam tarehe 28 mwezi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na jitihada hizo, lakini uhifadhi haukuachwa nyuma. Kazi kubwa imefanyika kwenye uhifadhi kuhakikisha kwamba tunalinda rasilimali zetu. Matokeo ya kazi kubwa zilizofanyika katika uhifadhi leo hii Tanzania inaongoza katika Bara la Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya simba.

Mheshimiwa Spika, tunao simba takribani 17,000. Vilevile, tumeweza kuhifadhi nyati, tunaongoza kwa kuwa nchi ya kwanza Barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya nyati. Tunao nyati 225,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, mnyama chui tunaongoza katika Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya chui. Leo hii tunao chui 24,000. Hata kwa mnyama ambaye amekuwa na tishio la kutoweka faru Weusi, tulikuwa na faru 163 tu, leo hii ninafurahi kusema tunao faru 263 sawa na ongezeko la 61%. Hii inaonesha jinsi ambavyo kazi ya uhifadhi imefanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tumefanya vizuri ni kwenye kuimarisha biashara ya mazao ya misitu. Tanzania kwa mwaka uliopita tumeweza kuwa na mapato ya shilingi bilioni 458.4 yanayotokana na uuzaji wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, mwaka 2024 nchi yetu imeweza kuingia makubaliano ya kimkakati na soko kubwa la

manunuzi ya asali, nchi ya China, ambayo kwa mwaka wao wanahitaji tani milioni 38. Leo hii asali yote inayozalishwa Tanzania ina uwezo wa kuuzwa katika soko hili.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Watanzania, tujikite kwenye ufugaji wa nyuki. Fursa ya kupata soko ni ya uhakika, Serikali imeshafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa mapana sana ni eneo la kuhakikisha kwamba tunalinda uhai wa Watanzania kuondokana na migogoro ya wanyamapori wakali na waharibifu. Kazi kubwa imefanyika kujenga mabwawa kwenye hifadhi kuhakikisha wanyama hawatoki hifadhini kwenda kwenye maeneo ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, tumetumia teknolojia za kisasa; ndege nyuki, kufunga mikanda kwenye makundi ya tembo na kadhalika. Vilevile tumekuja na teknolojia ya mabomu baridi kwa ajili ya kutusaidia kufukuza tembo.

Mheshimiwa Spika, kazi hii imefanyika, lakini Bunge hili limeitaka Serikali ifanye zaidi. Nafurahi kusema katika mwaka huu wa fedha Bunge hili limetuidhinishia zaidi ya shilingi bilioni 48 zitumike kwa ajili ya kupambana na changamoto hii ya wanyama wakali na waharibifu. Fedha hizi tunaenda kuzielekeza katika maeneo yatakayotusaidia kuepusha migogoro hii. Katika mwaka ujao wa fedha tunaenda kununua helikopta mbili zitakazotusaidia katika udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha unaokuja tunaenda kununua ndege nyuki 26 ili tuweze kupambana na tatizo hili. Vile vile tunaenda kununua mikanda 50 ya mawasiliano tutakayoifunga kwa wanyama waharibifu hasa tembo. Katika mwaka ujao wa fedha pia tunaenda kununua mabomu 40,000 ili yaweze kusambazwa katika maeneo yenye changamoto.

Mheshimiwa Spika, tunaenda kujenga mabwawa 12 kwenye maeneo ya hifadhi zetu, na pia tunaenda kujenga visima 18 kwenye

maeneo ya hifadhi zetu ili kuhakikisha wanyama hawatoki nje ya hifadhi kwenda nje kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge cha kuona umuhimu wa kujenga uzio wa umeme kwenye baadhi ya maeneo yetu. Katika mwaka wa fedha unaokuja tunaenda kujenga kilometa 53 za uzio wa umeme kwenye eneo la Serengeti, kilometa 38 kutoka Tabora B' mpaka kwenye Mto Mara. Vilevile kule Ngorongoro tunaenda kujenga kilometa 15 kutoka eneo la Lodoare mpaka O'Ideani, vilevile tunajenga vituo 19 vya Askari na vizimba 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda huu ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana. Ninamhakikishia Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, hakuna zuio la wananchi kwenda kufanya matambiko kwenye maeneo yao. Tunachofanya ni utaratibu wa kuomba vibali ili waweze kufanya matambiko yao. Elimu itatolewa kwa maeneo mapya ambayo walikuwa hawajui utaratibu huu. Niwatoe hofu wananchi waendelee na shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, ambao ni viongozi wa CCM kutoka Kibiti wakiongozwa na Moza Iddi Gogomeko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest ambao ni Waandishi wa Habari na marafiki zake kutoka Kyerwa Mkoani Kagera, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 35 wa Mheshimiwa Mohamed Maulid Ali amba ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Leera kutoka Magharibi Zanzibar, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, katika kundi hilo, wapo watoto wawili wa Mheshimiwa Ally Hassan King ambao ni Thuwaiba Ally Hassan King na Thuweini Ally Hassan King. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 67 wa Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ambao ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mlowa kutoka Mkoani Dodoma. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex ambao ni wanafunzi wa Shahada ya Elimu Maalumu na Shahada ya Elimu ya Saikolojia na Walimu wa Watu Wasioona na Viziwi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni 60 wa Taasisi ya Chanzo cha Matumaini Tanzania, CHAMATA kutoka Mikoa mbalimbali, haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 74 na walimu watano wa Shule ya Msingi *Rightway* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 14 na wahadhiri watano kutoka Chuo cha Biblia, *Evangelistic Central Bible College* cha Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Nimejulishwa yupo mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ambaye anaitwa Mudrik Mohamed Rashi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Mheshimiwa Dennis Londo, Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikweke, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DENNIS L. LONDO):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, ambaye imempendeza yeye kwako wewe Spika, Naibu

Spika, Wenyeviti wa Kamati ya Uongozi, kuongoza Bunge letu hili la Bajeti kwa umahiri mkubwa na umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze pia kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza tangu nimepata uteuzi, kukushukuru wewe kwa malezi, usimamizi na uongozi wako katika kipindi chote ambacho niko Bungeni nikiwa kama Mjumbe wa Kamati, Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Mwenyekiti wa Kamati na sasa hivi Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote hiki cha Bunge la Kumi na Mbili ambalo linakamilisha majukumu yake kwa mafanikio makubwa leo, hatuwezi kuacha kukushukuru wewe pamoja na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoelekea kuhitimisha hoja ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti Kuu ya Serikali na Bunge hili la Kumi na Mbili, ninayo furaha kubwa kuwasilisha mchango wangu kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Nje mbele yako na mbele ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, diplomasia ya Tanzania iko vizuri sana na Tanzania chini ya Mwanadiplomasia namba moja ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu iko salama sana Kimataifa na demokrasia yetu upo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna viashiria vingi ambavyo vinaweza vikaonesha jinsi demokrasia ya Tanzania inavyoendelea kung'aa. Idadi ya maombi ya mikutano ya Kimataifa hapa nchini, idadi ya mikutano ya Kimataifa inayoendelea hapa nchini, ziara za viongozi wa Kimataifa kuja hapa nchini, maombi ya ndugu zetu ambao wanaona Tanzania ni sehemu salama ya kufanya mazungumzo yao ya amani, ni viashiria vinavyoonesha kwamba diplomasia yetu iko juu na Serikali ya Tanzania inang'aa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo inaonesha kwamba diplomasia yetu iko vizuri ni pamoja na imani kubwa ambayo Jumuiya ya Kimataifa inaendelea kuwapa Watanzania, chini ya

Jemedari Kiongozi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anaongoza katika kukuza imani ya Watanzania Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe Rais wa *IPU* ni tunda la diplomasia ya Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia tuna Watanzania wengine, Marehemu Dkt. Faustine Ndugulile ambaye alichaguliwa kuwa Mkurugenzi wa *WHO* Kanda ya Afrika, ni kielelezo kingine cha kuonyesha imani ya Jumuiya ya Kimataifa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Dkt. Mohamed Janabi na wenyewe unaonyesha ni jinsi gani Jumuiya ya Kimataifa ina imani na Tanzania. Juzi juzi hapa Dkt. Ntuli Kapologwe naye amechaguliwa kuongoza katika nyanja za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na Watanzania wengine wengi ambao hivi karibuni wamepata imani kubwa kuchaguliwa kuongoza na kubeba dhamana Kimataifa, inaonyesha ni jinsi gani Jumuiya ya Kimataifa ina imani kubwa na nchi yetu, lakini ina imani kubwa na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia ipo katika hali ya sintofahamu. Machafuko yanayoendelea maeneo mbalimbali yanaifanya nchi yetu kuwa sehemu ya dunia hii. Tanzania siyo kisiwa, ni sehemu ya waathirika wa haya mambo ambayo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, diplomasia ya Tanzania katika historia tumeona ni jinsi gani inavyotimiza majukumu yake katika kuhakikisha kwamba dunia inakuwa ni sehemu ya amani kwa ajili ya mwanadamu kufanya shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana hiyo bado tunaendelea nayo na ndiyo maana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya maelekezo yake, tumekamilisha ndani ya mwaka huu wa fedha, mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Toleo la Mwaka 2024, na mkakati wa utekelezaji wake kama sehemu ya

utekelezaji wa ahadi ambayo aliitoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya Bunge lako mwezi April, mwaka 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera hii inaweka msisitizo katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi ikiwemo upatikanaji wa masoko ya bidhaa za nje ya nchi, kutangaza na kuvutia fursa za uwekezaji, utalii, fursa za Uchumi wa Bluu, kuimarisha ushiriki wa *Diaspora* katika maendeleo ya Taifa, matumizi ya Kiswahili kwa manufaa ya kiuchumi, usawa wa kijinsia, na fursa kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Mambo ya Nje ni mwendelezo wa Sera yetu ya Ndani. Sera ya Mambo ya Nje ni jitihada za Watanzania ambao wanaongozwa na sera hii katika kutafuta majawabu ya changamoto zetu za ndani, kwa kutafuta fursa ambazo zinatokana na maeneo mbalimbali duniani, sekta mbalimbali duniani kutoa majibu ya changamoto zetu ndani ya nchi, ikiwemo ajira, uwekezaji, utalii, na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, katika hali hii kuimarika kwa ushirikiano wa uwili kati ya Tanzania na Mataifa mengine, ambapo pamoja na mambo mengine Tanzania imejaribu kushiriki katika mikutano 42 ya Kimataifa pamoja na Tume za Kudumu za Ushirikiano, *JPC*, na mashauriano ya Kisiasa kati ya Tanzania na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mathalan, kupitia ziara hizo Tanzania imefanikiwa kusaini mikataba na hati za makubaliano 51, katika kipindi cha mwaka huu wa fedha pekee. Haya yote ni utekelezaji ambao unachochea utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi katika Sekta mbalimbali zenye manufaa ya kiuchumi, kisiasa, kijamii kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba, Sera yetu ya Nje ni mwendelezo wa mikakati yetu ya ndani kutafuta fursa duniani za kuendeleza ama kutafuta majawabu ya changamoto ya ndani. Hivyo, baadhi ya mafanikio ya kisekta ambayo yanapatikana na hapa nchini kama reli ya kisasa *SGR*, upatikanaji wa fursa za masomo kwa vijana wetu nje ya nchi, kuongezeka kwa safari za

ndege yetu ya *ATCL* nje, upatikanaji wa masoko ya bidhaa zetu, na ongezeko la watalii, yamewezeshwa kwa juhudi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kubwa kuliko yote ni jinsi gani wapiganaji wetu katika Balozi zetu mbalimbali wanavyotimiza wajibu wao kuhakikisha kwamba Tanzania inafaidika na fursa ambazo dunia inatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba, bado dunia iko kwenye sintofahamu kutokana na machafuko ambayo yanaendelea katika sehemu mbalimbali. Hivi sasa familia nyingi katika nchi yetu ambao wana ndugu, jamaa, au marafiki katika nchi za Israeli na Irani wako katika sintofahamu, hawajui hatma ya Watanzania ambao wako huko.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nilijulishe Bunge lako kuwa tuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo yanaelekeza Wizara yangu. Chini ya maelekezo hayo, Wizara ya Mambo ya Nje inaendelea kuratibu zoezi la kuwarejesha nchini Watanzania kutoka nchi za Israeli na Irani kufuatia kudorora kwa hali ya amani Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na jumla ya Watanzania 168 nchini Irani na 495 nchini Israeli. Hadi sasa Serikali imewezesha kurudisha Watanzania 107; 42 kutoka nchini Israeli na 65 kutoka Nchi ya Irani, kuondoka kutokana na hatari na kuanza safari ya kurejea nchini na maeneo mengine ya kiusalama. Juhudi hizi zinatekelezwa kwa uratibu wa Wizara na Balozi zetu *Tel Aviv*, *Cairo*, *Ankara*, *Kuwait*, na *Abu Dhabi*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yetu kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anarejea nchini salama. Aidha, Tanzania inalaani migogoro inayoendelea na inasisitiza umuhimu wa kushughulikia changamoto mbalimbali kwa njia ya kidiplomasia na kwa kuzingatia makubaliano katika Umoja wa Mataifa na sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa ushirikiano wetu wa Kikanda ambapo Tanzania imechangia kushiriki katika Mtangamano wa

Kikanda, hususan utekelezaji wa soko la pamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na utekelezaji programu za Mtangamano katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kiuchumi, *SADC*, na ushirikiano wa utatu kwa maana ya *SADC*, *EAC*, na *COMESA*, na Eneo Huru la Biashara Afrika.

Mheshimiwa Spika, tuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo tumeanza kuyatekeleza. Tumekuwa katika mazungumzo na Wizara ya Biashara katika bajeti hii. Tunaenda kuendelea na mazungumzo na Wizara ya TAMISEMI kuhakikisha kwamba mikoa na halmashauri zote ambazo zinapakana na wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanaenda kuwezeshwa kushiriki kikamilifu katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuimarika kwa ushirikiano wa Kimataifa ambapo Tanzania kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumefanikiwa kuongoza ajenda kubwa za kimkakati duniani ikiwemo kusimamia suala la matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia hususan kwa akina mama Barani Afrika, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, na kushiriki kikamilifu katika kusuluhisha migogoro ya ulinzi wa amani kupitia juhudi za Kikanda na Umoja wa Mataifa kama hatua muhimu katika kufikia malengo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa Diplomasia ya Uchumi ambapo Wizara yetu imewezesha na kufanikisha ziara za kimkakati za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nchini na viongozi wa Kimataifa wengine kuja nchini, ziara hizi ni kielelezo cha kukubalika kwa diplomasia yetu Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ingawa siyo kwa umuhimu, tunashukuru kwa Bunge lako kupitisha bajeti ya Wizara yetu kwa ongezeko la 30% katika bajeti ya maendeleo. Ongezeko hili ni ongezeko kubwa ambalo litawezesha Serikali, Wizara yetu kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa tija na ufanisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. DENNIS L. LONDO):** Mheshimiwa Spika, pia tumepata ajira mpya 71. Kulikuwa na kilio kikubwa cha Wabunge kuona kwamba kuna ongezeko la watumishi ndani ya Wizara. Ongezeko hili linaenda kutekeleza kwa umakini diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa maelezo hayo kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Waziri wa Madini ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa sana Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, awali ya yote naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Neema, aliyenijaalia mimi kuwa na afya njema pamoja na sote humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, kabla sijaanza kuchangia, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini mimi kuwa Waziri katika Wizara hii; pili kunipa nafasi nikishirikiana na nikiongozwa na Waziri Mkuu kuweza kutimiza majukumu ambayo ametupangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka pia kabla sijakwenda mbali nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ziara yake nzuri aliyoifanya juzi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kwa kweli, imeleta faraja kubwa sana, lakini ninampongeza zaidi kwa kulimaliza Daraja la Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, ambalo kwa kweli ni alama ya kipekee katika Mikoa ya Mwanza, Geita na maeneo yote ya Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nikushukuru wewe na kukupongeza kwa kazi nzuri kama ambavyo wenzangu wameeleza, lakini kwa upekee kabisa kwa jinsi ambavyo umetuongoza na

umekuwa msaada mkubwa sana kwa Wizara na Serikali yetu kwa jumla. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, kabla sijaingia kwenye kueleza na yale ambayo nimepanga kufafanua katika Bunge lako, nitumie nafasi hii ya kipekee kabisa kuwashukuru sana wananchi wa Chalinze.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Chalinze walinipa heshima ya kuja kwenye jengo hili katika kipindi cha miaka mitano ambayo inakwenda kwisha wiki hii. Kwa kweli katika kipindi chote cha miaka mitano, najua yapo mazuri tumeyafanya, upo upungufu ulioonekana, lakini ninawahakikishia kwamba upungufu ni kwa sababu sisi ni binadamu, lakini mazuri yote tunafanya kwa heshima kubwa ambayo wao wametupatia.

Mheshimiwa Spika, pia ninataka niwaambie tu kwamba Jumamosi nitakwenda kwenye Ofisi za Chama cha Mapinduzi kuomba tena ile karatasi ili sasa waweze kunipa miaka mingine mitano ya kuweza kufanya kazi pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, ninaomba sasa nijibu baadhi ya hoja ambazo zimeelezwa na Wabunge wako na baada ya kujibu hoja hizo pia nitaomba unipe nafasi kwa uchache wa dakika zitakazokuwa zimebakia niwaeleze yale ambayo tumeyafanya ndani ya Wizara yako katika kipindi cha miaka mitano inayokwenda kwisha wiki hii mwishoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Ndakidemi alichangia mchango wake akishauri Serikali kulipa mafao ya uzeeni kwa wazee ambao hawana mafao kama wanavyofanya kwa upande wa Zanzibar. Serikali imesikia wazo lake na kwamba hilo wazo malipo yake tunaangalia kutokana na uwezo wa uhimilivu wa mifuko yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama fursa itapatikana ninataka nikuhakikishie wewe na Mheshimiwa Mbunge, kwamba hilo nalo tutaliangalia, lakini kwa sasa hivi ninataka nieleze tu ni dhamira ya

dhati ya Serikali kuhakikisha kuwa wazee wote nchini wanalipwa pensheni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yeye, pia Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, ameeleza hitaji la Serikali kuunda mkakati mahususi kwa ajili ya kutatua changamoto ya ajira kwa vijana. Serikali imefanya mambo mengi sana na mikakati mingi sana katika kutatua changamoto ya ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na mabadiliko mbalimbali ya sheria ambayo Bunge lako limepitisha ikiwemo sheria ile ya Manunuzi ya Umma ambayo Bunge lako lilielekeza Serikali itenge 30% ambazo makundi maalum ya vijana, wakina mama na wenye ulemavu watayakimbilia ili waweze kupata fedha hizo na baada ya hapo waweze kujiajiri wenyewe au waweze kufanya kazi zile ambazo zitawaingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa Arusha kwenye Mkutano ambao hili suala la mgawanyo wa 30% zinazotoka kwenye manunuzi, nalo pia tulijadili sana. Furaha yangu kubwa ni kwamba fedha hizi zimeendelea kutengwa na watu wameendelea kuzikimbilia japo kweli ni kwamba elimu inatakiwa iendelee kutolewa ili wafaidika ambao wamelengwa waendelee kuzikimbilia fursa hizi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, programu mbalimbali ikiwemo programu za kukuza ujuzi na ujenzi wa miundombinu ya kongani za viwanda nazo pia ni moja ya eneo ambalo Serikali imeendelea kuliangalia na kuliwekea msisitizo. Pia, sisi tunaendelea kuwakaribisha wawekezaji wenye nguvu waje kuwekeza, lakini msisitizo mkubwa ni kwamba kwenye *local content* ni lazima izingatiwe.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuanzisha maeneo maalum ya uendelezaji wa ubunifu na teknolojia kama ambavyo mnaona katika vyuo vikuu mbalimbali, lakini pia kwenye maeneo ambayo yametengwa maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba *talent* za vijana au makundi ya vijana zinahakikishwa zinatazamwa; hilo nalo ni moja ya eneo ambalo tumeliangalia.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, yeye alizungumzia juu ya kima cha chini cha pensheni kwa watumishi wastaafu wa zamani. Kama nilivyoeleza, kupanda kwa pensheni hutegemea hali ya uhimilivu wa mifuko. Serikali hufanya tathmini kila baada ya miaka mitatu, na pale inapoona kwamba sasa mfuko unaweza kuwa himilivu, basi inafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hilo Serikali kupitia Mfuko wa Hifandi ya Jamii imepandisha kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000.00 kama ilivyokuwa katika miaka minne ilivyopita na sasa pensheni ipo katika shilingi 150,000.00. Tumefanya hivi kwa mifuko yote miwili ikiwemo Mfuko wa *PSSSF* na *NSSF* na mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, alitoa ushauri kwa Serikali, iweke bunifu mbalimbali kuhakikisha kuwa wasomi wanaohitimu kutoka vyuo vikuu wanaweza kujiajiri ikiwemo kuwapa mitaji. Serikali inaendelea kuhamasisha vijana wahitimu kujiunga na vikundi ili hatimaye waweze kuwezeshwa ikiwemo kupitia 10% zinazotolewa na halmashauri na pia zile 30% ambazo nimeeleza hapo mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika mwaka 2023/2024 mikopo yenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 1.2 ilitolewa kuwezesha miradi 56 ya vijana 392 kupitia Mfuko pia wa Maendeleo ya Vijana ambao Serikali imeendelea kutoa pesa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe alitoa hoja yake kwamba Serikali izingatie mafao ya kuustaafu kwa maprofesa waliokuwa wanafundisha vyuo vikuu katika *formula* za mafao ya wastaafu ambao hawajaguswa ili kuwawezesha wao kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa sheria na miongozo haituambii kutekeleza katika makundi maalum kama haya ya maprofesa, lakini Serikali imeshafanya maboresho ya mafao na kuwa kanuni moja ya ulipaji ya mafao kwa wanachama wote wa mifuko ya *PSSSF* na *NSSF*. Katika ulipaji wa mafao hayo, hakuna vyeo wala wadhifa ili kuwa mwanachama ambaye ni mchangiaji iangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka nilihakikishie Bunge lako kwamba Serikali inaendelea kuangalia mafao ya makundi yote na itakapotokea maelekezo yameletwa ya kuwa tuangalie makundi maalum, basi Serikali yako sikivu itaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, pia ninayo furaha ya kulitaarifu Bunge lako kuwa Serikali kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imepandisha mshahara wa watumishi wa Umma kwa 35.1% kwa mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni katika yale maelezo ya mwanzo niliyoeleza kuwa mifuko yetu imekuwa himilivu, lakini pia tunao uwezo wa kulipa mafao hayo. Kwa hiyo, katika kuelezea uhimilivu wa Mfuko wetu, tunapozungumza sasa hata ukwasi wa mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii nao pia umeongezeka sana. Kwa mfano Mfuko wa *NSSF* tunapozungumza sasa hivi ukwasi wetu umefikia shilingi trilioni 9.3 ambayo ni kubwa zaidi na hili ni ongezeko la 92% ukilinganisha na ukwasi wa shilingi trilioni 4.84 uliokuwepo mwaka 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa sana katika miaka minne ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi kwa kweli ndani ya Wizara ambao tunasimamia mifuko hii ya Hifadhi tunakuwa na maisha mazuri ya kutekeleza majukumu yetu kwa sababu ukwasi huu umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *PSSF* kwa sasa hivi ukwasi unakaribia shilingi trilioni 11 ambapo nalo ni ongezeko kubwa sana la 94% ukilinganisha na ilivyokuwa mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, pia tumeendelea kuratibu na kufanikisha uwezeshaji katika maeneo mbalimbali. Tunapozungumza sasa kwenye eneo la uwekezaji, tumeanzisha Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi ambacho ni mafanikio makubwa sana ikiwa pamoja na uanzishaji wa skimu ya wananchi waliojiajiri wenyewe. Haya yote ni mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, pia tumeweza kukamilisha miongozo mbalimbali ambayo miongozo hiyo inawezesha makundi mbalimbali yakiwemo makundi ya wenye ulemavu, makundi ya vijana nayo pia kuwezeshwa ili waweze kufaidika katika fursa ambazo zinatolewa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, nikitaja kwa uchache, tumetengeneza mwongozo wa teknolojia saidizi ambapo mwongozo huu unalenga kuwezesha kutoa miongozo ya bei elekezi ya teknolojia saidizi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, pamoja na mengineyo mengi niliyokuwa nimejiandaa nayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKIA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, atafuatiwa na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, ajiandae.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuendelea kuchangia hoja hii ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2025/2026 tukiwa na afya na Taifa letu likiwa na amani na mshikamano.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na unyenyekevu, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na mafanikio lukuki katika kuimarisha ulinzi na amani na hivyo kulileteа maendeleo Taifa letu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyokubaliana, hakuna maendeleo bila ya ulinzi imara, imani na mshikamano wa Kitaifa. Pia,

ninamshukuru sana kwa kuniamini na kuwa sehemu ya Baraza lake la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wachangiaji waliotangulia kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi, viwango vya hali ya juu vya Kitaifa na Kimataifa, ukisaidiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, niwapongeze Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ikiwa ni pamoja na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa wanayoifanya na niwapongeze watendaji wote wa Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia katika hoja iliyo mbele yetu hususan masuala yanayohusiana na Sekta ya Ulinzi, ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ziara ya kishindo katika Kanda ya Ziwa; mikoa ya Simiyu na Mwanza. Ziara hiyo imekuwa na mafanikio makubwa sana kiuchumi, kisiasa na hata kiulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ama kweli ziara hii imekonga nyoyo za wananchi wa Simiyu na Mwanza ikiwa ni pamoja na kwetu Magu. Hadi sasa wananchi bado wanaongelea matokeo ya ziara hii ikiwa ni pamoja na miradi mingi iliyotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita, ikiwemo miradi mikubwa ya kimkakati iliyozinduliwa wakati wa ziara hii ikiwa au niseme hususan daraja la kimkakati la John Pombe Magufuli ambalo lina manufaa makubwa sana Kitaifa lakini hata kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziara hii pia imechangia katika kudumisha mila na desturi, imeyaleta makundi maalum pamoja ikiwa ni pamoja na maafisa usafirishaji, pia walinzi wa jadi na kusherehekea tukio ambalo ni muhimu sana katika Kanda ya Ziwa. Ni tukio la mavuno ambalo linajulikana kama Burabo. Wanamwanza tunamshukuru sana sana Mheshimiwa Rais na kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee

kumpa afya njema na maono zaidi na tupo tayari kabisa kutiki Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyowasilishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti Kuu ya Serikali, na kama ilivyo dhamira ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, mipaka ya nchi yetu ipo salama, nchi ina amani na utulivu chini ya uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunu muhimu za Taifa; amani, ulinzi na usalama, zimelindwa; na umoja, mshikamano na utulivu, vimeimarishwa. Hayo yote yamewezekana kutokana na uwekezaji mkubwa au uwezeshaji mkubwa unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiwezesha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeimarishwa kizana, imeimarishwa kivifaa hususan Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, kimafunzo na utaalamu, kiteknolojia na kimaslahi. Katika kipindi hiki cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita, Wizara imepata ongezeko la bajeti la jumla ya 52% toka mwaka 2020/2021 hadi 2025/2026. Hii ni historia haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, Wizara imekamilisha miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa ya kisasa kabisa huko Kikombo - Dodoma. Mradi huu umekamilishwa kwa kutumia wataalamu wa ndani na pesa za ndani kiasi cha shilingi bilioni 70.2. Hii ni heshima kubwa, haya ni makao yetu sisi wenyewe, tumeyajenga wenyewe. Macho ni yetu, masikio ni yetu na yote yaliyomo kule ndani yatabaki kuwa yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitu kikubwa sana cha kujivunia kwamba Taifa linaweza likajenga makao yake ya ulinzi wao kwa kutumia wataalamu wao na fedha zao za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa ya Jeshi la Kanda ya Dodoma ya daraja la nne yenye hadhi ya viwango vya umoja wa Mataifa katika eneo la Msalato Jijini Dodoma imekamilika. Hii itatoa huduma kwa wanajeshi, lakini pia kwa raia. Ipo miradi mingine ambayo imetekelezwa katika kipindi hiki ambayo nilishaitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita pia imetoa uzito mkubwa sana katika kuboresha maslahi ya watumishi hii ikiwa ni pamoja na Makamanda, Maafisa na Maaskari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, pensheni na mafao ya Maafisa na Maaskari imeboreshwa ili kwenda na hali ya sasa ya kiuchumi. Utekelezaji wa maboresho haya utaanza Julai mwaka 2025 katika mwaka wa fedha 2025/2026 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara inamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuwathamini wapiganaji wake kwa kiwango cha hali ya juu, kwani hawa ni watu ambao muda wote wapo macho, usiku na mchana kutulinda sisi na kulilinda Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu, nimhakikishie Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kuwa Jeshi lake lipo imara, linampenda na litamlinda na kuilinda mipaka na uhuru wa nchi yao kama walivyoapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nitoe shukrani kwako wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi walivyowapigania sana maveterani waliopigana vita ya Kagera. Kweli waliwapigania sana sana na kama nilivyoeleza katika Bunge lako Tukufu wakati nikijibu swali hapo tarehe 28 mwezi wa Nne kuwa Wizara imewasilisha mapendekezo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ambayo ni sikivu sana inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imesikia kilio hiki cha muda mrefu sana cha Maveterani waliopigana vita ya Kagera.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango wao mkubwa, Maveterani hao kuanzia Julai, mwaka 2026 wote watalipwa pensheni. Wote wale ambao walikuwa hawalipwi pensheni wataanza kulipwa pensheni kwa kima cha chini cha pensheni ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kiwango hiki kitaendelea kuongezeka kadri viwango hivi vitakavyobadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili limefanyika takribani baada ya miaka 45 tangu vita vya Kagera kumalizika. Huu ni moyo wa upendo wa kipekee na utu wa Mheshimiwa Rais wetu. Binafsi kama Waziri wa Ulinzi na viongozi wenzangu kwa niaba ya Maveterani hawa, hatuna cha kusema zaidi ya kusema ahsante sana sana kwenu ninyi mliowapigania hususan kwa Mheshimiwa Rais aliyesikia kilio hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine makubwa katika Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Ulinzi ni utatuzi wa migogoro ya ardhi. Tulikuwa na mpango wa kutatua migogoro ya ardhi wa miaka minne 2020/2021 – 2024/2025 chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita na tumeweza kutatua migogoro takribani 230 kwa kupima, kuhuisha mipaka, kufanya uthamini na kuweza kulipa fidia ya takribani shilingi 54,130,521,088.00.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki kimelipwa kwa maeneo 61; mawili yakiwa Lindi, sita yakiwa Kagera, matatu Mara, matatu Mwanza, Geita moja, Dodoma Matano, Singida tisa, Kigoma moja, Pwani manane, Kilimanjaro matatu, Tabora manne, Arusha manne, Morogoro matatu, Tanga sita, na Dar es Salaam moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, maeneo 22 yameshafanyiwa uthamini na jumla ya kiasi cha shilingi 60,698,692,315.00 kinatarajiwa kulipwa kwa wananchi kama fidia katika maeneo hayo ambayo nayo yapo katika mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fanikio lingine kubwa limekuwa ni kuimarisha Diplomasia ya Ulinzi. Katika Awamu hii ya Sita, mambo mengi makubwa yamefanywa ambapo kama sehemu ya kuimarisha Diplomasia ya Uchumi, Diplomasia ya Ulinzi haikuachwa nyuma, na

hapa Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa mno kuimarisha ushirikiano wa Kimataifa, kikanda na nchi rafiki katika Sekta ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni imara chini ya Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Basi ninawaomba wote hiyo Oktoba tukakamilishe kazi iliyo mbele yetu ya kutiki kwa Mheshimiwa Rais. Ninawatakia mafanikio wale wote wanaokwenda kugombea, Uyole inakuhitaji sana, tunakuombea na wewe wananchi waone kazi kubwa uliyoifanya na waendelee kukuamini. Baada ya kuyasema hayo, ninatoa shukurani kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano walionipatia wakati wote.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, ajiandae.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote naanza kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyeturuzuku uhai na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu siku hii ya leo tukiwa tunaelekea ukingoni mwa shughuli hizi za Kibunge.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa heshima kubwa aliyonipa kuniteua kuwa Waziri wa Madini na kunipa dhamana hii kubwa ya kusimamia rasilimali za Nchi yetu ya Tanzania. Pili, ninamshukuru sana kwa maono na utayari wake wa kuhakikisha kwamba, sekta ya madini inachangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa ninachukua fursa hii kumshukuru sana Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ambao muda wote wamekuwa wakitoa maelekezo na ushauri mbalimbali ambao umesaidia katika

kuiendeleza na kuikuza sekta ya madini. Kipekee kabisa ninachukua fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Naibu Spika, Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa uliotupa katika kutekeleza yale ambayo yalitupasa kuyafanya kwenye Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani zangu ninaomba sasa nijielekeze katika hoja ambazo zimejadiliwa ndani ya Bunge lako. Katika miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sekta ya madini imepiga hatua kubwa sana na imeendelea kutoa mchango katika uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Sera yetu ya Madini ya Mwaka 2009 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano mitano ulituelekeza ya kwamba, ukifika Mwaka 2025 sekta ya madini inatakiwa iwe inatoa mchango kwenye pato la Taifa kwa 10%. Katika taarifa iliyotolewa na Shirika la Takwimu la Tanzania *(NBS)* sekta ya madini hivi sasa inachangia pato la Taifa kwa 10.1%, ikiwa ni mwaka mmoja kabla ya mwaka wa kimalengo. Haya ni mafanikio makubwa sana chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni akiba ya dhahabu kupitia Benki Kuu. Katika Bara letu la Afrika, Tanzania ni miongoni mwa nchi tano zinazozalisha dhahabu kwa kiwango kikubwa sana, lakini Tanzania haikuwemo katika orodha ya nchi zenye akiba ya dhahabu kupitia Benki Kuu pamoja na kwamba, tuko tano bora kwa uzalishaji wa dhahabu katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais juu ya rasilimali madini tuliyonayo, tulifanya mabadiliko ya Sheria. Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini, Sura ya 123, tulikifanyia marekebisho, ili madini yote yanayozalishwa nchini Tanzania na ambayo yanasafirishwa nje ya nchi yatengwe asilimia isiyopungua 20 na kubaki ndani nchini, kwa ajili ya kuchakatwa, kuyeyushwa, kusafishwa na kufanyiwa biashara ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii iliiwezesha Benki yetu Kuu ya Tanzania ianze kununua dhahabu kupitia 20% inayotengwa. Tarehe Mosi, Oktoba, 2024, Benki Kuu ya Tanzania ilianza kununua dhahabu. Katika Bara la Afrika nchi inayoongoza kwa kuwa na hifadhi kubwa ya dhahabu kupitia Benki Kuu ni Algeria, ina tani 174 na nchi ya 10 bora ni Msumbiji, ina tani 3.984. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho haya ya Sheria, *BOT* ilivyoanza kununua dhahabu mpaka hivi sasa imekwishanunua tani 5.7 ndani ya miezi tisa. Ndani ya muda mfupi ujao, tunakwenda kuongeza kiwango kufikia mpaka tani saba na hivyo kuivuka Msumbiji ambao wamekuwa kwenye 10 bora kwa miaka yote. Tanzania ndani ya miezi nane imeingia kwenye 10 bora, hii ni kuonesha kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 sekta ya madini iliingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 162 tu kwa mwaka mzima. Baada ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Mwaka 2017, ambayo yalianzisha masoko ya madini na vituo vya ununuzi, mapato kupitia sekta ya madini yakaanza kuongezeka. Katika Mwaka wa Fedha uliomalizika, 2024/2025, sekta ya madini imeingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, kama sehemu ya maduhuli, shilingi bilioni 753. Mwaka huu wa Fedha unaoishia 2024/2025 tuliwekewa lengo la kukusanya shilingi trilioni moja kuingiza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya tarehe 30 haijafika, leo ninasimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa heshima na taadhima kubwa kulitaarifu Bunge lako kwamba, Wizara ya Madini imevunja rekodi yake yenyewe. Mpaka siku ya leo tumeshaingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi trilioni 1.1 kabla ya Mwaka wa Fedha haujamalizika. Haya ni mafanikio makubwa sana chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt.Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni uongezaji thamani madini yetu. Kifungu cha 100D cha Sheria ya Madini, Sura ya 123, kinatoa katazo la kusafirisha madini ghafi nje ya nchi. Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kuhakikisha Wizara inasimamia kikamilifu eneo hili. Katika

eneo la kuongeza thamani madini yetu yapo mambo matatu ya haraka; la kwanza ni, tuna viwanda nane hivi sasa vya kusafisha madini ya dhahabu katika Nchi yetu ya Tanzania. Jambo la pili ni, tuna viwanda tisa, vinajengwa maeneo mbalimbali vya kuongeza thamani madini ya metali hasa madini ya shaba na *nickel* ambapo Mkoa wa Dodoma peke yake kuna viwanda saba vipya vinajengwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatupa nafasi ya badala ya kusafirisha jiwe la shaba kulitoa nje, tuna uwezo wa kutengeneza *copper cathode* na *copper loads* ndani ya Nchi yetu ya Tanzania. Haya ni mafanikio makubwa sana chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa Bungeni, ninarudia tena, hivi sasa Serikali tumetoa *statement* ya kwamba, hakuna leseni nyingine yeyote ya madini ya kimkakati itakayotolewa mpaka mwekezaji atuwekee mezani mpango madhubuti wa kuongeza thamani ya madini ndani ya nchi. Vinginevyo hatutatoa tena leseni katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tano, ambalo ninataka nilisemee ni la madini ya kimkakati. Nchi yetu imejaliwa kuwa na madini mengi sana ya kimkakati na hivi sasa tumeona katika eneo hili ni lazima tutengeneze mkakati maalum wa kuweza kusaidia kuyavuna na kuyaendeleza kwa sababu, mahitaji ya madini haya ni makubwa sana duniani. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu tuna miradi mikubwa ambayo inakuja katika eneo hili, lakini kubwa zaidi ni kwamba, hivi sasa tunaweka mkakati maalum wa kuyavuna na kuyaendeleza, ili nchi yetu iweze kunufaika katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, katika moja ya nguzo kwenye mkakati huu ni eneo la uongezaji wa thamani. Ndiyo maana katika eneo la ekari 1,331 pale Buzwagi tumetenga kongani maalum, kwa ajili ya viwanda vya kuongeza thamani madini yetu. Moja kati ya mafanikio makubwa ambayo tutakwenda kuyapata ni Kampuni ya Tembo *Nickel* ambay itakwenda kuchimba *nickel* kule Kabanga; wanajenga kiwanda cha dola milioni 500 pale Kahama cha kuongeza thamani ya madini yetu

ya *nickel,* ambapo tutakuwa tuna uwezo wa kutoa bidhaa ya mwisho kutoka Kahama kuingiza kwenye betri la gari la umeme pasipo kuongeza thamani nyingine yoyote hapa katikati. Hayo ni mafanikio ambayo tumeendelea kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni katika madini ya vito. Tanzania imejaliwa kuwa na madini ya *Tanzanite,* ambayo huyapati kokote kule duniani. Tutarejesha minada ya madini ya *Tanzanite* na maonesho ya kimataifa, ili kuvutia tena madini yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Mkenda na Mheshimiwa Jenista Mhagama, ajiandae.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kuweza kuiona siku hii ya leo. Kipekee kabisa, vilevile, ninatumia nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ahadi yangu kwake ni kwamba, sitamwangusha, nitaendelea kujituma usiku na mchana katika kuhakikisha kwamba, tunaiendeleza sekta nzima ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa maelekezo yao wanayotupatia mara kwa mara, yanayotuwezesha sisi katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa pia, ninakushukuru wewe kwa umahiri wako wa namna ambavyo unaendesha Bunge letu hili Tukufu, lakini vilevile kwa namna ambavyo unatushauri sisi Serikalini na hasa katika sekta ya ardhi ambapo inatuwezesha kuendelea kuboresha

utendaji kazi wetu. Ninakushukuru sana na ninakutakia kila la heri kule Uyole katika uchaguzi wa mwaka huu 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana wenzetu wa Wizara ya Fedha, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Vilevile ninawapongeza sana wenzetu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Manaibu wote wawili, Mheshimiwa Chande na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Ninawapongeza sana kwa wasilisho zuri lililo mbele yetu, lakini pia, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Bajeti Kuu ya Serikali na hasa wale ambao waligusia sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya mambo makubwa katika kuhakikisha kwamba, sekta ya ardhi yanafanyika mageuzi makubwa sana. Katika hayo tumeona hivi karibuni Mheshimiwa Rais mwenyewe akizindua Sera Mpya ya Ardhi ya Mwaka 1995, Toleo la Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi humu walikuwa wakiililia kuhakikisha kwamba, tunapata sera mpya, kama Taifa, ya ardhi. Tayari tumezindua na ni kwa maelekezo yake Mheshimiwa Rais na kwa kuwezesha yeye Wizara ya Ardhi ndiyo tumefikia hapa katika kuhakikisha Sera Mpya ya Ardhi tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini si kwenye sera tu, tunafanya *transformation* kubwa kutoka kwenye *analogue* na sasa kwenda kwenye *digital land management* kwa kuwa na mfumo wa e-Ardhi, ambapo tayari katika mikoa sita tumeweza kusimika mfumo huu. *Data conversion* inaendelea, hapa Dodoma tumekamilisha, Mbeya kule inaendelea, vilevile Mkoa wa Mwanza *data conversion* ndio inakamilika na mpaka ufikapo mwaka 2027 mfumo huu wa e-Ardhi utakuwa umesimikwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa mfumo huu ni kwamba, wananchi wanapata huduma kwa haraka zaidi. Si huduma kwa

haraka zaidi, hata migogoro ya ardhi inakwenda kupungua ama kwisha kabisa kwa kuwa na mfumo huu kwa sababu, kila kitu kitakuwa wazi. Haya ni mafanikio makubwa sana ambayo tunayapata kutokana na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali hii ya Awamu ya Sita imewezesha upatikanaji wa fedha, kwa ajili ya kwenda kuziangalia ramani zetu za msingi na kuweza kuzitengeneza upya. Kuna Dola za Kimarekani milioni 65 ambazo zinakwenda kufanya kazi hii. Kwa nini ramani za msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani zetu za msingi za mwisho kabisa zilitengenezwa mwaka 1970, ambapo kuna miji mingi ambayo haikuwepo, ama ilikuwa ni midogo sana kipindi hicho, ramani hizi za msingi zinachukuliwa. Tuchukulie mfano, pale Mji wa Shelui, Shelui huenda ilikuwa ni kakijiji kadogo sana. Ama tuangalie mfano Uyole pale, mwaka 1970 wakati ramani zetu za msingi zinachukuliwa huenda Uyole ilikuwa ni mji mdogo sana, tofauti na leo ambapo Uyole imekuwa Jimbo kamili katika Jiji lile la Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha tunapata ramani za msingi mpya. Hatuendi kuchora upya mipaka au ramani ya nchi yetu, hapana, tunakwenda kutambua kilichopo ndani ya mipaka yetu, miji yetu imekaaje, miundombinu imekaaje, hifadhi zetu ziko vipi, mipaka yake iko vipi, ili tuondokane na migogoro isiyokuwa na maana yoyote ama itengenezwa na watumishi wetu wa ardhi ama binadamu kwa kuvamia maeneo ambayo tayari yana matumizi juu yake. Kwa hiyo, kazi hii tutahakikisha mpaka ufikapo Mwaka 2030 iwe imekamilika na tayari fedha hizo zimekwisha tengwa na Serikali hii ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda vilevile kuendeleza maeneo yaliyochakaa, yale ambayo watu walijenga bila kupanga, ambapo miundombinu haiwezi kuingia katika maeneo hayo; mfano barabara na miradi ya maji, hayo mabomba ya maji hayawezi kupita na kadhalika, ambapo miradi hii tunaanza kwanza utekelezaji wake katika eneo la Makangira pale Jijini Dar es Salaam na vilevile

tutakwenda Jijini Mbeya kuhakikisha kwamba, tunatengeneza upya maeneo ambayo hayajapangika katika Jiji la Mbeya, katika Jiji la Mwanza, Jiji la Arusha na hapa Dodoma vilevile tunakwenda kufanya kazi hiyo kubwa. Tayari utaona ni mafanikio makubwa ambayo yamepatikana chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta nzima hii ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uongozi wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeona vilevile uwekezaji wa vitendeakazi ambapo Wizara ya Ardhi ni muda mrefu ilikuwa haijapatiwa vitendea kazi. Ni majuzi tu Mheshimiwa Rais ametukabidhi magari 70, kwa ajili ya kwenda kwenye mikoa yetu na wilaya zetu kuhakikisha Watumishi wa Wizara ya Ardhi wanaweza kufanya kazi zao na kufika katika maeneo yenye changamoto kuhakikisha tunaipima nchi yetu na kuipanga kwa wepesi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 50 kwenye Mfuko ambao ulikuwa haujawahi kutumika, ambapo kwenye *KKK* ameweka shilingi bilioni 50. Tumeona viwanja vikipimwa, tumetambua maeneo ambayo tunatengeneza viwanja vya kutosha kuhakikisha kwamba, tuna makazi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tutakubaliana kwamba, ardhi ambayo ni rasilimali ya msingi ni wezeshi kwa sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya madini, sekta ya miundombinu na sekta ya maliasili na utalii na ni kitu wezeshi ambacho kinahitaji *management* ya hali ya juu. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba, tumejipanga vyema katika kuhakikisha *land management* inakwenda vizuri katika Taifa letu ili kuweza kuondokana na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga mpaka ufikapo mwaka 2030 kila kipande cha ardhi katika Taifa letu kiwe kimetambuliwa, ili kuondokana na migogoro. Tayari kazi hiyo tumeianza na hadi kufikia 2030, kama nilivyosema hapo awali, tutakuwa tumetambua kila kipande na kitakuwa kiko tayari, kwa ajili ya kumilikishwa pale ambapo itabidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kufanya mageuzi makubwa, kama nilivyoeleza yale yaliyofanyika na tutazidi kuendelea kuyafanya katika siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja iliyopo mbele yetu na ninakushukuru sana kwa fursa hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tutamalizia na Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ili niunge mkono hoja. Ninawapongeza sana Mawaziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Stanslaus Nyongo; vilevile Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake Mheshimiwa Chande, Makatibu Wakuu na watumishi wote kwa maudhurisho mazuri sana na hoja iliyoletwa hapa mezani. Hoja ambayo inasaidia kuhitimisha kwa kishindo kikubwa ngwe ya kwanza ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; na vilevile kutuandaa kuanza kwa kishindo ngwe ya pili ya Awamu ya Sita ya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapa tunahitimisha ngwe na Bunge litavunjwa kesho kutwa, ninaomba nitoe kwanza shukrani nyingi sana kwako wewe kwa uongozi mzuri wa Bunge letu hili na kwa mafanikio yako. Si hapa tu kwenye Bunge bali pia umekuwa ukitung'arisha huko duniani kwa nafasi uliyoishika kama Rais wa Mabunge Duniani; pamoja na Mheshimiwa Zungu. Vilevile ninapenda kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Elimu, Utamaduni na Michezo na Wenyeviti wengine wote wa Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kufanya kazi vizuri mpaka hapa tulipofika. Haya tutakayoeleza ni yale ambayo wenzangu wanaeleza na vilevile kuonesha kwamba kwa kweli Serikali katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaondoka hapa kifua mbele, tunajivuna, na tunajua baada ya kutiki Oktoba tunaanza tena kwa kishindo kwenye ngwe ya pili ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Abubakari Asenga wamezungumzia kidogo kuhusu umuhimu wa mafunzo ya amali, umuhimu wa sisi kuwekeza vizuri katika mafunzo ya amali. Ninapenda kukuhakikishia kwamba kupitia mpango uliowasilishwa na bajeti iliyowasilishwa tumejipanga vizuri, tunaendelea na kazi ambayo imeshaanza kwenye bajeti zilizopita kwa kutekeleza mageuzi makubwa ya elimu ambayo aliyaanzisha Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wote tunakumbuka kwamba aliagiza, amesimamia na tumeweza kukamilisha *blue print* ya utekelezaji na yeye mwenyewe anafuatilia.

Mheshimiwa Spika, nitakumbusha tu yale ambayo tulikubaliana na ambayo yalipitishwa kwenye sera, kwamba kuanzia mwaka 2027; na bajeti hii inatusaidia sana kwenye maandalizi; elimu ya lazima Tanzania itakuwa ni miaka 10 na si miaka saba tena. Kwamba, kwa kila mwanafunzi Mtanzania ni lazima afike kidato cha nne. Kwa upande wa Zanzibar wanafanya hivyo, kwa upande wa bara tumekuwa tukiishia darasa la saba kama elimu ya lazima.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hatuna *instrument* yoyote ya kumlazimisha mtu yeyote kuendelea mbele, kwa maelekezo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kutuhakikishia kwamba Tanzania yote, bara na visiwani sasa tunakwenda kuwa na elimu ya lazima ya miaka 10. Mtoto akimaliza elimu yake, kama ameanza na miaka sita kama inavyotakiwa kwa taratibu zetu na sera atamaliza walau akiwa na miaka 16; kwa hiyo wakati huo atakuwa tayari kuingia kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, katika mageuzi haya, kama alivyosema Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Abubakari, tumejiandaa kwa ujenzi wa mfumo wa amali. Juzi hapa tukiwa Simiyu Mheshimiwa Rais wetu alizindua kwa kuweka jiwe la msingi, ujenzi wa shule za amali na ufundi. Maana yake ni kwamba, kuna amali michezo, amali kilimo, kuna amali uvuvi, amali muziki na amali ufundi *(technical secondary*

*school).* Alizindua kwa kuweka jiwe la msingi shule ya kwanza ambayo ni kielelezo cha ujenzi wa duru ya kwanza ya shule 103 hapa Tanzania ya mafunzo ya amali ufundi *(technical secondary school).*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo umefuatilia na pengine uliona mbali sana, itajengwa vilevile shule kama hiyo pale Uyole na mipango hiyo ipo mbioni. Kwa hiyo shule hizi zinajengwa kwa nchi nzima. Hii ni duru ya kwanza, tutajenga duru nyingine na nyingine, na shule nyingine za amali takribani 115 ambayo siyo ufundi tayari zimeshaanza kufanya kazi. Kwa hiyo ningependa kuwahakikishia Mheshimiwa Sanga na Mheshimiwa Abubakari Asenga kwamba kazi hii inaendelea. Haya maelekezo ya Rais wetu, ni maono ya Rais wetu kwa hiyo Wizara haina *choice* na tunafurahia kutekeleza kazi hii inavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, lazima nifafanue kidogo na sitaelezea mageuzi yote, lakini nitaelezea tu mafunzo ya amali ufundi. Mwanafunzi yeyote atakayesoma sekondari ya amali ufundi akienda *high school* anaweza akachagua kurudi elimu jumla akafanya miaka miwili au akaenda *polytechnic* akafanya miaka mitatu. *Polytechnic* kama ilivyokuwa *Dar Tech*. Sasa hivi kwa maelekezo ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumekamilisha ujenzi wa *Polytechnic* ya kwanza mpya hapa Dodoma ambayo ina uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 1,500. Sasa hivi tumeiegesha *DIT* kabla haijaanza kusimama pamoja, ita-*constitute high school* ambayo itatoa cheti cha *form six* na diploma baadaye. Focus sasa hivi ipo kwenye TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, tunajenga nyingine Mwanza, ninadhani itakuwa Magu. Tunajenga nyingine Kigoma, tunajenga nyingine Mtwara, tunajenga nyingine Morogoro na tunajenga nyingine upande wa Zanzibar. Kwa hiyo tutakuwa na *polytechnic* hizo ambazo zinakwenda kuwachukua wanafunzi katika mafunzo ya amali. Ni kuwahakikishia tu wenzangu Waheshimiwa Wabunge waliosema suala hili kwamba kwa kweli tunaenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pengine wakati ninalizungumzia suala hili la mafunzo ya amali nirudi tena kwenye masuala ya *VETA*. Nielezee,

hapa majuzi mwezi Desemba nilikutana na kijana mmoja Mtanzania. Yeye ni *technician*, anafanya kazi kwenye migodi ya madini Guinea Conakry. Guinea Conakry ni nchi inayoongea kifaransa. Nikamuuliza, wewe umejifunza wapi? Akasema nimejifunza *VETA* Tanzania. Nimemaliza kusoma *VETA* pale nikawa ninafanya kazi kwenye makampuni ya madini hapa Tanzania, hatimaye nikachuliwa na mwekezaji nikaenda Namibia, nimetoka nimekaa Maurtania, wanaongea Kiarabu na Kifansa, ameenda Guinea Conakry. Akanihakikishia kama ambavyo nilikuwa nimeshasikia, kwamba kuna Watanzania wengine wengi wapo Ghana, wapo hapa Congo DRC, wapo huko Mauritania na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maono ya Mheshimiwa Rais wetu ni kufungua fursa hizo kwa vijana wengine wote hapa Tanzania. Rais wetu ameagiza, na kama tunavyofahamu, kwamba kila wilaya ambayo haina *VETA* ya Serikali tujenge *VETA* ya Serikali. Ujenzi unaendelea katika wilaya 64 Tanzania nzima. Vilevile aliagiza na Waheshimiwa Wabunge watakumbuka, kwamba wakati Rais wetu anakula kiapo kulikuwa na mikoa mitano haikuwa na *VETA* za mikoa na mingine ujenzi ulikuwa umeanza lakini haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, alivyoingia madarakani haraka, bajeti ya kwanza alihakikisha kwamba fedha zinaenda kukamilisha *VETA* ya Geita ambayo tunataka iwe *dedicated* kwenye mambo ya madini, tumekamilisha *VETA* ya Simiyu, tumekamilisha *VETA* ya Ludewa na *VETA* ya Rukwa, sasa hivi ujenzi wa *VETA* ya Mkoa wa Songwe unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia fursa hii ya *VETA* kwa vijana kuweza kupata kazi ndani ya nchi na nje ya nchi kwa kweli lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake haya na kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vijana wetu inakuwa rahisi zaidi kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha amezungumzia sana masuala ya Nelson Mandela na Elimu ya Juu kwa ujumla wake. Labda niseme tu, katika elimu ya juu Rais wetu alivyoingia madarakani alikuta kuna Mradi unaitwa *HEET (High*

*Education for Economic Transformation)* ambao ulikuwa ume-*focus* kuendeleza *campas* zile ambazo zilikuwa hazipo. Baadaye aliagiza tubadilishe mradi ule wa *World Bank* ili kuhakikisha kwamba mikoa ambayo haina Chuo Kikuu ipelekewe *campus* za vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja tu; Mkoa wa Kigoma sasa hivi utakuwa na *Campus* ya Chuo Kikuu cha Mhimbili cha Afya Shirikishi kwa upande wa kule, na ujenzi tayari umekwishaanza. Mikoa mingine yote ukiacha Mkoa wa Pwani ambao tutauwekea mkakati wake itakuwa angalau na *campus* ya chuo kikuu. Kwa mfano Mtwara, Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara wamesema muda mrefu sana, kilikuwa ni kilio cha Mtwara, Mheshimiwa Rais wetu alisikia na akaagiza kwamba tuchukue vile vyuo viwili, Mtwara ufundi na Mtwara ya kawaida, tumeviunganisha vinakuwa *campus* ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kuhakikisha kwamba tunatimiza azma ya Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili kuna suala la mikopo ya wanafunzi na wanafunzi walisikia wa elimu ya juu wakati Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakula kiapo cha kuongoza nchi yetu mikopo ya elimu ya juu ilikuwa ni bilioni 464. Sasa hivi, bajeti hii aliyoileta Mheshimiwa Mwigulu hapa Bungeni, bajeti ya mikopo ya elimu ya juu pamoja na ile kidogo ya diploma ni bilioni 839, ni karibu mara mbili ya bajeti ambayo Mheshimiwa Rais aliikuta. Kwa hiyo pamoja na kwamba tunajua tunahitaji kwenda zaidi na zaidi lazima kwa kweli tuwe wepesi kushukuru na kupongeza kwa hatua kubwa aliyoifikia.

Mheshimiwa Spika, na kwenye masuala ya sayansi ambayo Mheshimiwa Nahodha alizungumzia labda niseme, Chuo Kikuu hiki cha Nelson Mandela tumeki-*dedicate* kama *research university* kwa hiyo kina *post graduate* tu na tutajitahidi kisilete *undergraduate*. Nimekwishapata kibali, ninamwalika Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Afrika ya Kusini, atakuja kukitembelea; kinabeba jina la Mandela, tunadhani tunaweza tukashirikiana nao kukifanya chuo hiki kuwa cha kimataifa zaidi na pia kinyanyuke juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumeidhinisha, tumeanzisha *Campus* ya *Indian Institute of Technology* pale Zanzibar; na tumesema ile ni *campus* ili kuhakikisha kwamba vile viwango vyao ambavyo ni vya juu sana duniani navyo tunaviona hapa Zanzibar na kwa kweli tunapata wanafunzi sasa hivi kutoka dunia nzima wanakuja Zanzibar katika kile chuo na tunakisapoti.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kuhusiana na kufundisha Kiswahili, dakika moja tu. Ningependa nianze kumzungumzia Mheshimiwa Rais wetu, lakini ninakuwa na-*abuse* nafasi ambayo umenipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja vilevile, ninadhani na Mheshimiwa Kiswaga, kwamba tujiandae kufundisha Kiswahili, ninajua Mheshimiwa Kabudi labda atalielezea zaidi, lakini kwa upande wa elimu tumehakikisha sasa hivi tutakuwa na chuo kimoja kile cha Marangu ambacho kinafundisha lugha, kianze kufundisha walimu ambao wanaweza wakawa wakalimani vilevile. Huwezi kwenda kufundisha Kiswahili huko nje kama humudu lugha nyingine. Kama unakwenda nchi za *Latin America* uongee Kihispaniola, unakwenda Arabuni uongee Kiarabu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kule kwa kuanzia tutahakikisha kwamba tunaweka ile maabara ya lugha ya Kichina, Kifaransa, Kiarabu kwa kuwaandaa walimu ambao wanaweza wakafundisha Kiswahili, Kiingereza na hizo lugha nyingine; ili wengine kama hawafundishi wawe wakalimani waende wakafundishe na Kiswahili sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi kwa kweli muda hautoshi. Tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu na tunatumaini kwamba wote mwezi Oktoba tunaweka tiki ili ngwe ya pili haya mambo makubwa ya kishindo yaendelee.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu. Pia nikushukuru wewe kwa umahiri na ubobezi uliouonesha katika kuendesha Bunge letu. Kwa dhati na kwa unyenyekevu mkubwa ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio haya makubwa ambayo yameongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, kila nikitazama sura ya kila Mheshimiwa Mbunge humu ndani ninawiwa kusema ahsante kwa michango yao ambayo imeboresha sana Sekta ya Afya katika kipindi hiki chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na ninaomba niwatakie kila la kheri katika jambo letu zito linalokuja mbele yetu na Mwenyezi Mungu aturudishe wote kwa kishindo ndani ya ukumbi huu tukiongozwa na wewe Spika wetu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kunipa hii dhamana ya kuongoza Wizara ya Afya. Ninaposimama hapa leo ninasimama kifua mbele katika kipindi cha miaka hii mitano, Wizara hii imepewa fedha ambayo imeendeleza Sekta ya Afya yenye thamani ya fedha za Kitanzania zaidi ya trilioni 6.3; haijapata kutokea. Kwa hiyo ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais

Mheshimiwa Spika, upo usemi unaosema kanzu ya Ijumaa hufuliwa mapema na gauni la Jumapili nalo hufuliwa mapema. Mheshimiwa Rais amekwishajifungia kazi yake mapema na gauni lake mapema; tunachosubiri ni mwezi Oktoba kazi yetu itakuwa ni moja tu, kwa kweli tutakwenda kutiki haya mafanikio makubwa ya sekta ya afya nchini.

Mheshimiwa Spika, wote tunakumbuka, Mheshimiwa Rais alianza kuongoza nchi hii katika kipindi kizito sana, tulikuwa na msiba mkubwa,

simanzi kubwa na tulikuwa na matukio mengine makubwa sana ambayo yalikuwa yanaathiri sekta ya afya. Mheshimiwa Rais katika kipindi kile cha msiba mkubwa alituvusha vizuri kweli kweli. Haitoshi, anamaliza kutuvusha kwenye ule msiba tunakutana na tatizo kubwa la kiafya la ugonjwa wa *corona*. Mheshimiwa Rais ametuvusha vizuri katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka hata tulipopata fedha kwa ajili ya mapambano ya UVIKO, fedha ile ilikuwa ikanunue barakoa, lakini Mheshimiwa Rais aliamua kubadilisha matumizi ya fedha ile. Leo tunajivunia vituo vya kutolea huduma ya afya vingi katika nchi yetu ya Tanzania, kutoka afya msingi mpaka afya rufaa na hivyo kuwezesha 80% ya wananchi wa Tanzania kuwa na uwezo wa kufikia huduma za afya katika umbali ambao ni chini ya kilometa tano. Kwa hiyo hilo ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka Mheshimiwa Rais alivyotuvusha katika magonjwa ya mlipuko makubwa ikiwemo ugonjwa wa *marburg*. Tuna taarifa ambazo Waheshimiwa Wabunge wengi tumezisikia, ni namna gani ugonjwa wa *marburg* umepoteza maisha ya wananchi wengi katika mataifa mbalimbali ulimwenguni. Tumeona Mheshimiwa Rais alivyotuongoza vizuri na jinsi tulivyoweza kupambana na magonjwa hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka huu wa 2023 ugonjwa wa *marburg* tumeweza kupambana nao kwa siku 54 tu mpaka *WHO* wametupongeza kwa kasi hiyo kubwa. Hii imetokana na jinsi alivyojenga mifumo kwenye sekta ya afya. Tumejiimarisha sana na tuna uwezo sasa wa kukabiliana na kila jambo linalohusiana na sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amebadilisha mwelekeo wa sera za kimataifa kwenye sekta ya afya na wote tumeshuhudia, haijapata kutokea nchi moja inashinda kiti cha Mkurugenzi wa Afya Kanda ya Afrika mara mbili; na ni mara mbili katika mwaka mmoja. Ukichukua toka ule mwezi Agosti mpaka mwezi Mei ni ndani ya mwaka mmoja tumeweza kushinda kiti hicho mara mbili. Kwa hiyo sasa hivi Mheshimiwa Rais ameifanya nchi yetu iingie katika medani

ambazo zina uwezo wa kujenga hoja na kushughulika na diplomasia ya kimataifa kwenye sekta ya afya. Tumpigie makofi na tumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki kifupi tumekumbana na mabadiliko ya sera za kimataifa na hasa yale mataifa makubwa ambayo yalikuwa yamewekeza sana kwenye sekta ya afya; kwamba sasa walianza kujitoa katika kuwekeza kwenye sekta ya afya. Eneo ambalo lilikuwa ni tatanishi sana ni eneo la kuhudumia magonjwa msonge yote, magojwa yanayoambukiza, UKIMWI, malaria na TB. Mheshimiwa Rais ni kati Marais wachache na nchi chache; pamoja na mabadiliko ya sera hizo za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwahakikishie Wabunge ametuongoza vizuri Mheshimiwa Rais hatuna shida na tutavuka salama na hivyo basi matibabu kwa magonjwa hayo yote, ikiwemo dawa na vitendanishi vyote tunavyo vya kututosheleza mpaka mwaka 2026. Huyu ndiye Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, ukiwaangalia wanazuoni na kuwasikiliza mara zote wamekuwa wakisema, unaweza kuwa na kiongozi, lakini unaweza ukampata kiongozi ndani ya viongozi akawa ni kiongozi bora. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan si kiongozi tu, lakini ni kiongozi bora, mzalendo, mwenye uwezo mkubwa wa kuiongoza nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa sababu gani? Leo nitazungumza maeneo mawili tu kati ya vigezo hivyo vya wanazuoni vya kiongozi bora. Ya kwanza, kiongozi bora ni lazima alete mabadiliko makubwa katika eneo analoongoza Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya hivyo kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, kiongozi bora ni lazima ajenge maono ya wapi anataka kulipeleka taarifa zake ama eneo lake kwenye uongozi. Kwa mara ya kwanza Tanzania imeweka historia ulimwenguni kwa kupunguza vifo vya akinamama kwa 80%. Tumetoka vifo 556 tumefika vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000. Hiyo imepelekea hata wenzetu wa kimataifa kuja kutupa tuzo, Bill Gates wamekuja kutupa tuzo,

wamempa Mheshimiwa Rais tuzo, tena ndani ya nchi yetu ya Tanzania, haijawahi kutokea.

Mheshimiwa Spika, leo nchi yetu ya Tanzania ni kati ya nchi 46 katika Bara la Afrika ambazo zina *MRI Machine;* na nchi yetu sisi inashika nafasi ya nane kati ya nchi za Afrika kwa kuwa na mashine za *MRI*. Zipo nchi hazina hiyo mashine, zina zero kabisa, lakini Tanzania haipo, sisi Tanzania tumeweza kufanikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, nilisema wakati wa hotuba, kwamba tuna *pet scan machine* na ni kati ya nchi mbili tu katika East Africa ndio tuna *pet scan machine*. Kwa hiyo ni hatua kubwa sana ambayo imefikiwa; tumpongeze Rais wetu. Mheshimiwa Rais ameongeza Madaktari Bigwa na wabobezi kutoka 2,180 na sasa hivi tunao 4,980 katika nchi yetu na hivyo kupunguza utegemezi wa Madaktari Bigwa kutoka katika mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwamba yajayo yanafurahisha zaidi. Mheshimiwa Rais amejipanga sasa, kwamba huko tunakokwenda tunakwenda kuanzisha kituo kikubwa cha umahiri Afrika Mashariki kitakachotoa matibabu ya magojwa ya damu na upandikizaji wa uroto. Tunaenda kuanzisha kituo kikubwa cha kimataifa na si kikubwa tu bali pia chenye ubora wa hali ya juu kwenye Ukanda wa Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika kitakachokwenda kutoa matibabu ya figo. Tutajenga umahiri huo ndani ya nchi yetu na katika Bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda sasa kuanza kuzalisha *ARV's* hapa nchini Tanzania, tunakwenda kuzalisha bidhaa tiba za pamba hapa nchini Tanzania, tunakwenda kuzalisha *rapid testing kits* hapa nchini Tanzania, tunakwenda kuzalisha viungo tiba na viungo saidizi vya tiba hapa hapa nchini Tanzania. Pia tunakwenda kuanza kutekeleza bima ya afya kwa wote ili wananchi wote wa Tanzania wanufaike na huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, Rais huyu mwenye maono, ili tuone mwezi Oktoba tunaenda kuchagua nini, sasa tunakwenda kufanya tafiti na

kuboresha tiba asili na kuziingiza kwenye mfumo rasmi kwa kufanya tafiti nzuri na hivyo kuanza kujitegemea wenyewe kwa kuzalisha dawa zetu za asili na kuzifanya ziwe bora na ziweze kutumika katika nchi yetu. Vilevile tunakwenda kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kwa kuzuia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mambo ni mengi na tungekuwa na muda tungeyaeleza mengi. Kubwa zaidi tunakwenda kuingia kwenye *telemedicine*, sasa tunaanza kutumia sayansi na teknolojia katika kutoa tiba na kuboresha huduma za tiba kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mambo ni mengi sana, lakini ninaomba niseme kwamba, tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuna kila sababu ya kuwaeleza Watanzania umuhimu wa kuendelea kuwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan na hasa kwenye sekta ya afya ambayo ni sekta yenye usalama kwa kila mwananchi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Dkt, Samia amefanya kazi kubwa, anastahili kupongezwa na anastahili kupigiwa kura za kishindo mwaka huu wa 2025, mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, baada ya hayo, ninaomba niseme kwamba, ninaunga mkono hoja na ninawapongeza Mawaziri waliotoa hoja hii hapa Bungeni. Ninakupongeza wewe pia kwa kuendesha Bunge letu sawasawa na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kukutana kwetu siku ya leo, ahsanteni sana kwa michango yenu. Sasa tunao wachangiaji wa mchana, ninafikiri kwa sababu hawa wachangiaji wote ni wa Serikali basi wote wajikute hapa kwa sababu hapa tuliweka hii orodha ndiyo maana mtagundua baadaye kuna Naibu Mawaziri watapata nafasi ya kuchangia kwa sababu kipindi hiki cha kwanza hawakupata nafasi.

Nasema hivi kwa sababu, watu wasije wakaona kama tunachanganya mambo kabla ya Naibu Waziri kuzungumza anazungumza Waziri; na hata mchana wapo Manaibu Waziri ambao wapo hapa kwa ajili ya kuchangia. Kwa hiyo kadri watakavyokuwa wamefika hapa basi watakuwa wanaitwa ili waweze kupata hiyo nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao wameingia baada ya matangazo ya awali ya wageni kupita.

Wageni 25 wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni Jumuiya ya Wafanyabiashara kutoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania wakiongozwa na Ndugu Hamis Gizembe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 65 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Walimu Wakuu kutoka Mkoani Katavi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanachama 50 wa Kikundi cha Faraja *Online* Tanzania Fahari Yetu kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi watatu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Fransiscan kutoka Pangani Mkoani Tanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Wabunge wote kwamba kama mjuavyo kesho siku ya tarehe 24 Juni, 2025, Bunge litapiga kura ya uamuzi wa Bajeti ya Serikali kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni yetu ya 126(2). Kama ambavyo tumekuwa tukikumbushana siku zote Waheshimiwa Wabunge na Wabunge ambao hawapo humu ndani sasa, kura ya kesho ni kura ambayo kila mmoja anaitwa na kuitika kwa jina lake. Kwa hiyo ni muhimu sana ukiona jirani yako hayupo basi mkumbushe. Kwa tangazo hili ni kwamba kesho kila Mbunge awepo Bungeni. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo ni muhimu tukakumbushana kupitia tangazo hili, ni kwamba tumezoea Bunge kwamba wakati wa kupiga kura huwa tunaanza saa 11.00, kesho kura zitaanza kupigwa saa

10.00. Kwa hiyo ni muhimu sana kukumbushana Wabunge ili mtu asije akaitwa jina lake akasema nilijua muda fulani, ndiyo maana umetangaziwa leo mapema kabisa; na wote tunafahamu umuhimu wa ile kura. Kama ikikupita imekupita na utajua mwenyewe cha kujieleza kwenye chama chako kwa kadri kilivyokuelekeza upigeje kura hii. Ninafikiri wote tunaelewa kwa sababu tumekuwepo hapa miaka mitano. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.06 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na tulikuwa kwenye uchangiaji ambapo upande wa Serikali walikuwa wanachangia, lakini kama tulivyosema, kama

Mheshimiwa Spika alivyotoa maelekezo, kunaweza kukawa na wengine wachache ambao watakuwa wanachangia, lakini kwa kiasi kikubwa tunaongelea upande wa Serikali.

Kwa hiyo, nina *list* ya wachangiaji hapa, maana yake tumeambiwa na Naibu Mawaziri na nyie mnachangia sasa hivi. Kwanza, nimwite Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kama uko tayari Mheshimiwa maana yake nisije nikawa nimekushtua. Leo ni siku yenu wote. Kama hayuko tayari basi nimwite Mheshimiwa Chande, *sorry* Mheshimiwa Profesa Kabudi. Haya Mheshimiwa Dkt. Kachwamba basi utafuata. Mheshimiwa Kabudi, basi nikwite uweze kuchangia.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu rahimu kwa ruzuku ya uhai lakini kwa kutujalia afya ambayo inatuwezesha leo kuweza kujadili bajeti na mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameipa kipaumbele Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Wizara ambayo inashika mtima wa Taifa letu. Wizara ambayo inaleta furaha ya Taifa letu, Wizara ambayo inashika mshikamano wa Taifa letu, lakini Wizara ambayo inajenga matumaini ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amelionesha hilo kwa dhahiri kwa kutuongezea bajeti. Ukichukua bajeti ya Wizara hii mwaka wa fedha 2022/2023 ilikuwa ni shilingi bilioni 35.4 na imepanda sasa katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2025/2026 kufikia shilingi bilioni 519 ambalo ni ongezeko la 1,366%. Kwa hiyo, unaweza ukaona kabisa jinsi ambavyo Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameijali sekta hii kwa ongezeko la 1,366%. Ninaamini haijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kufanya mambo makubwa katika kipindi chake. Katika bajeti ambayo imepita mwaka huu, tunakwenda

kufanya jambo kubwa ambalo lilifanyika miaka 95 iliyopita. Mwaka 1930 ndipo Lugha ya Kiswahili iliposanifishwa na kupata Lugha Sanifu ya Kiswahili ambayo msingi wake ulikuwa ni Lahaja ya Kiunguja, lakini pia kuchukua maneno katika lahaja nyingine na usanifishaji huo ulifanywa na Waingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mara ya kwanza tunakwenda kufanya usanifishaji mkubwa wa Lugha ya Kiswahili, miaka 95 baada ya hilo kufanyika na tofauti ya wakati huo na sasa, safari hii tunafanya usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili sisi wenyewe Watanzania na Waafrika wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hilo, hatutazingatia tu Lahaja za Kiswahili lakini pia lugha nyingine za Kiafrika ili kukifanya sasa Kiswahili kuwa ni lugha ya Kiafrika na hiyo itakuwa inatekeleza mapendekezo yaliyotolewa miaka 1977 wakati wa Tamasha la Sanaa na Utamaduni wa Waafrika *(FESTAC)* lililofanyika Lagos Nigeria ambapo Profesa Akinwande Oluwole Babatunde Soyinka au maarufu kama Wole Soyinka, alipendekeza Kiswahili kuwa ni Lugha ya Afrika na akapendekeza sasa Kiswahili kichukue msamiati na istilahi kutoka katika lugha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usanifishaji huu, utazingatia makundi yote makuu ya Lugha za Kiafrika yaani Lugha za Kibantu (Niger Bantu), Lugha za Noritiki (Nilo-Saharan), Lugha za Kikhoisani na Lugha za *Afro-Asiatic* (Wakushitiki) ambapo lugha zote hizo zinapatikana katika pia Nchi ya Tanzania. Huu utakuwa ni mradi wa aina yake ambao tunaamini baada ya kukamilika sasa utatuwezesha kutoa kamusi mama ya Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kiswahili pia tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha kufungua vituo 33 vya kufundisha Kiswahili na Utamaduni wa Mtanzania nje ya nchi. Kwa hiyo, huko nje hatufundishi tu Kiswahili, tunafundisha pia Utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pia ametusaidia sana katika kuimarisha sekta ya habari ambapo kama tunavyofahamu tarehe 8 Disemba ilihamishiwa kutoka Wizara hii, kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na nimshukuru sana aliyenitangulia kuiongoza Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Jerry Silaa kwa msingi mkubwa aliouweka wa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na vyombo vya habari ambao umeimarisha uhuru wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imepanda kutoka nafasi ya 48 kwa 48% kwa viwango vya uhuru wa habari duniani. Tulikuwa nafasi ya 143 mwaka 2023, sasa tumefikia nafasi ya 95 mwaka 2025. Haya ni mafanikio makubwa sana na hii siyo sisi tunaosema, ni taarifa ya *reporters without borders* ambao wanaona ni jinsi gani Tanzania sasa uhuru wa vyombo vya habari umepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya habari, pia niishukuru sana *TAMWA* ambapo kwa kushirikiana na Serikali tuliweza kuandaa Tamasha la *Samia Kalamu Awards,* ambalo nalo lilikuwa na mafanikio makubwa sana na nichukue nafasi hii kuwashukuru Mawaziri wa Wizara zote ambao kila Waziri alitoa zawadi kwa waandishi wa habari walioandika mambo yanayohusu sekta yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sasa imekuwa ni nchi inayovutia mikutano mikubwa ya upande wa habari. Mwaka huu tutakuwa na mkutano mkubwa tarehe 14 Julai kule Arusha kuhusu mambo ya habari katika Bara la Afrika, yaani siku ya uhuru wa habari duniani ambao unasimamiwa pia pamoja na *Media Council of Tanzania*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana *Media Council of Tanzania* kwa kuwezesha kuitisha huu mkutano mkubwa ambao utafanyika Tanzania ambao unaonesha imani kubwa ambayo dunia inayo sasa na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha uhuru wa habari na vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, Tanzania imeendelea kuwa kinara kwa waandishi wake nguli wa habari

wanaoshikilia nafasi za juu katika vyama vya kihabari vya kikanda. Waandishi hao ni pamoja na Deodatus Balile ambaye ni Rais wa Jukwaa la Wahariri Afrika Mashariki; Bwana Kajubi Mukajanga ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Habari la Afrika Mashariki na Bwana Ernest Sungura ambaye ni Mwenyekiti wa Mabara Huru ya Habari Barani Afrika. Hayo yote yanaonesha ni jinsi gani ambavyo Tanzania sasa inapaa katika suala zima la sekta ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya habari pia, *TBC* imefanya kazi kubwa sana. Tumeweza kuongeza kufikia maeneo mbalimbali. Kwa mfano, sasa tumeweza kuzifikia wilaya 139 na kabla ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi ya uongozi tulikuwa tumefika katika wilaya 102 tu. Hayo yote ni mafanikio makubwa sana ambayo hatuna budi kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuyafanya yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusu Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Tanzania ilikuwa ni Makao Makuu ya Kamati ya Nchi Huru za Afrika ya Ukombozi na sasa tuna kituo hicho ambapo tuna vituo mbalimbali 266 ambavyo tumevichambua na sasa tunaanza kuviweka katika orodha na kituo hicho kimepata ugeni mkubwa mwaka huu wa Rais wa Msumbiji, Daniel Chapo na Rais wa Namibia, Bi. Netumbo Nandi-Ndaitwah na ni lengo letu sasa kujenga kituo kikubwa Eneo la Kiromo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa ni suala la michezo. Ningependa kutoa taarifa katika Bunge lako kwamba diplomasia kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo iliyoiwezesha Tanzania kuwa mmoja wa wenyeji wa Mashindano ya *CHAN* na Mashindano ya *AFCON*. Tayari ratiba imetolewa ya Mashindano ya *CHAN* na *AFCON* na Tanzania tumepewa heshima ya kuwa na mechi ya Ufunguzi ya *CHAN* itakayofanyika katika uwanja wa Benjamin Mkapa tarehe 2 Agosti mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanikiwa pia kuongeza kituo kimoja cha michezo, yaani sasa Zanzibar imetambuliwa kuwa kituo cha michezo. Kwa hiyo, Tanzania tutakuwa na makundi mawili; kundi

moja ambalo litakuwa Dar es Salaam na ambalo litakuwa ni Tanzania, Madagascar, Mauritius, Burkina Faso na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Kundi la nne litakwenda Zanzibar ambapo itakuwa ni Senegal, Congo, Sudani na Nigeria. Uganda wamepata kundi moja na Kenya wamepata kundi moja na Kenya ndiyo atakayekuwa mwenyeji wa mchezo wa fainali na Uganda atakuwa mwenyeji wa mchezo wa mshindi wa tatu. Haya ni mafanikio makubwa sana katika diplomasia ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, katika michezo siyo mpira tu, tumekuwa washindi katika mchezo wa *cricket,* tumekuwa washindi katika mchezo wa soka wa wanawake, lakini katika miaka hii mitano, Timu za Tanzania zimeongezeka ambazo zinashiriki katika mashindano. Tulitoka mashindano 68 duniani na sasa tumeweza kushiriki mashindano 402. Ushiriki wa Timu za Tanzania katika mashindano hayo umesaidia wanamichezo kujifunza na kujitangaza zaidi huko duniani na yote haya ni mafanikio ambayo yameletwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake ambao umezingatia diplomasia ya uchumi lakini pia diplomasia ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulitolea taarifa kwako ya mafanikio makubwa sana ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kukuza sanaa. Kama Wabunge wanavyofahamu sasa wasanii wetu wamekuwa ni maarufu duniani na siyo tu kuwa maarufu duniani, lakini kupitia sasa *COSOTA,* tumeweza kuhakikisha kwamba wanapata mikataba mizuri na wanapata mapato ya kutosha ambayo yanawawezesha wao kuweza kujikimu katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu sana. Sanaa na michezo leo ni uchumi na kundi kubwa ambalo liko kwenye sanaa na michezo ni vijana, lakini upande wa sanaa hasa katika sanaa ya utengenezaji wa vifaa mbalimbali kundi kubwa ambalo liko katika nafasi hiyo ni kundi la wanawake. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewawezesha vijana wa Tanzania kuboresha hali yao ya uchumi lakini amewawezesha wanawake wa Tanzania kuboresha hali yao ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa tuliyonayo sasa ni kuitangaza Tanzania ili iweze kufahamika na katika kufanya hivyo, Wizara imeanza mchakato wa kuyafanya mambo haya manne sasa yaingie katika urithi usioshikika wa dunia kule *UNESCO (Cultural Intangible Heritage)*. Moja ni tamasha hili ambalo tumekuwa nalo Jumamosi la Bulabo, ambalo tayari mchakato umeanza na tunategemea ifikapo Machi mwaka ujao, tutaweza kupeleka dozi ya kule *UNESCO* ili Bulabo sasa itambuliwe kuwa ni urithi usioshikika wa kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sherehe za Mwaka Kogwa, wale wenzetu wanaotoka Zanzibar wanafahamu. Tumeanza mchakato sasa wa kufanya utafiti kuhakikisha Mwaka Kogwa nao unatambuliwa kuwa ni urithi wa dunia usioshikika. Lingine ni uchoraji wa picha za Tingatinga ambazo watu wengi wamedhani zinatoka nchi nyingine lakini ni Tanzania. Mwisho ni Muziki wa Singeli ambao nao tunaupeleka katika hilo. Sasa nimalizie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Profesa, muda wako umekwisha, malizia.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa shukurani nyingi sana. Kwanza, shukurani sana kwa Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Akson kwa uongozi wake mahiri; Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu; pia, na wewe mwenyewe, nitamke hapa, mimi nina fahari kubwa sana kwamba katika historia yangu ya maisha nimekuwa mwalimu wa wakuu wawili wa mihimili. Yaani Spika na Jaji Mkuu lakini na wewe mwenyewe ni mwanafunzi wangu wa *criminal law* mwaka 1986 na mwanafunzi wangu wa *land law* mwaka 1987 na ninakushukuru sana wakati namwoa Mke wangu Amina ulikuwa ni mmoja wa watu waliokuja kucheza ili kusherehesha ile harusi yangu tarehe 15 Agosti, 1987. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lile ninalienzi sana kwamba wewe ulikuwa ni mmoja wa wale waliyoifanya ile harusi yangu siku hiyo ipendeze baada ya misa takatifu katika Kanisa la Mtakatifu

Albano. Kwa hiyo, nikushukuru wewe na wengine wote ambao ndani ya jengo hili nimewafundisha sheria. Ninapokuona wewe, ninapowaona akina Mheshimiwa Salome, Mheshimiwa Damas, Mheshimiwa Ummy, ninapowaona wote ninapata fahari kibwa na hiyo inanikumbusha maneno ya Zaburi kwamba, "Mungu huushibisha uzee wako mema na hurejesha ujana wako kama tai." *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Palamagamba Aidan Mwaluko. Sasa mwalimu anapokuwa anaongea hata kumkatisha inakuwa tabu. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry William Silaa na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, ajiandae.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuifikia siku hii ya leo, ambapo Serikali nasi tunasema kuhusu hoja mbili zilizowekwa mezani tukiwa na afya njema kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya nchi yetu na nje ya mipaka ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwapongeze watoa hoja hizi mbili, *the two brothers* kutoka Iramba: Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba zao makini kabisa zilizojaa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa uniruhusu nami nichangie machache kwenye hotuba hizi mbili ambazo zimewekwa mezani na kwa wiki nzima Bunge letu Tukufu limejadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoanza kuchangia, ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya Taifa letu, lakini kipekee ninamshukuru sana kwa kuniamini mimi Ashatu Kijaji ninaamini aliwaamini na Wanakondoa ambao walinileta Bungeni. Kwa Wizara tano ndani ya miaka minne, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa imani yake hii kubwa kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejipambanua kwenye mambo mengi makubwa na ninaomba nisemee machache yaliyofanyika kwenye sekta ya mifugo na uvuvi. Alipoingia madarakani tu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema kwa Watanzania anataka kutengeneza ajira za kutosha kwa Watanzania, vijana wa Kitanzania pamoja na akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira hizi zinapatikana kwenye sekta za uzalishaji ambapo sekta yetu ya mifugo na uvuvi ipo pia. Hakusita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alituongezea bajeti ya kutosha, ukiwa kama Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Kilimo, Mifugo na Biashara, tumeona kutoka shilingi bilioni 66 Mwaka wa Fedha 2020/2021 leo hii tumefika bilioni 476 ambayo ni sawa na 613%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa akili ya kawaida ni ngumu sana kuielewa, lakini kwa kuwa tunaye mama mpenda watoto wake, mama mlezi wa Taifa, yamewezekana ndani ya kipindi kifupi sana tangu alipoingia madarakani. Hakika sisi wavuvi na wafugaji wa nchi hii tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu na kama tulivyomwahidi juzi tukiwa pale Bariadi kwamba, kura zote za wavuvi na za wafugaji ni za Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongezewa bajeti hii tumefanya mambo mengi makubwa na jambo la kwanza kabisa

ambalo ninatamani niliseme mbele ya Bunge hili Tukufu ni kampeni yetu ya chanjo na utambuzi wa mifugo yetu, ambalo ni jambo la kihistoria, jambo ambalo halijawahi kufanyika kwenye nchi yetu, ameliweza Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu tulitengewa shilingi bilioni 69.2 na amezindua mwenyewe kampeni hii ambayo inakwenda kuwa ni mkombozi mkubwa kwenye sekta ya mifugo. Tunakwenda kuchanja mifugo yetu nchi nzima, tunakwenda kuitambua mifugo yetu nchi nzima. Hii inatupelekea Watanzania sasa kwenda kupata ithibati kutoka Shirika la Afya ya Wanyama Duniani. Maana yake nini, sasa tuna uwezo wa kupeleka mifugo yetu pamoja na mazao yake dunia nzima, kwa sababu ya jambo hili kubwa lililofanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi tayari mwaka 2021 tulisafirisha nyama nje ya nchi yetu tani 1,774 tu, lakini leo tayari tumefika tani 14,000 ndani ya kipindi cha miaka minne tu. Haya ni mapinduzi makubwa na haya yote yamefanyika tukiwa hatujaianza kampeni hii. Tulipozindua kampeni hii tayari tumeitwa na mataifa matano duniani, sasa wako tayari kusafirisha mifugo yetu ikiwa hai kwenda kwenye nchi zao, haya ni mapinduzi makubwa sana ambayo yameletwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ongezeko hili la bajeti, tumeweza pia kujenga majosho 754, ambayo yametuwezesha sasa kwenda kuogesha mifugo yetu na tumeweza kupunguza magonjwa ya mifugo yetu kutoka 78% mpaka 44% ndani ya kipindi cha miaka minne. Hii ni hatua kubwa sana kwenye sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwitikio huu ambao ni kazi nzuri aliyoianza Dkt. Samia Suluhu Hassan, wafugaji wameamua kubadilika na sasa wanasema wanakwenda kufuga kibiashara, ile kawaida ya kuwa na ng'ombe wa miaka 15, ng'ombe wanaopewa majina ya mababu zetu na mashangazi zetu, wafugaji wamesema sasa inatosha, wanataka kudhihirisha utajiri wao na mipaka ya nchi yetu imefunguka tunapeleka mifugo yetu pamoja na mazao yake duniani. Haya ni mapinduzi makubwa ndani ya sekta yetu ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania ni mashahidi pia kwa upendo uleule wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akaamua kuleta programu ya 'Jenga Kesho Yako iliyo Bora' kwa vijana wa kitanzania kwenye mifugo. Ni fahari na faraja kubwa sana leo tayari vijana 106 wameshakopeshwa shilingi bilioni moja ya Kitanzania, wameshanunua ng'ombe zaidi ya 1,500 na zote wameshazipeleka sokoni. Haya ni mapinduzi makubwa na hii inaonyesha fursa ni kubwa kwenye sekta ya mifugo, tunawaambia Watanzania sasa waje tuwekeze pamoja kwenye sekta yetu ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kidogo kwa sababu ninasikia kengele imegonga kwenye sekta yetu ya uvuvi. Kwenye uvuvi Dkt. Samia Suluhu Hassan hakutuacha hivi hivi. Alituelekeza sasa tuelekee kwenye kuyatumia maji yote yaliyopo ndani ya nchi hii na tayari tumeanza kufanya utafiti ili tuyatumie ipasavyo maji yaliyopo kwenye mito yetu, kwenye mabwawa yetu na kwenye maziwa yote ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari sasa, wewe ni shahidi tayari tumeshakabidhi vizimba 507 kwa vijana wa Kitanzania na wameanza kufanya kazi nzuri, wameshavuna zaidi ya mara mbili na wanasema huku ndiko utajiri ulipo na hii yote ni yale mapenzi mema ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya utafiti na tumeanza na Ziwa Viktoria, tumeenda Ziwa Tanganyika na ninaomba nilisemee iwa Viktoria pekee yake. Kwenye Ziwa Viktoria tumefanya utafiti na tuko tayari kupeleka vizimba kwenye eneo la kilometa za mraba 220 kwa ajili ya vijana wa Kitanzania na akinamama ambao wako tayari kufanya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji huu ni muhimu pia tukaelewa, nilimsikia shemeji yangu Mheshimiwa Mwijage akilisemea jambo hili, Mheshimiwa Mwijage, alilisemea jambo hili na ninaomba nimtoe hofu kwenye hizi hekta 220 ni sawa na asilimia 0.63 tu ya Ziwa letu Viktoria ambayo ipo tayari kwa ajili ya ufugaji wa vizimba. Kwa hiyo, nimtoe hofu bado tuna eneo kubwa ninaomba tuwaite wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi yetu kwa pamoja tuweze kuifikia fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili, kwa sababu tuna nakisi kubwa ya upatikanaji wa samaki ndani ya Taifa letu. Mahitaji ya samaki kwa mwaka ni tani milioni moja, laki tano na senti kadhaa, lakini tunachoweza kukivuna ni tani 400,000 tu. Kwa hiyo bado tuna upungufu mkubwa, tuna nakisi kubwa lakini tuna maji mengi ndani ya Taifa letu, tuwaite wawekezaji wote wa ndani pamoja na wa nje ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja aliyoisema shemeji yangu Mheshimiwa Mwijage, aliishauri Serikali na ninamwomba sana sana tuelewane kwenye jambo hili ili tusafiri wote pamoja kwenye ngalawa hii ya maendeleo ambayo ameianzisha Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nalo ni kwamba, Serikali imeshauriwa kutokupunguza tozo ya kuingiza samaki kutoka dola za Marekani 2.5 hadi 0.5 kwa kilogramu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuelewa shemeji yangu lakini ninaomba nimwambie bado tuna nakisi kubwa na bei ya samaki ni kubwa ndani ya Taifa letu. Wizara tumepewa jukumu la kuwahudumia Watanzania ni muhimu tukashirikiana kwa pamoja ili tuwawezeshe Watanzania kupata samaki kwa bei nafuu, lakini tukiendelea kulinda uwekezaji uliofanywa na Watanzania ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii *quarter* ambayo tumeruhusu samaki kuletwa kutoka nje ya nchi, hatujaruhusu samaki aina ya *tilapia*, aina ya sato hatujaruhusu. Hii yote ni kuwalinda wawekezaji wetu waliowekeza ndani ya nchi yetu. Hii yote pia tunakwenda kulinda viwanda vyetu ambavyo tuna viwanda 11 Kanda ya Ziwa, vinavyochakata samaki aina ya sangara, kwa kukosekana kwa *tilapia* na Samaki wengine sasa wananchi wanavua Sangara wakiwa wachanga na viwanda vyetu vinakosa Sangara mwisho wake viwanda vinafanya kazi sasa mara tatu kwa wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani sana kuwalinda wawekezaji wetu wa kwenye viwanda, kuwalinda wawekezaji wetu walioweza kwenye ufugaji wa samaki, lakini kuendelea kuwekeza kwa sababu fursa bado ni kubwa tunayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari, muda umekwisha, nilikuwa ninafurahia viwanda, kwa hiyo ninaomba uhitimishe.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nihitimishe kwa kumwambia Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi wafugaji na wavuvi tunamshukuru sana, hawa wapiga kelele kule nje, ninamwomba Mheshimiwa Rais aangalie aya ya 14 na 15 ya Sura ya 75, pale Mwenyezi Mungu aliposema baada ya *"A'udhu billahi minash-shayṭwani r-rajim* akasema*: Balil-insanu ʿala nafsihi baswirah, Wa lau alqa maʿadhirah''.* (Bali kila nafsi ya mwanadamu inajua kile kilichofanywa na nafsi yake na kila kilichofanywa na ndugu yake.)"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais achape kazi, hawa wanatafuta tu fitna ambazo hazina sababu na tutazishinda, nasi kule Kondoa kwa watani zako tuliwaambia juzi walipofika, walipofika tuliwaeleza wazi sisi tuta-*tick* Oktoba, 2024. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Jerry William Silaa, nifanye marekebisho ningependa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo afuate baada ya Jerry Silaa *and then* tutaenda kwa Mheshimiwa Mbarawa. Mheshimiwa Jerry Silaa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu kwa hoja iliyoko mezani. Awali ya yote ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali kuwa sehemu ya Bunge la Kumi na Mbili, vilevile aliyenipa kibali kuhudumu kwenye Awamu ya Sita. Jitihada hazizidi kudura, kudra ya Mwenyezi Mungu ndiyo imetufikisha hapa ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua na kuniamini kumsaidia kazi kwenye Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wizara ambayo inabeba maono na ndoto za vijana wengi, vijana maarufu kama *Gen Z*, vijana

wabunifu na matumizi makubwa ya TEHAMA katika huduma za Serikali na huduma binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wachangiaji waliozungumza leo na siku zilizopita kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa alizofanya katika kutekeleza miradi ya kimkakati nchini na hakuiacha nyuma sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka wa Fedha 2020/2021 bajeti ya Wizara hii ilikuwa shilingi bilioni 15 kwa mwaka mzima. Hoja iliyoko mezani ina sehemu ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha2025/2026, Bunge hili lilipitisha bajeti ya shilingi bilioni 291, kutoka bilioni 15 wakati anaingia madarakani mpaka bilioni 291, ongezeko la 1840%, ni mambo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amefanya mageuzi mengi, mageuzi ya kisera tuko katika hatua za mwisho za kutunga sera mpya ya TEHAMA mwaka 2025, mageuzi ya kisheria, mwaka 2022 Bunge hili lilitunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na ilianzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye dunia ya leo *data is a new gold*. Kwa hiyo, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeliona hili na kutunga sheria hii kwa ajili ya kulinda *Data* za Watanzania ili wanaoweza kuzichakata, wazichakate kwa utaratibu na Watanzania wanaoweza kuzitumia kama rasilimali wazitumie kujiingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizotengwa zinaenda kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wizara hii ilipewa maelekezo ya kuhakikisha mifumo inasomana, mpaka ninasimama hapa mbele ya Bunge leo jumla ya mifumo 898 inasomana, katika mifumo hiyo, mifumo 514 ni ya Serikali na mifumo 384 ni ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii imefanywa na kazi inaendelea kufanywa na kwenye bajeti hii umeona Waziri akipewa mapendekezo

ya kurekebisha sheria ili Taasisi za Serikali zisitozwe fedha zinavyotumia namba ya *NIDA* ya Mtanzania. Haya ni mageuzi makubwa, yanaenda kusogeza huduma kwa Mtanzania, yanaenda kufanya Tanzania ya kidigitali iweze kutendeka na kuweza kumsaidia mwananchi na kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya miaka minne hii na miezi mitatu amejenga jumla ya kilometa 3,621 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufanya ujenzi huu kufikia 84% ya kilometa 4,442. Amejenga vituo vya kutolea huduma 111 ni 100% ya malengo tuliyojiwekea, amefanya jumla ya mkongo wa nchi nzima kufikia kilometa 13,820 kati ya mkongo wote wa Taifa wa kilometa 16,280. Haya ni mageuzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo umeongezwa uwezo toka 200*GBPS* mpaka 2,000*GBPS (two terabits per second)*, hii ni kazi kubwa. Mkongo umeungwa na Mozambique, mkongo umeungwa na Malawi; mkongo umeungwa na Uganda na sasa tuna Mradi wa kuunga Mkongo na Nchi ya Kongo *(DRC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza tumeanza kuuza *internet*, tunauza *30GBPS* Malawi, 20 kwa kampuni ya Serikali na 10 kwa kampuni ya *NTN* Malawi. Tumesaini mkataba na kampuni ya Somanga kuuza *MBPS* 100 nchi ya Uganda. Tukiunga na Congo tukiongeza nguvu na tuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya *TTCL* kuongeza nguvu ya kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni kazi tunayoenda kuifanya kwa bajeti tuliyopitishiwa hapa na hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema, katika sekta ya posta mwaka 2022 Mheshimiwa Rais aliendesha operesheni ya anuani za makazi. Jumla ya makazi 12,855,991 yametambuliwa na tunaendesha zoezi la uhakiki jumla ya makazi 535,000 yamefanyiwa uhakiki. Tumeunda Mfumo wa *NaPA*. Mfumo wa *NaPA* ni *Google Map* ya Kitanzania. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tupakue mfumo huu, tuwahamasishe wananchi wetu, leo ukitaka kufika eneo lolote la Tanzania unaweza ukafika kwa mfumo wa Kitanzania. Waheshimiwa Wabunge tarehe 28 kuna kazi inaanza, ukitaka kufika kwa Balozi wa

Shina, ukitaka kufika kwenye Tawi mfumo huu unaweza kusaidia kufika kidigitali hiyo ndiyo Tanzania ya Kidigitali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 29 Julai, 2024 Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua mkakati wa Tanzania ya Kidigitali *(Tanzania Digital Economy Strategy)* ya miaka 10, toka mwaka 2024 – 2034. Mkakati huu unatekelezwa na una nguzo sita na Wizara imejipanga kikamilifu katika kuhakikisha nguzo hizi zinafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamechangia hoja mbalimbali na wako walioonesha maeneo ambayo Wizara inatakiwa kufanyia kazi, ninaomba kulitaarifu Bunge lako na kuliondoa shaka, Wizara imejiapanga kwenye eneo la *Emerging Technologies* (Teknolojia zinazoibukia), *Artificial Intelligence* (Akili Unde). Wizara imejipanga na tuko katika hatua za mwisho za kuandaa *Artificial Intelligence Strategy* ya Taifa (Mkakati wa Akili Unde) ambao utasaidia kuweza kufanya matumizi bora zaidi ya Akili Unde (Akili Mnemba) katika kuletea maendeleo Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kampuni changa - *Startups* ambazo zinaajiri vijana wengi wabunifu. Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa *Incubation Hubs* nane nchi nzima kwenye Majiji makubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha, Lindi na Zanzibar. *Innovation Hubs* hizi zinaenda kuwasaidia vijana wetu wabunifu kuweza ku-*incubate innovation* zao kuweza kuwasaidia, tunafanya kazi kwa karibu na *Startup Association (TSA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara vilevile, tumepewa jukumu la kuandaa Sera ya *Startups* ambayo imeshaanza kufanyiwa kazi na Dkt. Samia Suluhu Hassan nia yake na maelekezo yake ni kuona vijana hawa wabunifu, bunifu zao zinalindwa, bunifu zao zinasaidiwa na zinaenda kutoa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la *PAPU* Arusha limekamilika ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita, tarehe 2 Septemba, 2024 Mheshimiwa Rais mwenyewe amelizindua. Iko taasisi

kubwa inaanzishwa hapa Dodoma, *Digital Tanzania Institute (DTI)*. Taasisi hii nia yake, ni taasisi pekee itakayokuwa na uwezo wa kuchukua vijana walioko kwenye sekta ya elimu na wale wabunifu ambao hawajapata kwenye mfumo wa elimu kuweza kuwasaidia, kuwafundisha, kuwaelekeza na kuwasaidia ili bunifu zao ziende kufanya kazi ya kuwatengenezea ajira, hayo ndiyo mafanikio, hiyo ndiyo kazi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ni nyingi, maeneo ni mengi, lakini ninaomba kusema kwamba, katika kipindi cha miaka minne na miezi mitatu ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi kubwa imefanyika kwenye mawasiliano. Minara ya simu imejengwa, *Mobile Broad Band* imetanuka, minara 758 inayohudumia Watanzania 8,500,000 imekamilika, ujenzi wa minara 636 inayohudumia Watanzania 2,500,000 inajengwa, jumla ya Watanzania 11,000,000 ambao kabla Dkt. Samia hajaingia madarakani walikuwa hawapati mawasiliano ya *internet* kwenye simu ya *3G* na *4G,* leo wanakwenda kupata mawasiliano ni kazi kubwa. Nasi wa mawasiliano tunaungana na wachangiaji wote na Watanzania kwamba Oktoba tuna-*tick*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni shukrani. Shukrani kwa Wizara yangu sifanyi kazi mwenyewe nina Naibu Waziri wangu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Wizara na Wakuu wa Taasisi zote Saba tunazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika huyu ni mtu mwenye roho ya kipekee, sisi ambao tumepata bahati ya kufanya naye kazi tunajua moyo wake na upendo wake kwa Bunge hili. Tunajua moyo wake na upendo wake kwa Wabunge, tunajua moyo wake na upendo wake kwa Taifa lake. Niungane na wenzangu kuwaomba wananchi wa Uyole waturudishie Spika huyu, waturudishie kiongozi huyu, nami nitaungana na wale wote wanaosema ikipendeza chama kumleta hapa siamini kuna mtu atakayekuwa na pingamizi ya yeye kurudi kukalia kiti hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Naibu Spika Mheshimiwa Zungu, Mbunge Ilala ambaye ni Mbunge mwenzangu wa Wilaya ya Ilala. Nikushukuru wewe na Wenyeviti wenzako. Ninamshukuru Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mbunge Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kwa usimamizi na maelekezo, yeye pamoja na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wake wanaotupa maelekezo sisi kama Wizara. Mheshimiwa Kakoso ni Mwenyekiti mtulivu, anatulea, anatuelekeza kwa sauti ya chini, lakini kwa maelekezo ambayo anasimamia kidhati na amekuwa msukumo mkubwa katika utendaji kazi wa Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombee dua njema Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili ambao tumeishi vizuri pamoja kwa upendo kwa miaka mitano, ninawaombea mema, nichukue sura zote zile alizozisoma Mheshimiwa Ashatu Kijaji, kwa sababu ya muda, ninaamini wote tutarudi hapa mwezi Novemba kwa kazi kubwa ambayo Dkt. Samia ameifanya na ameifanya kwenye majimbo yetu, tutembee kifua mbele, tukayaseme kwa uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso ameniambia nilimwomba msemo mmoja, anasema mtu akikaribia kufa lazima atupetupe mikono na miguu, hawa wanaosema huko mtaani ni kauli ya mtu anayekaribia kufa, lakini kazi kubwa imefanyika, Wabunge watembee kifua mbele, waende wakayaseme na Mwenyezi Mungu atufanyie kila la kheri, tukutane hapa mwezi Novemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jerry Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza awali ya yote ningelipenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola kwa mara nyingine ametupa kibali tukiwa katika dakika za lala salama katika Bunge letu hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa letu hili. Sisi Watanzania tunajivunia sana na hasa maelekezo yake na kazi yake ambayo imetukuka sana na Watanzania wanajivunia kwa umahiri mkubwa wa uongozi ambao unaacha alama ndani ya Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wetu wa Bunge, Mama mchapakazi na Mungu amfanyie wepesi sana kiasi kwamba tunamuhitaji katika Bunge hili lakini na dunia vile vile inamhitaji sana. Mheshimiwa Spika tunamshukuru sana pamoja na Naibu Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana pia, Mheshimiwa Mwenyekiti wangu. Leo uko katika Kiti lakini katika Kamati ndiyo Mwenyekiti wangu wa Kamati. Nikushukuru sana kwa miongozo yako mahiri na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati tumekuwa katika kipindi kizuri zaidi cha kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele katika upande wa viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yatakuwa madogo na hasa katika upande huu wa tasnia ya biashara. Hivi karibuni tumeendelea kufanya kazi kubwa kuhakikisha Watanzania wazawa tunawawekea misingi mizuri wafanye biashara vizuri na ndiyo maana katika hotuba ya bajeti hii imeainisha wazi kwamba kutakuwa na mabadiliko ya Sheria, Sura ya 108 katika Ibara ndogo ya 4(3) kuondoa kifungu kile, kuruhusu biashara ziweze kufanyika kuzuia wataalam wetu wakati mwingine wanaofunga biashara bila sababu ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badiliko lingine tutalifanya katika kifungu cha 8(7). Hiki tutaingiza kifungu kidogo kwa lengo kubwa kuhakikisha kuainisha aina ya biashara ambayo wageni hawapaswi kuifanya ndani ya Taifa letu hili. Eneo hili lilikuwa kilio cha muda mrefu ambalo Bunge hili sasa linaenda kuweka historia kwa mara ya kwanza kuainisha biashara hizi zinazoweza kufanywa na zipi ambazo wenzetu wageni hawapaswi kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu siyo ubaguzi, hii kokote inapotokea katika nchi mbalimbali lengo kubwa ni kwamba kuangalia watu wahusika wa eneo hilo watanufaika vipi katika maeneo hayo. Katika eneo hili ninaomba niwashukuru sana Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo kwa kazi kubwa ambayo tumeendelea kuifanya pamoja kuhakikisha kwamba tumeainisha kwa pamoja kuona kwamba jinsi gani Watanzania katika maeneo mbalimbali (ile pale ndiyo ilikuwa kama ndiyo *reference point*), maana yake tutatoka pale itaenda katika maeneo mbalimbali na hasa katika eneo hili linalokuja na mwongozo maalum kuhakikisha aina gani za biashara haziwezi kufanywa na watu ambao siyo wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe Watanzania, hii ndiyo *commitment* ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo ameahidi kuwalinda Watanzania na ameifanya kwa vitendo sana, sana. Tumpigie makofi sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa mfano sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kama tunavyofahamu vijana wetu kina Mheshimiwa Profesa Ndakidemi hapa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru anafahamu. Vijana kila mwaka wanazalishwa katika vyuo vyetu; hawa walikuwa wataalam wazuri sana wakiwa wanatoa wakufunzi katika maeneo ya vyuo vikuu na leo hii idadi ya vijana inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nimezungumza takwimu zinapanda kila wakati. Mwaka 2021 vijana walikuwa takribani elfu 54.8. Leo hii idadi ya *graduate* inapanda kila mwaka na wameshafikia takribani 67,000. *Absorption capacity* siyo ya Tanzania peke yake, dunia nzima hamna *public sector* itaweza kuchukua watu wote *and especially* katika nchi yetu inayoendelea. Sekta muhimu ni Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ninaona bajeti ya mwaka huu jinsi gani imeainisha suala zima. Tutengeneze misingi mizuri ya kuhakikisha viwanda vyetu vinafanya vizuri nchini mwetu. Sasa kama nchi tumeenda vizuri na katika sera nzuri za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya kipindi hiki cha miaka minne

tumetoka idadi ya viwanda 52,128 tumefika viwanda 80,128 ambalo unaona ni ongezeko kubwa sana katika viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili maana yake nini? Kama nchi tumeanza kujitosheleza katika baadhi ya maeneo. Kwa mfano eneo la mabati; mahitaji yetu ya mabati kwa nchi kwa mwaka ni tani 130,000. Leo hii viwanda vyetu vya *ALAF*, Kiwanda cha Lodhia, *King Lion* na *MMI* wameweza kuhakikisha kuzalisha idadi ya mabati imefikia tani 260,000. Maana yake ni nini? Tumeweza kukidhi mahitaji ya ndani na kuwa na *surplus.* Katika eneo hili lazima tulinde viwanda ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunashukuru bajeti ya mwaka huu imekuja na mipango mahususi ya kuhakikisha inalinda viwanda vya ndani na hasa katika upande wa mabati. Leo hii angalia hata kiwanda cha *flat glasses.* Sisi leo Tanzania tumekuwa nchi ya mfano, tumeweza kuwekeza viwanda viwili kile cha *Saphire* na kile cha *KEDA* ambayo mahitaji yake sasa yame-*exceed expectation* zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kusafirisha sasa mahitaji yetu mpaka nchi mbalimbali za Afrika mpaka *Middle East.* Eneo hili lazima tulilinde na ndiyo maana nimshukuru sana *Comrade* Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alivyokuja na bajeti ambayo inaakisi mwelekeo wa nchi yetu tufanye vipi. Hii ndiyo sera nzuri ya kuwafanya wawekezaji wawe na *confidence* wanapokuja kuwekeza Tanzania kwamba wataweza kulindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie ndugu zangu, tumeenda mbali. Leo hii ukienda katika Bwawa la Nyerere na Mradi wetu wa *SGR* ambapo idadi ya nondo zinazotengenezwa zote zinazalishwa nchini. Tuna viwanda takribani 24 nchini mwetu ukianzia kiwanda cha Lodhia, Kamal, MMI na wengine wengi. Leo hii tunaweza kuzalisha nondo ambazo zinatosheleza zaidi ya 200% bado tunatakiwa tuzipeleke nje ya nchi na ndiyo maana Serikali imekuja na mipango jinsi gani kulinda tasnia hii. Eneo hili maana yake siyo ubaguzi, lengo ni kwamba kuwalinda Watanzania. Tukishindwa kulinda bidhaa hizi wenye viwanda watashindwa kuendeleza viwanda, vijana watashindwa kupata ajira, nchi yetu itakuwa siyo nchi salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa mara nyingine. Amekuja na bajeti ya mikakati ambayo inatafsiri dhana ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha viwanda hivi tunalinda. Ndugu zangu ninaomba niwaambie kazi kubwa inaendelea. Leo hii hata kwa mfano upande wa *cement, demand* yetu ni tani milioni nane. Leo hii *production* yetu karibuni tumefika tani milioni 10. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaenda kujitegemea zaidi na maana ni kwamba tunapofanya sera kama hizi tunawapa *confidence* wawekezaji na vijana wetu tunatengeneza misingi mzuri ya ajira. Hatupaswi kuwa wachuuzi wa biashara za wengine, lazima tutengeneze misingi ya biashara za kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndugu yangu Mheshimiwa Bashe inawezekana atakuja kuzungumza katika tasnia ya sukari. Kumbukeni tulivyokuwa tunahangaika miaka ya nyuma. Leo hii unaona jinsi gani sera nzuri zimesaidia suala zima la uwekezaji viwanda vya sukari. Kiwanda chetu cha Kagera (kaka yangu Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru yuko kule) uzalishaji wake unapanda leo karibu tani 130,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Kilimanjaro Sugar* tumeenda kuweka jiwe la msingi pale na *expansion* yake inatoka tani 130,000 mpaka tani 270,000. *Bagamoyo Sugar* kiwanda *capacity* yake ni tani 50,000 lakini *Kilimanjaro Sugar* leo hii ni tani 100,000 ambayo hii unaona kwamba ni jinsi gani maeneo mbalimbali tunaenda kuondoa matatizo ya kufanya *importation* katika baadhi ya maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama nchi tulinde biashara zetu. Ndugu zangu ninaomba niwape habari njema. Mara ya kwanza nchi inaweka historia katika upande wa viwanda, Bunge hili limelia na Mabunge mengine yamelia suala la miradi mikubwa ya vielelezo (Mradi wa Engaruka na mradi wa Mchuchuma na Liganga). Nikushukuru kwa hili, wewe umetoka Mkoa wa Njombe umelisimamia kwa vitendo katika Kamati yako ya Bunge. Leo hii ndugu zangu tunaenda kuweka historia Mungu akijalia huenda mwezi Septemba tunaenda kuweka jiwe la msingi la Kiwanda cha Mchuchuma na

Liganga *for the time;* haijawahi kutokea. Hii ni kazi kubwa inayoendelea na ni *outstanding performance* katika Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi ya Engaruka tumeshamaliza taratibu zilizobaki na si muda mrefu tutapata muwekezaji na kuhakikisha tunazalisha magadisoda. Hii maana yake ni kwamba nchi inaenda kujitegemea zaidi na maana yake tunaweka misingi mizuri ya kuwa *exporters* zaidi kulikoni kuwa *importers*. Pia, tunaenda kutengeneza misingi ya heshima ya nchi inayojitambua na nchi inayoweka vielelezo kuhakikisha kwamba wananchi wake wanalindwa. Niwaombe Watanzania tunapoenda katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 mafanikio haya yote hayawezi kujivunia nayo kama tutashindwa kulinda amani yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani ndiyo jambo la msingi. Bajeti hii Mheshimiwa Dkt. Mwigulu aliyoiwasilisha hapa na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo mpango wa nchi yetu; yote haya yatafanikiwa endapo amani inakuwepo. Tuangalie mataifa mengine leo hii, watu mabwana wamedhalilika wanakuwa watwana ni kwa sababu amani imetoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwombee sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameonyesha mfano wa Rais ambaye anafanya kwa vitendo sana. Watanzania niwaombe tutumie fursa hii tulinde amani yetu tusikubali hata kidogo. Kama kuna yeyote katika njia moja au nyingine anataka kuhatarisha amani ya nchi yetu hasa tunapoelekea katika uchaguzi tusikubali hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana na hakika Waheshimiwa Wabunge wanafahamu hii sasa ni lala salama kuamkia gazetini. Waheshimiwa Wabunge wote tuombeane, tuna siku chache tuombeane na kila mtu anatamani kurudi hapa. Tuombeane sana na mimi sina mashaka kwa kazi hii kubwa iliyofanyika ndani ya nchi yetu, Watanzania wataona. Watanzania wameshuhudia kwamba hii kazi imefanyika kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni na Mheshimiwa Deus Sangu ajiandae.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii ya kipekee kwanza kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu na kutimiza miaka minne katika Uongozi wake imara na wenye maono makubwa ambao umeleta maendeleo makubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na masuala mengine Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kuendeleza sekta mbalimbali za maendeleo hapa nchini ikiwemo Sekta ya Usafiri, Usafirishaji na Usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tumekuwa mashuhuda na tumeona uthubutu mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza na kusimamia miradi ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR*, ujenzi na uboreshaji wa mabandari nchini, ujenzi na uendelezaji wa Sekta ya Usafiri majini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa meli, uboreshaji wa kampuni yetu ya *Air Tanzania* ikiwemo na ununuzi wa ndege za kisasa za *Air Tanzania* pamoja ununuzi wa rada za kisasa kwa ajili ya utabiri wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ninapenda kutumia nafasi hii vilevile kuwashukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa

Naibu Waziri Mkuu kwa maelezo yake mbalimbali wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa wanayofanya na michango yao mikubwa ambayo wametupatia katika bajeti hii hasa kwenye eneo la Sekta ya Uchukuzi, Sekta ya Usafirishaji na Sekta ya Usambazaji kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite zaidi kwenye mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Eneo la kwanza ambalo tumepata mafanikio makubwa na la kujivunia ni ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeandika historia katika Afrika na nje ya Bara la Afrika kwa ujenzi mkubwa wa Mradi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* pamoja na uendeshaji wa reli hiyo ya kisasa. Hatua hii ni kubwa na ya kupongezwa kwani imekuwa ya kipekee tangu tupate uhuru wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nijikite kwenye eneo la uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR*. Ninaamini katika Bunge hili kila mmoja wetu amepata fursa ya kutumia usafiri wa reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma au kutoka Dodoma kuja Dar es Salaam. Usafiri wa reli hii ulianza tarehe 14 Juni mwaka jana kwa kuanzia kipande cha Dar es Salaam mpaka Morogoro halafu tarehe 25 mwezi Julai kwa kuanzia Dar es Salam mpaka Dodoma na safari hizo ni nzuri na Watanzania sasa wanafaidika na usafiri huo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatumia saa tatu na nusu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma au Dodoma kwenda Dar es Salaam. Zamani tulikuwa tunatumia saa nane mpaka saa tisa. Sasa maisha ya Watanzania yamebadilika hasa kwenye Sekta ya Usafiri na Usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuliambia Bunge lako Tukufu au kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwezi wa Julai yaani mwezi unaofuata tutaanza usafiri au usafirishaji wa mizigo kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma. Tunaamini usafiri huu utapunguza kwa asilimia kubwa ajali zinazotokea barabarani hasa katika ya Dar es Salaam mpaka Dodoma na pia zitapunguza msongamano wa magari kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani kipande cha kwanza cha kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro chenye urefu wa kilometa 300 ulikuwa 83%, leo hii imefikia 99.7% na reli hiyo sasa inatumika kwa ajili ya kutoa huduma kwa Watanzania. Kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora chenye urefu wa kilometa 422 wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani kilikuwa 57.7%. Leo hii tunavyozungumza kipande hicho tayari kinatoa huduma kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vipande vingine; (kipande cha Makutupora - Tabora chenye urefu wa kilometa 368, Tabora - Isaka yenye urefu wa kilometa 165, Tabora - Kigoma yenye urefu wa kilometa 506, Isaka - Mwanza yenye urefu wa kilometa 344 na Uvinza - Msongati - Gitega huko Burundi yenye urefu wa kilometa 244) vipande hivi vyote wakati Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani vilikuwa havipo na havijaanza kujengwa. Leo hii wakandarasi katika maeneo yote wapo *site* na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni eneo la ununuzi wa ndege. Mheshimiwa Rais toka aingie madarakani tumenunua ndege saba za kisasa ambazo zinatumiwa na *Air Tanzania* na kuifanya *Air Tanzania* kwa sasa iwe ndege mpya takribani 15. Pia, kwa sasa *Air Tanzania* inakwenda vituo 27 ukilinganisha na vituo 25 ambavyo ilivihudumia mwezi Machi mwaka 2021 kabla Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan hajaingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio au faniko la tatu ni kuendelea kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji katika Maziwa

Makuu. Serikali wa Awamu ya Sita tumejipanga na tunaendelea na uboreshaji na ujenzi wa meli mbalimbali kwenye Maziwa Makuu (Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria). Meli ya *MV* Mwanza Hapa Kazi Tu inaendelea vizuri na hivi sasa tunavyozungumza imefikia 97.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani kazi ya ujenzi ilikuwa ni 40%, lakini tunaamini kwa *speed* inayokwenda hivi karibuni mwisho wa mwezi Julai itakuwa imemalizika. Wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani, Meli ya *MV* Umoja ilikuwa haifanyi kazi, lakini sasa meli hiyo inafanya kazi na inachukua mizigo kutoka Tanzania kwenda Uganda na Kenya na ina uwezo wa kubeba takribani tani 1,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli kongwe ya *MV* Liemba sasa hivi inafanyiwa ukarabati na imefikia 15% wakati Meli ya *MV* Sangara tayari imeshakamilika ama imefikia 98% na inafanya kazi kutoa huduma kati ya Tanzania na huko DRC Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kujenga meli za kisasa ambapo meli mbili za mizigo zitajengwa; moja itatoa huduma Ziwa Tanganyika na ya pili itatoa huduma Ziwa Victoria. Huko Kigoma tunajenga kiwanda cha kisasa cha kujenga meli ambapo takribani shilingi bilioni 630 zitatumika kwa ajili ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine yaliyopatikana ni uboreshaji wa huduma za bandari nchini. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumefanya maboresho makubwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara na bandari za maziwa makuu. Pia, tumefanya kazi kubwa ya kushirikisha Sekta Binafsi katika uendeshaji na uendelezaji katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai Mwaka wa Fedha 2021/2022, shehena ya mizigo iliyohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam ilikua kwa 15.23% kwa mwaka kutoka takribani tani milioni 20.78 zilizohudumiwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani milioni 27.55 zilizohudumiwa Mwaka wa Fedha 2023/2025. Kwa kasi hii

tunaamini kwamba malengo iliyojiwekea *TPA* ya kufikia tani milioni 30 yataweza kufikiwa mapema kabla ya Mwaka wa Fedha 2029/2030 ambayo *TPA* ilitegemea kufikia lengo hili. Haya yote yamekuja kutokana na uongozi makini na maoni makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika eneo la bandari. Kwa mfano, Mradi wa ukarabati wa Bandari ya Kemondo, Bukoba umekamilika na inafanya kazi. Bandari ya Kibirinzi huko Kigoma umekamilika na inafanya kazi, ujenzi wa Gati ya Malindi, Wafu, ambao upo Dar es Salaam, tunatumia takribani shilingi milioni 559.7. Mkandarasi yuko *site* na inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kujenga matenki ya kuhifadhia mafuta, ili kupunguza gharama ya uingizaji mafuta. Tayari mkandarasi yuko *site,* tunajenga takribani matenki 15 na tutatumia takribani shilingi bilioni 578.6. Hii yote ni kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ujenzi wa Bandari ya *Mbamba Bay* ambao unagharimu takribani shilingi bilioni 75, mkandarasi yupo na anaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi kwenye sekta ya uchukuzi. Ninaomba niishie hapo, lakini nasema kwamba, ninaunga mkono hoja na naitakia kila la kheri Bajeti Kuu hii ya Serikali. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Makame Mbarawa. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Sangu, Naibu Waziri na Mheshimiwa Jumaa Aweso, ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba nianze kuchangia kwenye sekta ya mazingira, hususani, nikianza na eneo la mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu kwamba, changamoto ya mabadiliko ya tabianchi imekuwa inaleta athari kubwa sana katika nchi yetu na dunia kwa ujumla Kwa hiyo, Tanzania kama nchi haiwezi kukaa bila kutafuta namna ya kuweza kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko haya ya tabianchi tumeyashuhudiwa katika maeneo mengi, tumeshuhudia ukame katika nchi yetu kutokana na hali ya hewa isiyotabirika ambayo imeleta athari kubwa katika sekta takriban zote. Tumeshuhudia mito ikikauka na kuathiri sekta ya maji na nishati kwenye uzalishaji wa umeme kupitia vyanzo vya maji, kwenye sekta ya kilimo na hata kuathiri vilevile usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kutokutabirika kwa hali ya hewa huku kumeleta athari za mafuriko ambayo yameathiri uchumi, kumeleta majanga kwa wananchi wetu, miundombinu na hata utalii, fukwe zimeharibika na kadhalika. Kwa hiyo, sisi kama Taifa tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba, tunafanya kila linalowezekana kuunga juhudi za kimataifa na za nchi nyingine ulimwenguni kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichukue fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, kwa habari njema kabisa nchi yetu Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimefanya kazi kwa mafanikio makubwa sana ya kupunguza gesi joto duniani. Gesi joto ambayo inatolewa ama inazalishwa nchini mwetu ni kidogo kuliko gesi joto ambayo inafyonzwa kwa njia mbalimbali katika nchi hii kwa hiyo, nikisema kwamba, Tanzania ni miongoni mwa machujio makubwa ya kufyonza gesi joto nitakuwa sijakosea. Kwa mfano, katika kiwango cha kufyonza ambacho tumejipangia, kulingana na *NDC* (*Natural Determine Contribution*), cha tani milioni 138 mpaka 155 kwa mwaka nikitoa mfano wa mradi mmoja tu, kama ungeweza, ninazungumzia *potential* vilevile sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia Mradi wa Mwalimu Nyerere *Hydro – Power,* huu una uwezo wa kufyonza tani takribani milioni tatu, ni mradi mmoja tu ambao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameukamilisha hivi karibuni. Sijazungumzia Mradi wa *SGR*, sijazungumzia Mradi wa *BRT,* sijazungumzia utitiri wa misitu iliyopo,

*National Park* zilizopo, sijazungumzia takataka zilizozagaa, sijazungumzia *renewables*, sijazungumzia bahari, sijazungumzia mikoko, sijazungumzia kabisa maeneo ambayo ni fursa pana sana ambayo nchi yetu inaweza ikayatumia na ambayo vilevile, hata kama haijayatumika, lakini bado yamekuwa yakitumika siyo moja kwa moja kuweza kukabiliana na changamoto ya gesi joto duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi ni dhahiri kabisa Taifa letu lina haki ya kutumia fursa zilizopo katika kuhakikisha kwamba, siyo tu tunapambana kuweza kupunguza gesi joto duniani wakati ambapo sisi Taifa letu halitoi gesi joto nyingi na linafyonza zaidi ya kinachotoka, lakini liweze kufaidika na fursa mbalimbali duniani kuhakikisha kwamba, zinatumika, ili kuweza kuleta maendeleo mengine ya kiuchumi katika nchi yetu. Katika kufanya hivyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali, lakini kabla sijaeleza hatua hizo ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii ambayo tunaizungumzia kupitia hotuba yake amechukua hatua mbalimbali. Moja katika hatua ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake wamechukua, ni kuhakikisha wanaondoa *VAT* kwenye gesi asilia ambayo inatumika kwenye matumizi ya magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni zuri sana kwa sababu, tukifika mahali tukaweza kuwa na magari mengi ambayo hayatumii mafuta, yanayoweza kutoa gesi joto, siyo tu itasaidia kuongeza mchango wa nchi yetu kupunguza hiyo gesi joto katika anga, lakini kuweza kufanya nchi yetu iongeze mapato kupitia biashara ya *carbon*. Lingine ambalo tumefanya, la kimapinduzi, ni tutakumbuka Mwezi Februari tulifanya mabadiliko ya Sheria na kuweka eneo la mabadiliko ya tabianchi kwenye sheria yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba, sasa miradi yote ni lazima izingatie mabadiliko ya tabianchi. Vilevile katika Bunge hili niliwahi kutoa *commitment* ya Serikali kuhusiana na mabadiliko makubwa ya Sheria ya Mazingira ambayo inaelekea kwenda kufanya Baraza letu la

Taifa la Mazingira kuwa neema. Nilitoa *commitment* ya Serikali kwamba, tutajitahidi kadiri inavyowezekana, ili katika Bunge hili tuweze kupitisha Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa mbele yenu niwahikikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, *commitment* hiyo tuliitoa tukiwa na dhamira njema kabisa. *Commitment* hiyo dhamira yake bado ipo, lakini nisikitike kwamba, dhamira yetu haijatimia kwa sababu, jambo hili ni kubwa sana na linahitaji mchakato wa Kiserikali uliokuwa makini. Kwa hiyo, sisi tunaamini, kama Serikali kwamba, jambo hili litakapokuwa limekamilika litasaidia sana katika mambo mengi ikiwemo kuhakikisha wananchi wanazingatia zaidi Sheria za Mazingira na vilevile kuhakikisha kwamba, uelewa katika masuala ya mazingira, ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji unaimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaambia kwamba, jambo hili lipo katika hatua nzuri. Ni imani yangu katika Bunge lijalo kwa kuwa, dhamira ya Serikali ipo, ikitokea Waziri yeyote ambaye atakuwepo mazingira wakati huo, lakini kama itapendeza Waheshimiwa Wabunge waniombee kwanza Mwenyezi Mungu anijalie niendelee kuwa mzima, niwe hai na katika uchaguzi wa mwezi Oktoba niweze kushinda na kurudi hapa Bungeni na amjalie Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, impendeze anirudishe kwenye Baraza lake la Mawaziri na vilevile anirejeshe kwenye Wizara hii. Akifanya hivyo, tutahakikisha dhamira hii ya kuona kwamba, sheria hii inakuja tunaendelea kuisimamia kwa nguvu zote kwa sababu, ni imani yangu mabadiliko ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kuzungumza, ambalo ni jema katika bajeti yetu, ni 20% ya ushuru wa bidhaa ambayo imeondolewa katika vifaa vya jikoni. Jambo hili linakwenda kusaidia sana kupunguza changamoto ya athari za mazingira zinazosababishwa na vifaa vya kielektroniki na vya jikoni hata kabla ya mabadiliko ya Sheria hii ambayo tunaenda kuyafanya hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yako mambo ambayo tumeendelea kuyafanya bila hata mabadiliko ya Sheria. Kwa mfano, tumefanya kazi kubwa sana ya kuweza kuwa-*activate* wale Maafisa

wa Mazingira kwenye Halmashauri kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI, ili waweze kusaidia kufanya kazi kwa pamoja na Maafisa wa Mazingira waliopo katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhakikisha kwamba, wanatekeleza wajibu wao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza kuhusu umuhimu na ulazima wa nchi yetu kutumia fursa katika eneo la mabadiliko ya tabianchi. Moja katika jambo ambalo ninataka nichukue fursa hii kulipongeza Bunge lako Tukufu ni mbali na ukweli kwamba, kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya ya kufungua nchi yetu na kujenga mahusiano mema ya Kimataifa, amefanya tuweze kufaidika na fursa nyingi sana kufikia Mifuko mbalimbali ya Mazingira, ikiwemo *GEF, GCF, Climate Change Fund* na mingine mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo Bunge lako hili Tukufu limefanya, ni la kihistoria na linastahili kupongezwa sana. Jambo lenyewe ni kupitisha Sheria ya kukitambua Kituo cha *NCMC* cha *Carbon* kilichopo Morogoro. Jambo hilo limeleta mafanikio makubwa sana katika muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kupitishwa Sheria ile nimepata mialiko ya Mawaziri wenzangu wa mazingira wa nchi takribani tatu ulimwenguni; nimekwenda katika Nchi za Japan, Norway na Denmark. Katika ziara hizo mambo ambayo tumeyafanya ni kusaini mikataba ya makubaliano na ushirikiano katika biashara ya *Carbon,* jambo ambalo kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii, chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumefanikiwa kuweza kupata masoko na bei za uhakika hata kwa ile miradi ambayo imekuwa si kivutio kwa sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda mfupi ujao tunatarajia kuona mchango mkubwa sana wa sekta ya mazingira, hususani katika eneo la *climate change* kwenye pato la Taifa na itakwenda kuchangia kwa kiwango kikubwa haya mapinduzi ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya kwa muda mfupi.

Ni mapinduzi ambayo yanastahili sana kupongezwa kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ambayo Bunge hili limeyafanya yanakwenda kufanya sasa tuwe na *registry,* ambayo itasababisha kuwe na uwazi na kuondoa ujanja ujanja uliokuwa unaendelea katika biashara hii ya *carbon* kwa muda mrefu. Nataka nikuhakikishie kwamba, katika kufanikisha hayo tutakuja kuona mafanikio makubwa sana katika siku siyo nyingi zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulichangia, kwa haraka haraka, ni masuala mawili kwa sekunde moja moja. Moja ni suala la uchumi wa bluu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa fanya haraka muda umekwisha. Hebu kamilisha hiyo haraka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Suala la uchumi wa bluu; naipongeza Serikali kwa kupitisha sera na katika mabadiliko mliyoyazungumza ya Sheria itakuja vilevile, itaambatana na *component* ya Sheria ya Uchumi wa Bluu, jambo ambalo litahakikisha kwamba, linaipa nguvu Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kuratibu eneo la mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia haraka haraka kwenye suala la Muungano. Ninaomba nichukue fursa hii kuwahakikishia wananchi kwamba, ni muhimu sana tuendelee kuhakikisha tunalinda na kuuimarisha Muungano wetu. Misingi ya amani, utulivu, umoja, mshikamano na maendeleo ya nchi hii yanatokana na Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Nilimwita Mheshimiwa Deus Sangu, Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso, Mheshimiwa Festo Dugange, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Awali ya yote ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye amenijalia leo kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuchangia katika hoja hii. Pili ninamshukuru sana na kumpongeza Spika wetu wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson, na wasaidizi wake kwa kazi nzuri walizofanya na kusababisha Bunge hili la Kumi na Mbili linalofikia katika kikomo chake kuweza kufanya kazi yenye mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pia, ninawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wametupa ushirikiano, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; hapa kipekee ninatambua mchango wa Wabunge wawakilishi wa wafanyakazi, Mheshimiwa Kamishna Janejelly na Dkt. Alice Kaijage, wamekuwa karibu sana kuwasemea watumishi masuala yanayohusu watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika mambo makuu mawili; namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita ilivyofanya mapinduzi makubwa kwenye sekta ya utumishi wa umma na katika eneo la utawala bora. Nitaanza kwenye utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo makubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiyasema ndani ya Bunge hili kwa sauti na unyenyekevu mkubwa ambao Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitusikiliza na kwenda kuyafanyia kazi kwa haraka. Tumepata mafanikio makubwa sana kuwahi kutokea kwenye sekta ya utumishi wa umma katika kipindi hiki cha miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi, tulikuwa tunasema sana juu ya watumishi wa umma kupandishwa vyeo. Watakumbuka kilipita kipindi hapa zoezi hili lilisitishwa kupitia uhakiki wa vyeti feki na watumishi hewa, lakini katika kipindi chake cha miaka minne Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alikuja kwa kasi kubwa sana akalirudisha hili zoezi la upandishaji vyeo na kwa kipindi hiki cha miaka minne tayari jumla ya watumishi 476,470 walimepandishwa vyeo na fedha ambazo zimetumika katika zoezi hili ni shilingi bilioni 689.9. Ni mafanikio makubwa sana ndani ya kipindi hiki cha muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na kelele nyingi hapa Bungeni na Wabunge wengi wamekuwa wakipaza sauti juu ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi, ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya kwa kasi kubwa sana. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Mheshimiwa Rais amelipa jumla ya shilingi bilioni 318.3, kwa ajili ya watumishi wastaafu wapatao 187,152, lakini pia, watumishi wengine wa umma ambao walikuwa wana malimbikizo ya mishahara wapatao 130,443 nao walilipwa kiasi cha shilingi bilioni 226.46 kama malimbikizo ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo kubwa ambalo ndani ya miaka minne ni fedha nyingi ambazo Mheshimiwa Rais ameamua kuzitoa, ili kuondoa kero hii kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, katika Bajeti ya mwaka wa fedha ujao 2025/2026 ataendelea kulipa malimbikizo haya ya mishahara. Kwa mwaka huu tunaoufunga Juni tayari kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuendelea kulipa malimbikizo ya mishahara ambayo watumishi wamekuwa wakidai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameonesha jambo kubwa sana la kiungwana kwa watumishi wa umma hapa Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 alichukua jukumu la kuongeza kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 300,000 mpaka 370,000 lilikuwa ni ongezeko la kama 23.3%. Isitoshe Mei Mosi ya Mwaka huu, 2025, Mheshimiwa Rais pia, amewastaajabisha watumishi wa umma, amepandisha mshahara kima cha chini kutoka shilingi 370,000 mpaka shilingi 500,000 ambayo ni sawa na 35.1%. Ni ongezeko kubwa la kihistoria, halijapata kutokea, mshahara kima cha chini kupandishwa

kwa kiwango kikubwa hivyo cha 35.1%. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuwapenda Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili Waheshimiwa Wabunge walipiga kelele sana kuwatetea watumishi wa umma, wanufaika wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hapa mwalimu wangu, Mheshimiwa Esther Matiko, aliongelea habari ya watumishi waliokuwa wanakatwa tozo ya asilimia sita kwenye mikopo waliyokopa. Mheshimiwa Rais amewasikiliza Waheshimiwa Wabunge na amefuta ile tozo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na kufanya hivyo, Serikali ime-s*acrifice* shilingi trilioni1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa Mheshimiwa Rais hawahurumii hawa watumishi Watanzania, angesema hii shilingi trilioni 1.1 ninaipeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ikafanye mambo mengine, lakini kwa kuwathamini Watanzania, wafanyakazi wa umma, ametoa hii asilimia sita na kusababisha fedha shilingi trilioni 1.1 ikaenda kwa watumishi wa umma na kuboresha maisha yao. Ukiacha hilo, tuliongelea suala la *Pay as you Earn,* ilitoka asilimia tisa kuja asilimia ambayo ni sawa na msamaha wa asilimia moja; sasa mtu anaweza akasema asilimia moja ni ndogo, lakini *impact* yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kila mwaka Serikali ime-*sacrifice* shilingi bilioni 14.78 ambazo zingeingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Mheshimiwa Rais kwa upendo wake mkubwa kwa watumishi wa umma ameacha hiyo asilimia moja iingie kwenye mishahara yao, kama msamaha kwenye *Pay as You Earn.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hapo, Waheshimiwa Wabunge mlilalamika juu ya umri wa wanufaika katika wategemezi kwenye *NHIF* (Bima ya Afya). Rais amesikiliza jambo hili na baadaye akatoa umri wa kutoka miaka 18 mpaka 21 na hii, Serikali kwa kufanya hivyo, tayari walionufaika ni watoto 65,353. Kifedha *implication* yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetumia gharama ya ziada, shilingi bilioni 3.7 ambayo ingeingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Mheshimiwa Rais kwa upendo kwa watumishi wa umma, imeenda

kuwahudumia watoto 65,000 walioongezeka baada ya kubadilisha umri kutoka miaka 18 mpaka miaka 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaishia hapo, kelele kubwa imekuwa ikipigwa ndani ya Bunge hili juu ya ajira mpya, na katika kipindi hiki cha miaka minne Mheshimiwa Rais ametoa vibali vya ajira 149,000; vijana wetu wameajiriwa. Isitoshe, katika bajeti mliotupitishia hapa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tayari Mheshimiwa Rais alituelekeza tuweke bajeti tena katika mwaka ujao wa kuajiri ajira mpya 45,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mafanikio makubwa ambayo yanaonesha dhamiri ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kuwapenda vijana wetu ili waweze kuingia katika utumishi wa umma na kwa kadri fedha inavyopatikana na uimarikaji wa uchumi ameonesha kweli ana upendo kabisa na kutoa vibali vya ajira hizi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la utawala bora. Suala la utawala bora limeimarika kwa kiasi kikubwa sana, na hasa taasisi zetu zinazosimamia dhana ya utawala bora. kwa mfano taasisi yetu ya TAKUKURU Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiongelea sana hapa Bungeni wakisema kwamba wana upungufu wa vifaa. Mheshimiwa Rais alitoa fedha shilingi bilioni 39.17 kwenda kununua magari mapya 195 kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa taasisi yetu ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya magari hayo 88 tayari yameshafika na hivi karibuni yataingia magari mengine mapya 107. Hivi tunavyoenda kwenye michakato ya uchaguzi tayari magari yetu 195 yatakuwa barabarani ili pia zoezi hili liweze kufanyika vizuri, kwa sababu Mheshimiwa Rais pia anapenda uchaguzi huu ukafanyike vizuri na Watanzania waweze kuwapata viongozi waliobora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuiwezesha TAKUKURU Mheshimiwa Rais pia amewezesha ujenzi wa ofisi katika Wilaya Mpya za TAKUKURU, wilaya 22. Ofisi 12 zimeshakamilika na ofisi 10 katika wilaya 10 ziko katika hatua za mwisho kukamilika. Katika mikoa mitano ofisi mpya zimejengwa ambapo ofisi tatu za mikoa mitatu zimekamilika

na ofisi mbili katika mikoa hiyo miwili ziko katika hatua ya mwisho. Vilevile jengo la makao makuu liko katika hatua ya mwisho ambapo litakamilika hivi karibuni na tutahamia katika jengo hilo jipya la TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU pia ilikuwa na changamoto kubwa ya watumishi. Ndani ya kipindi kifupi hiki TAKUKURU imeweza kuajiri watumishi 1,190. Hii inaongeza nguvu ya kwenda kupambana na kuzuia rushwa huko. Kwa hiyo timu hii kubwa imeingizwa; na hivi juzi tu waliajiriwa vijana wapatao 434 ambao wanaingia kazini katika jambo la kupambana na rushwa na kuboresha hii taasisi yetu ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafanikio makubwa yote yaliyofanyika kwenye taasisi hii ya TAKUKURU imeweza kuisaidia TAKUKURU, katika kuzuia tu imeokoa fedha za Serikali zilizorejeshwa Serikalini takribani shilingi bilioni 2.5 ambazo ilikuwa zipotee kutokana na mambo ya rushwa na ubadhirifu. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwekeza kwenye taasisi hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetaifisha pia mali za mazalia ya uhalifu; mali zenye thamani ya shilingi bilioni 35.6 ambazo zinajumuisha viwanja, magari na fedha taslimu. Hii inaonesha namna gani ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa kinara wa upambanaji dhidi ya rushwa hapa nchini. Hii pia imetufanya TAKUKURU katika *rank* ya *Afrobarometer* inayopima viwango vya *improvement* kwenye masuala ya upambanaji na rushwa viwango kwa taasisi yetu ya TAKUKURU katika Bara la Afrika imeenda kukaa viwango vya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninashukuru kwa nafasi hii na ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deus Sangu. Nilikwishamwita Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji; atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI; na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri ajiandae.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nami kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita hadi kufikia Juni 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu ya muda niombe tu kulieleza Bunge lako Tukufu ya kwamba kazi ambazo amezifanya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na mafanikio yake katika nchi yetu ya Tanzania hayahitaji umulike na tochi, yanajiuza yenyewe. Ndani ya Tanzania na nje ya mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maji miaka ya nyuma ilikuwa ni sekta ya kero na ilikuwa ni sekta ya lawama. Katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikija bajeti ya maji palikuwa hapatoshi. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 22 Aprili, 2021 katika Bunge hili Tukufu alitoa maelekezo mahususi katika Wizara yetu ya Maji. Alisema ya kwamba yeye ni mama na asilimia kubwa ya wanaoteseka juu ya adha ya maji ni akinamama; hivyo hataki kusikia na hataki kuona akinamama wa nchi hii wanateseka juu ya adha ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo yale ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuliasisiwa pia na kauli na kudhamiria kwenda kumtua mwanamama ndoo kichwani. Hivyo tulipewa malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kwamba itakapofika 2025 tuweze kutimiza 85% ya upatikanaji wa maji vijijini na 95% ya upatikanaji wa maji mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo nitumie nafasi hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa *reforms* mbalimbali zilifanyika, kama vile mabadiliko ya kisheria, maoni na ushauri mbalimbali chini ya Spika wetu wa Bunge Dkt. Tulia. Tunasema tunawashukuru sana. Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti, Kamati yetu ya Bunge ya Maji na Mazingira wamefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninazungumza hivyo? Ninasema, usione vyaelea ujue vimeundwa. Mafanikio haya yanayoonekana katika Wizara yetu ya Maji yameundwa kutokana na jitihada za Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma katika sekta ya maji miradi ilikuwa ikijengwa chini ya kiwango. Fedha zinatolewa matokeo hakuna. Miradi imejengwa lakini haitoi maji, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kazi ya kwanza ambayo ameanza nayo ni kuhakikisha kwamba miradi 177 ambayo ilikuwa imeainishwa kwamba imejengwa lakini ilikuwa haitoi maji, moja ya maelekezo yake ni kuhakikisha miradi ile inakamilika na watu wanapata huduma ya maji. Ninataka nilieleze Bunge lako Tukufu, miradi ikiwemo ya Bunda, Kigoma, Mradi wa Same Mwanga kazi imemalizika na watu maeneo hayo wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto nyingine kubwa ambayo ilikuwa ikiikumba Wizara yetu ya Maji ni ufinyu wa bajeti. Miradi mingi Waheshimiwa Wabunge wakija Bungeni walikuwa wakilalamika, kwamba miradi ya miaka 1970 haijawahi kukamilika kwa kisingizio cha ufinyu wa bajeti. Kwa mfano, ukienda kule Serengeti kuna Mradi wa Mugumu, umejengwa tangu miaka ya 70 haujawahi kukamilika, umekuja kukamilishwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ameweza kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji kutoka shilingi bilioni 500 leo tunazungumza shilingi bilioni 800. Hapa si tu kutenga bajeti ya Wizara ya Maji, kwa maana ya kuiongeza, lakini pia kutoka kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Wakurugenzi wote. Hakika ukimwona kobe juu ya mti amepandishwa, hapandi mwenyewe. Wizara ya Fedha imefanya kazi kubwa imefanya kazi nzuri ya kutuwezesha Wizara ya Maji ili tuweze kupata haya mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni nadra sana kuona Wizara ya Maji kujenga miradi mikubwa kwa kutumia fedha zetu za ndani, ni nadra sana. Miradi yote mikubwa ilikuwa ikijengwa kutokana na fedha za nje. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uthubutu mkubwa. Tumeshuhudia katika Bunge lako hili kuna maazimio ambayo yaliwahi kufanywa tangu Baba wa Taifa juu ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda na juu ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa, hayajawahi kutekelezwa. Uthubutu

wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan leo yanatekelezwa kupitia Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie Watanzania, ukisoma maandiko ya dini yanasema, *"Wa amma bini i'mati Rabbika fahaddith* (zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru)" Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya hasa kwa makusanyo ya ndani na kuweza kujitegemea. Leo tunaona miradi kila kona ukienda zako kule Mbeya kwa Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia kuna mradi wa zaidi ya shilingi bilioni 119 wa kuyatoa maji ya Mto Kiwira kwa ajili ya kulinufaisha Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi unajengwa kwa fedha za ndani. Ukienda zako Tunduma kuna mradi wa zaidi ya shilingi bilioni 119. Tunaujenga lakini ni kwa uthubutu wa Wizara ya Fedha kupitia makusanyo yake. Ninataka niseme Wizara ya Fedha ipewe maua yake kupitia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hilo, tunaona kabisa uthubutu wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Bunge lako Tukufu miaka yote lilikuwa linazungumza kwamba nchi yetu ya Tanzania siyo maskini wa vyanzo vya maji. Ukienda zako kanda ya Ziwa kuna Ziawa Victoria, Katavi kuna Ziwa Tanganyika, Mtwara kuna Mto Ruvuma, ukija Dar es Salaam, Rufiji, Lindi, kuna Mto Rufiji lakini watu wameshindwa kunufaika kwa muda mrefu juu ya ujenzi wa miradi ya maji mikubwa. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja na uthubutu juu ya uanzishaji wa *National Grid (Gridi ya Taifa ya Maji)* amefanya kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunashuhudia namna alivyoyatoa maji ya Ziwa Victoria ameyaleta Tabora. Siyo Tabora Mjini ameyapeleka Igunga na ameyapeleka Nzega na ameyapeleka Kaliua. Leo anahakikisha hadi kwa Mama Sita kule Urambo, watu wote wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Ziwa ilikuwa ajenda ya Waheshimiwa Wabunge katika Bunge hili. Ukienda Kagera kuna maji ya Ziwa Victoria miradi imetekelezwa, ukienda zako Mara kuna Mradi

mkubwa wa zaidi ya shilingi bilioni 34, lakini kule Mugango-Kiabakari-Butiama kwa Rais Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tumeweza kujenga mradi wa shilingi bilioni 70. Hivi karibuni tumekwenda kuanzisha Mradi mkubwa pale Simiyu wa zaidi ya shilingi bilioni 440, utakaowezesha wilaya zote za Mkoa wa Simiyu kupata huduma ya maji safi na salama. Jiji la Mwanza tumekwenda kuzindua mradi wa shilingi bilioni 70. Huu ni uthubutu wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze kwa takwimu. Nchi yetu ya Tanzania ina vijiji 12,318. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka minne tu tumetoka katika vijiji ambavyo tulikuwa chini ya 50% leo tunazungumzia 83% ya upatikanaji wa maji. Tumeweza kufika vijiji 10,779. Tumebakisha vijiji 1,500. Ametoa maelekezo anasema 2030 wakati anaporudi kule Kizimkazi anataka vijiji vyote vya Tanzania vipate huduma ya maji safi na salama. Amesema kauli yake hiyo kwa vitendo kwa sababu *actions speak louder than words.* Ametununulia mitambo nchi nzima kwa ajili ya uchimbaji visima katika kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anatambua kuwa yapo baadhi ya maeneo ukichimba maji hakuna maji chini ya ardhi. Kwa hiyo ametupatia fedha kwa ajili ya ununuaji wa mitambo. Tumeshanunua zaidi ya seti tano kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa. Kazi tumeshaianza, tumeanzisha programu ya visima 900. Kila Mbunge katika Bunge lako hili ameweza kupatiwa visma vitano. Hayo ni zawadi ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumeweza kuchimba mabwawa zaidi ya 45. Ukienda zako Handeni pale Kwenkambala kazi tumeshaimaliza, ukienda kule Uyui Kizengi kazi tumeshaimaliza na ukienda kule Kwa Mjembe Bagamoyo nako kazi tumeshaimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kwamba Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila mahali. Rais aina ya Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila wakati. Tumempata lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata huduma ya maji safi wanapata maendeleo; na maendeleo ya nchi hii yanaanza

na mimi na wewe katika kuhakikisha kwamba tunaijenga Mama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio hayo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametambuliwa kuwa kinara wa uongozi katika masuala ya maji Afrika *(Pan African Water Sanitation and Hygiene Champion)*. Ni kazi ya kumtua mwanamama ndoo kichwani. Siyo Tanzania tu bali imeweza kuvuka mpaka Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tulikuwa na programu ya malipo kwa matokeo ambayo imeanzishwa na *World Bank*. Nchi mbalimbali tulishindanishwa, kwamba unapopewa fedha ukifanya vizuri unapewa fedha zaidi. Nchi ya Tanzania katika miaka miwili mfululizo ndiyo tunaoongoza katika hii programu. Aliitwa Mheshimiwa wa fedha, kaka yangu, Mwigulu Nchemba pale Ethiopia na kupewa hizo taarifa. Ninataka niwaambie, kwamba kazi iliyofanyika ni kubwa na nzuri. Tumuunge mkono Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jumaa Aweso. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Serikali Kuu ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuwa sehemu ya wachangiaji wa hotuba hii ya bajeti ya Serikali Kuu kwa mwaka ujao wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya. Kazi ya kutukuka ya kuliongoza Taifa letu la Tanzania. Kila mwananchi

amekuwa shuhuda kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi ya kupigiwa mfano na amefanya kazi ya kutukuka ambayo imeandikwa kwa wino wa dhahabu katika historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima aliyonipa katika kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Dhamana hii nyeti, kwa muda wa miaka yote minne. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani aliyonipa na wananchi wa Jimbo la Wanging'ombe. Tunamwombe Mheshimiwa Rais afya njema na tuna uhakika kwamba ifikapo Oktoba mwaka huu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Chama cha Mapinduzi kitakwenda kushinda kwa kishindo katika uchaguzi mkuu, kwa sababu kazi zimefanyika na kazi zinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wametoa michango mingi, lakini ni dhahiri kwamba katika eneo ambao Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali hii ya Awamu ya Sita imeitendea haki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kwenye miradi ya maendeleo katika ngazi za halmashauri na katika ngazi za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamepongeza sana kazi ya ujenzi wa miundombinu ya sekta ya afya, sekta ya elimu, barabara na shughuli zote ambazo zimefanyika katika mamlaka za Serikali za mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari ninaomba nieleze kwa ufupi mafanikio makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nikianza na sekta ya afya ya msingi; hoja nyingi za Waheshimiwa Wabunge zilikuwa za kupongeza namna ambavyo Serikali imeendelea kukamilisha maboma ya zahanati, kujenga vituo vya afya na hospitali za halmashauri na pia kuajiri watumishi wa sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne Serikali imejenga na kukamilisha jumla ya maboma 1,158 ya zahanati kote nchini. Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda, maboma haya yamekamilishwa katika majimbo yetu, pia vituo hivi vimesajiliwa na vinatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi hii miwili mwezi Mei mpaka leo Juni jumla ya shilingi bilioni 17 na milioni 360 zimetolewa kwa ajili ya kwenda kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati 346. Kazi zimeanza katika majimbo yetu na zinaendelea. Hii ni kazi kubwa sana iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili ni endelevu. Tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumekwishatambua jumla ya maboma 1,674 ya zahanati na tumeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yanakamilishwa na yanaanza kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vituo vya afya, katika kipindi cha miaka minne Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka historia ya kipekee kwa kujenga jumla ya vituo vya afya 367 ambavyo vina majengo yote muhimu ya huduma za afya, kama vile majengo ya upasuaji, mashine za *digital X Ray,* pamoja na mashine za *ultra sound.* Leo hii tunaongea wananchi katika kata zetu kote nchini wanapata huduma bora za afya katika vituo vya afya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita Serikali pia imekwishatoa jumla ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kwenda kujenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati 120. Leo tunaongea Waheshimiwa Wabunge wamekwishapokea fedha hizi na taratibu za kuanza ujenzi wa vituo hivi vya afya120 zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la rufaa ngazi ya wilaya, Serikali imeendelea kuboresha hospitali za halmashauri, imeendelea kuboresha upatikanaji wa vifaatiba, imeendelea kuboresha upatikanaji wa magari ya wagonjwa. Katika kipindi cha miaka minne jumla ya hospitali za halmashauri 129 zimejengwa na kupanuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya hospitali kongwe na chakavu 48 pia zimefanyiwa ukarabati mkubwa pia zimewekewa vifaatiba na miundombinu ya huduma za afya bora zaidi ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi. Ni dhahiri kwamba, historia hii imewekewa kipekee kabisa na Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ngazi ya huduma za afya msingi huko nyuma hatukuwa na msamiati wa majengo ya huduma za afya za dharura kwa maana ya *emergency medical department*, hatukuwa na msamiati wa majengo ya *intensive care unit* wala hatukuwa na msamiati wa mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya *oxygen*. Huduma hizi zote zilipatikana ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa, kanda, na hospitali maalum na hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongea katika kipindi cha miaka minne Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan ameweka historia ya kipekee kwa kujenga majengo ya huduma za dharura 86 katika halmashauri zetu, kwa kujenga majengo ya *ICU* 30, kwa kujenga mitambo maalum ya kuzalisha hewa tiba ya *oxygen* 21. Mheshimiwa Rais amenunua vifaatiba *digital x-rays,* amenunua mashine za *ultrasound* na vifaa vingine vya maabara katika vituo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo katika miaka minne hii tulikuwa na hoja moja muhimu ya magari ya wagonjwa *(ambulance)*. Mheshimiwa Rais katika miaka hii minne amenunua jumla ya magari 592 kwa ajili ya huduma za rufaa katika ngazi ya afya ya msingi. Kwa hakika Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana na anastahili kupewa maua yake kwa historia kubwa aliyoiweka katika kuboresha huduma ya afya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya afya imekwenda sambamba na ajira kwa watumishi. Jumla ya watumishi 32,740 wameajiriwa katika kipindi cha miaka minne na kupelekwa kwenye vituo vyetu kwa ajili ya kuboresha huduma za afya. Kwa ujumla katika sekta ya afya katika kipindi cha miaka minne Serikali imepeleka fedha zaidi ya shilingi 1,397,000,000,000; haijawahi kutokea uwekezaji wa aina hii katika sekta ya afya katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *indicator* ya muhimu au kiashiria kikuu katika uboreshaji wa huduma za afya ni kupungua kwa vifo vya akinamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais amepewa tuzo maalum *(The Global Goalkeepers Award)* tuzo adimu na adhimu kwa mafanikio makubwa ya kupunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka 556 kati ya vizazi hai 100,000 mpaka vifo 104 kati ya vizazi hai 100,000. Mafanikio hayo ni makubwa ya kupigiwa mfano katika Bara la Afrika haijawahi kutokea pia Shirika la Afya Duniani *(WHO)* limetambua mchango mkubwa wa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu kumekuwa na utaratibu wa ujenzi wa madarasa, ukarabati wa shule kongwe na katika kipindi hiki cha miaka minne, Mheshimiwa Rais amewezesha ujenzi wa madarasa kutoka 191,708 hadi madarasa 254,393. Amewezesha pia, ujenzi wa shule za msingi mpya kutoka 16,406 hadi shule 17,986. Amewezesha ujenzi wa shule za sekondari kutoka 3,865 hadi shule 4,894, ni kazi kubwa iliyofanywa ndani ya kipindi cha miaka minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja za ukarabati wa shule kongwe. Serikali hii ya Awamu ya Sita, imeendelea kufanya ukarabati wa shule kongwe, imefanya ukarabati wa jumla ya shule 868 kati ya hizo shule 794 ni shule za msingi na shule 74 ni shule za sekondari. Mpango wa elimu bila ada umeendelea kutekelezwa kwa ufanisi wa hali ya juu. Mpango huu unagusa elimu yote ya msingi kuanzia ngazi ya chekechea, ngazi ya elimu ya awali, elimu ya msingi na sekondari kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita. Kazi kubwa imefanyika na ruzuku ya elimu bila ada imeendelea kuongezeka kwa kipindi cha miaka hii minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2021/2022 ruzuku ilikuwa bilioni 243.66 na imeongezeka mpaka bilioni 484.27 ongezeko la zaidi ya 94% ndani ya miaka minne. Tunafahamu ujenzi wa shule za mikoa za sayansi 26 katika mikoa yote 26 na zimegharimu zaidi ya shilingi bilioni 130.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwenye sekta ya barabara ya mijini na vijijini. Kazi kubwa imefanyika kwa kuongeza urefu wa barabara kutoka kilometa 108,446 mpaka kilometa 144,430, lakini kilomita za barabara za changarawe zimeongezeka, barabara za lami zimeongezeka na bajeti ya *TARURA* imeongezeka kutoka bilioni 272 mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka bilioni 888 sasa. Ongezeko hili limewezesha ukarabati mkubwa wa madaraja zaidi ya 348, ujenzi wa makalvati na madaraja ya mawe zaidi ya 197, lakini miradi mingine inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha kazi hii nzuri na kubwa za kupigiwa mfano zimefanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan. Kwa dhati kabisa na kwa hakika Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan anastahili maua yake kwa kazi kubwa na ya kihistoria aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii imefanywa na Waheshimiwa Wabunge hawa wa Bunge hili la Kumi na Mbili linalokwenda kuhitimisha muda wake wiki hii. Kwa hakika Waheshimiwa Wabunge, nao pia wanastahili maua yao, pokeeni maua yao kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya kuwasemea wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni matokeo ya utekelezaji wenye ufanisi mkubwa wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2020. Kwa hiyo, tuna uhakika kwamba mwezi Oktoba Watanzania tuta-*tick* kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuta-*tick* kwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi na tuta-*tick* kwa Waheshimiwa Madiwani wote wa Chama Cha Mapinduzi kwa sababu kazi inajieleza na kazi inaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daktari Festo Dugange. Nilimwita Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri Nishati atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa Daniel Sillo ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee na kwa dhati ya moyo wangu ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika Taifa letu. Wakati Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo anaeleza hapa kuhusiana na Taarifa ya Hali ya Uchumi alieleza juu ya namna ambavyo sekta mbalimbali zimechangia katika ukuaji wa pato la Taifa. Mojawapo ya sekta ambayo kwa kweli imekuwa katika tatu bora katika kuchangia ukuaji wa pato la Taifa, ukiangalia kwa tathmini kuanzia 2014/2015 - 2024/2025 basi ni pamoja na sekta ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ilitoka 5.8% mwaka 2015 na sasa hivi tunazungumzia 14.4%. Jambo hili lisingewezekana bila umadhubuti wa kuendelea kuwekeza katika miradi inayohusiana na sekta ya nishati, lakini isingeweza kufanikiwa bila kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii na jambo hili limefanyika vizuri sana kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika chini ya Serikali ya Awamu ya Sita. Ndiyo maana kwa mwaka huu tumeona namna ambavyo sekta ya nishati imechangia kwa kiasi kikubwa sana katika ukuaji wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizi zote ni za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi tunaendelea kumpongeza sana kwa sababu kwa kipindi cha miaka minne ameweka nguvu kubwa sana katika kuendeleza sekta hii ya nishati na sisi chini ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati tunajivunia uwekezaji mkubwa ambao umefanyika katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mafanikio makubwa sana katika sekta ndogo zote ambazo zipo katika sekta ya nishati. Wizara ya Nishati ama sekta ya nishati ina sekta takribani nne na mojawapo ni sekta ya mafuta pamoja na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka minne tumeshuhudia mafanikio makubwa sana katika suala la gesi asilia. Katika Serikali hii ya Awamu ya Sita tumeendeleza kwa kiasi kikubwa sana miradi ya uzalishaji na uendelezaji wa gesi asilia katika vitalu vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwa kipindi cha hapo nyuma, gesi asilia ilikuwa inatumika kwa kiasi kikubwa sana katika uzalishaji wa umeme na kwa kweli tulifanikiwa kutokana na miradi ya uzalishaji na uendelezaji ambayo ipo katika vitalu vyetu vya gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitalu chetu cha *Mnazi Bay* tumeweza kuzalisha takribani futi za ujazo bilioni 25.51 kwa kipindi cha miaka minne, lakini tumefanya hivyohivyo katika kitalu chetu cha Songosongo. Vilevile, kwa mwaka jana tumesaini mikataba katika kitalu chetu cha Ruvuma Ntorya na sasa hivi tuko katika hatua za awali katika kuzalisha na kuendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii tumepata mafanikio makubwa sana ambayo hayakuwahi kutokea huko nyuma. Kupitia Shirika letu la Maendeleo ya Petroli tumeweza kuongeza hisa zetu katika kitalu chetu cha *Mnazi Bay*. Shirika hili lilikuwa lina 20%, lakini kwa sababu wanahisa wengine walijioa tumeweza kununua hisa kufikia 40% jambo ambalo limetuongezea uendeshaji wetu wa shirika, vilevile litaendelea kutuongezea mapato makubwa sana na kuweza kutufanya tunufaike na rasilimali zetu na tushiriki kwa hatua ya moja kwa moja katika kuendesha rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jitihada hizi zisingefanikiwa bila mkazo wa Mheshimiwa Rais kuendelea kutuhimiza juu ya kuchukua hatua za kuhakikisha tunaendelea kushiriki kwa kipaumbele katika uendelezaji wa rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya gesi asilia ni muhimu sana kwa sababu inachagiza sekta nyingine ikiwemo matumizi ya gesi iliyoshindiliwa katika magari ambapo mradi huu unaendelea vizuri sana kwa kushirikiana na sekta binafsi vilevile kupitia kuunganisha

mtandao wa gesi majumbani, miradi ambayo inafanyika vizuri sana katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yetu ni kuendelea kuwasisitiza Watanzania waendelee kubadili mifumo ya magari ili waweze kutumia gesi asilia kwa sababu ni gesi nafuu, lakini tuunge mkono jitihada za Mheshimiwa Rais za kutunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nyingine ambayo kwa kweli imeendelea kuwa muhimu sana katika kipindi cha miaka minne ni sekta ndogo ya mafuta. Katika miaka hii minne tumekuwa tuna mafanikio makubwa sana katika kusimamia na kudhibiti bei kikomo za bidhaa za mafuta. Bei ya ndani ya bidhaa za mafuta imeendelea kuwa himilivu na Wabunge wanafahamu, Mwaka wa Fedha 2021/2022 tulipitia changamoto kutokana na upandaji wa bei katika soko la dunia. Ni Serikali hiihii ya Awamu ya Sita iliweka ruzuku ili soko la ndani liendelee kuwa himilivu na imekuwa hivyo kuanzia kipindi hicho mpaka sasa hivi ambapo bei zimeendelea kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa kuagiza mafuta ni kupitia Uagizaji wa Pamoja *(Bulk Procurement System)*. Tumewasikia Waheshimiwa Wabunge wa kutushauri juu ya kudhibiti na kuongeza udhibiti katika mafuta ambayo yanakuja kwa ajili ya *transit* na sisi tunakubaliana nao kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki cha miaka minne, tumefanya jitihada kubwa sana katika kuimarisha udhibiti, sisi Wizara ya Nishati lakini kwa kushirikiana vilevile na sekta nyingine. Biashara ya *transit* ni biashara nzuri sana na sisi tunaipenda na ina manufaa makubwa sana kama nchi. Sisi tunaongeza uwekezaji pale katika bandari na kuweka *oil gate* kwa ajili ya kuongeza upakuaji wa meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ni kuweza kutumia fursa kwa nchi ambazo ziko *landlocked* tuweze kuwahudumia na hata 50% hiyo ya mafuta ambayo yanaingizwa bado ni ndogo. Tunafanya uwekezaji ili tuongeze tuweze kupata mapato na tuweze kutumia rasilimali ya bahari ambayo tunayo katika kuongeza mapato yetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo tunalo ni kuendeleza udhibiti na sisi kwa kipindi cha miaka minne tumefanya hivyo. Mafuta yakiingia iko mifumo ambayo tunadhibiti ikiwemo mita za Serikali *(flow meter)* pamoja na mifumo ya kieletroniki *(Scada)*. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika sekta hii ndogo ya mafuta, udhibiti kwa miaka hii minne umeendelea kuimarika na tutaendelea kufanya hivyohivyo na tutaendelea kutumia fursa ya biashara ya *transit* kwa ajili ya kujinufaisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya sekta ambayo ni moyo wa uchumi katika Taifa hili ni sekta ndogo ya umeme. Katika kipindi hiki cha miaka minne nyie wenyewe ni mashahidi mmeona uwekezaji mkubwa sana ambao umefanyika katika sekta ndogo ya umeme. Hapo ulikuwa ukija kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2025, uwezo wa kuzalisha mitambo ilikuwa takribani 1,600, lakini leo hii tumeenda mara mbili tunazungumzia uwezo wa kuzalisha umeme takribani *megawatt* 4,000. Ni uwekezaji mkubwa sana ambao haujawahi kufanyika tangia Taifa hili lipate uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza ku-*double* uzalishaji kupitia Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Jambo hili siyo rahisi linahitaji *consistency* ya *investment,* linahitaji *commitment* ya kutoa fedha na jambo hili Mheshimiwa Rais kwa kweli anastahili pongezi kubwa sana kwa sababu ametuletea uimara mkubwa sana katika sekta nzima ya kuendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ya uzalishaji, lakini ipo miradi ya usafirishaji pamoja na miradi ya usambazaji. Tulikuwa tuna kilometa za usafirishaji takribani 6,000 ilivyofika 2021 lakini mpaka sasa hivi tumeongeza kufikia kilometa takribani 8,000. Usambazaji tulikuwa tupo katika kilometa takribani 144,000 lakini leo tunazungumzia kilometa takribani 200,000. Ni kazi kubwa sana imefanyika katika sekta hii ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji na nyie wenyewe ni mashahidi kupitia miradi ambayo inafanyika katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ambayo tunayo. Tumeongeza matumizi makubwa sana kama nchi. Tumeongeza matumizi takribani *megawatt* 700 kutokea 2021 mpaka 2025. Hiyo ni *alert* kwamba inatupasa kuendelea kuwekeza zaidi katika miradi ya umeme na ndicho ambacho Serikali ya Awamu ya Sita inafanya. Ipo miradi ambayo sasa hivi inaendelea ikiwemo Mradi wa Malagarasi ambao unaenda kuzalisha takribani *megawatt* 34.5. Vilevile upo Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua wa Kishapu ambao unaenda kuzalisha takribani *megawatt* 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na utayarishaji wa kufanya miradi mingine ya uzalishaji ikiwemo Ruhuji na Rumakali, vilevile, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Gesi pale Mtwara, vilevile na miradi ya upepo ambayo pia itatekelezeka. Hii yote ni kwa sababu tunataka hapo mbeleni tusirudi katika changamoto ambayo tulikuwa nayo hapa nyuma na ndiyo maana tumejipanga kwa miradi hii ambayo inatekelezeka sasa hivi na tumejipanga kuanza miradi mingine inayokuja ili kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na umeme ambao unaendelea kuwa himilivu kwa kipindi kirefu kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenyewe ni mashahidi juu ya miradi inayotekelezeka katika vijiji na vitongoji. Kwa kipindi hiki cha miaka minne Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliahidi atamaliza kupeleka umeme katika vijiji na amefanya hivyo. Wakati tunapeleka umeme katika vijiji hivi 4,071 vilivyobakia, tumefanikiwa kupeleka umeme katika vitongoji takribani 14,400 kwa kweli ni kazi kubwa sana imefanyika. Hii inahusisha vitongoji ambavyo sasa hivi vipo katika mradi. Waheshimiwa Wabunge wenyewe wanafahamu kwa sasa hivi tumeanza utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 20,000 na tumeanza sasa hivi kwa kutafuta wakandarasi katika vitongoji vya awali 9,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ni miradi ya fedha nyingi sana na inatekelezeka kwa sababu Mheshimiwa Rais ameamua kuhakikisha kutokana na mpango wetu wa matumizi bora ya nishati kuelekea 2030 tuweze kufikia 100% ya upatikanaji wa umeme vilevile tuweze kufikia 75% ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha, ninaomba kutumia fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta yetu ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kutusimamia vizuri katika sekta yetu. Ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuendelea kutuongoza vizuri hapa Bungeni. Ninaomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta yetu ya nishati. Tusingefanikiwa bila ushirikiano mzuri ambao wametupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwashukuru sana watendaji wetu wa Wizarani Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote na viongozi wote wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati kwa ushirikiano mkubwa ambao walitupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninaomba nilishukuru Baraza Kuu la Vijana la Taifa kwa kuniamini kwa kipindi cha miaka hii mitano kupitia Mwenyekiti wangu, *Comrade* Kawaida Mohamed Kawaida na Katibu Mkuu Jokate Urban Mwegelo kwa ushirikiano mzuri ambao wamenipa katika kipindi cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Mbinga ambao walinipa fursa ya kutumikia Udiwani kwa kipindi cha miaka hii mitano na niwahakikishie ushauri walionipa nimeuchukua na nitaufanyia kazi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Judith Salvio Kapinga. Nilishamwita Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Daniel Sillo, tutamalizia na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa fursa. Pili, ninaomba nitumie nafasi hii vilevile kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na sote kuwa hapa siku ya leo salama, vilevile kutupa uhai wa kuweza kuwatumikia Watanzania na binafsi kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini, mpaka kufika siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ninaomba nitumie nafasi hii vilevile kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa jukumu la kuendelea kuwatumikia Watanzania katika nafasi ya Waziri wa Kilimo, nimshukuru vilevile Naibu wangu na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo kwa *support* ambayo wamenipa kwa siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuunga mkono hoja, ninaiunga mkono hoja kwa sababu zipo sababu za kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Mwenyekiti wa Kamati unayoongoza wewe ambaye mimi ni Mjumbe wa Kamati yako na unafahamu tulikotoka. Mwaka wa Fedha 2021/2022 wakati Mheshimiwa Rais anahutubia Bunge hili Bajeti ya Wizara ya Kilimo ilikuwa bilioni 294, leo tumepitisha katika Bunge hili bajeti ya zaidi ya trilioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya umwagiliaji ilikua bilioni 54 mwaka huu tumepitisha bajeti ya zaidi ya bilioni 360 ya Tume ya Umwagiliaji. Wakati tunaingia hapa Bungeni Mwaka wa Fedha 2020/2021 sote tunafahamu changamoto zilizokuwa zinaikabili sekta ya kilimo, ukuaji wa sekta ulikuwa asilimia 2.4 mpaka asilimia 2.7. Lengo tulilopewa na Mheshimiwa Rais kufika mwaka 2030 ni sekta hii ikue kwa 10%. Mwaka wa fedha 2023/2024 tumefika asilimia 4.2 na Mwaka wa Fedha 2025/2026, tutafika asilimia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anasoma Hotuba hapa mtandao wa umwagiliaji tuliojenga katika nchi hii kwa umri wa miaka 60 ulikuwa ni hekta 560,000, leo tumefika hekta 960,340. Lengo tulilopewa na Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi ni kufika hekta milioni 1.2, hivi sasa Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia inatekeleza jumla ya miradi 780 mipya yenye jumla ya hekta 560,000,

inatekeleza mabwawa 124 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi za awali wakati miaka michache iliyopita; Mwaka wa Fedha 2021/2022 *export value* ya nchi hii katika sekta ya kilimo ilikua ni bilioni 1.2. Mwaka wa Fedha 2023/2024 tumefika bilioni 3.5 dola uzalishaji wa mazao ya chakula ilikuwa ni jumla ya tani milioni 17, lakini leo tani milioni ishirini na mbili. Mwaka wa Fedha 2021/2022 uzalishaji wetu wa zao la mahindi lilikua ni tani milioni 6.8 leo tuna tani milioni 12 ni mara mbili na Tanzania sasa imeingia *among top three* za uzalishaji wa mahindi katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia katika kipindi cha miaka hii minne imechukua hatua za kumpunguzia mkulima mdogo mdogo gharama za uzalishaji. Serikali hii imeanzisha skimu kubwa ya ruzuku ya mbolea Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wote wanafahamu kwa kiwango gani tulilalamika kwa muda mrefu juu ya suala la wakulima wadogo kupunguziwa gharama za uzalishaji, ninaomba nizitaje skimu za ruzuku zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2021/2022 matumizi ya mbolea ya nchi hii yalikuwa ni tani 360,000, msimu wa mwaka wa fedha 2023/2024 matumizi ya mbolea yamefika tani 860,000 na wala hayajaongezeka kwa bahati mbaya, kwa sababu Serikali imetumia zaidi ya bilioni 700 ku-*support* skimu za kutoa ruzuku ya mbolea kwa kipindi cha miaka mitatu. Serikali hii haijaishia hapo, Serikali ilirudisha skimu ya kutoa pembejeo bure kwa zao la korosho, uzalishaji wa korosho ulianguka mpaka tani 180,000, msimu uliopita korosho imefika tani 526,000 na ruzuku iliyotolewa kwa kipindi cha miaka minne ina thamani ya shilingi bilioni 556. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba mwaka 2020 lilikuwa uzalishaji wake ni tani 120,000, mwaka huu nchi hii inaenda kuvunja rekodi kama ilivyovunja rekodi ya zao la korosho. Tunaenda kuzalisha

jumla ya tani 400,000 marobota zaidi ya 800,000 ambayo hatujawahi kuyapata toka nchi hii imepata uhuru na sababu ni moja Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia kwa miaka mitatu imewapa wakulima wa pamba ruzuku ya mbegu bure, viuatilifu bure, vinyunyuzi bure vyenye thamani ya shilingi bilioni 325. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 uzalishaji wetu wa tumbaku ulikuwa ni tani 56,000 na Tanzania ilikuwa katika kundi linaloitwa *others.* Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita hatumo tunaitwa na wengineo, sasa hivi mwaka huu soko linaloendelea uzalishaji wetu umefika tani 160,000 na Tanzania ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa tumbaku Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii haijaishia hapo ndani ya Bunge hili Waheshimiwa Wabunge mlisema sana juu ya kuhakikisha tunaanza kuchukua hatua ya *mechanizations,* ruzuku kwenye zana za kilimo. Si kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikihubiri na kuwaambia wakulima wadogo wenye heka mbili wanunue trekta la milioni 70, milioni 100 jambo ambalo haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia imeanza kutekeleza skimu kubwa ya ugawaji wa kutoa ruzuku za matrekta, jumla ya matrekta 10,000 na vituo 1,000 vimeanza kujengwa katika nchi hii, matrekta haya yako kwenye maeneo gani? Kwenye pamba, Serikali imegawa jumla ya matrekta 350 na wakulima wanalimiwa kwa bei ya ruzuku ya shilingi 35,000 kwa hekari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka niliseme kidogo ni eneo la utafiti na uzalishaji wa mbegu. Mwaka 2021 uzalishaji wetu wa mbegu wa ndani ulikuwa ni tani 35,000 leo nchi yetu inazalisha jumla ya tani 76,000. Kati ya kampuni zote 30 zinazouza mbegu nchi hii kwa mara ya kwanza tuna kampuni 24 za Watanzania, Serikali hii haijaishia hapo mashamba yote ya Serikali wamepewa *local companies* kwa ajili ya kuzalisha mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo la utafiti Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia, dunia sasa hivi teknolojia inabadilika, Bunge hili lilihoji sana juu ya suala la mbegu za asili, tayari Serikali

imeshasafisha jumla ya *variety* 330 na zimeshatangazwa na zimeanza kufanyiwa uzalishaji. Hata hivyo, hatujaishia hapo Serikali imeanza kujenga *GenBank* kwa ajili ya kuhifadhi mbegu zetu katika Taifa hili, haijaishia hapo Serikali imeanza kujenga *bioscience center* kubwa Afrika, inaanza kujengwa pale Morogoro na kwa nini Serikali inajenga *bioscience?* Hatuwezi kukimbia teknolojia hasa kwenye maeneo ya uzalishaji wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaishia hapo Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia inatoa ruzuku ya mbegu, inatoa ruzuku ya mbolea, inatoa ruzuku ya viuatilifu lakini wakulima wadogo wametengenezewa mfumo wa ruzuku kwenye kuuza mazao. *NFRA* uhifadhi kwa kipindi chote toka tunapata uhuru uwezo wetu wa kuhifadhi ulikuwa ni tani 250,000, sasa tumefika tani 770,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kununua mazao ya wakulima kwa bei ya ruzuku, kila mwaka mkulima wanapovuna mahindi bei huwa inaanguka 250 au 300, wakulima wa mahindi wanajua Serikali inaongeza bei 500 mpaka 700. Mwaka huu tumenunua kwa wastani wa shilingi 700 wakati soko lilikuwa limeanguka mpaka shilingi 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka niliongelee ni eneo la ugani. Maafisa Ugani kwenye historia ya nchi yetu wamekuwa wakilaumiwa kwa muda mrefu, lakini Serikali ya Dkt. Samia imechukua hatua gani? Hatua ya kwanza tuliwapatia vitendeakazi pikipiki 6,800 Maafisa Ugani Kilimo wote wana pikipiki sasa hivi. Hatua ya pili, Serikali imenunua vifaa vya kupimia afya ya udongo ambazo Halmashauri zote za uzalishaji wamepewa vifaa vya kupimia afya ya udongo na huduma hii ni ya bure kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya tatu Maafisa Kilimo wamenunuliwa magari 140 kwa jumla ili wapate vitendeakazi na waweze kuwatembelea na tayari magari yameshaanza kusambazwa katika baadhi ya maeneo. Serikali haijaishia hapo, imekamilisha mchakato wa kuanzisha Wakala wa Ugani wa Taifa na hilo lilikuwa ni kilio cha Bunge lako Tukufu na Watanzania katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni ushirika. Tunakumbuka sote suala la ushirika lilikuwa ni kilio na bado changamoto zipo, lakini Serikali imechukua hatua, tumezindua Benki ya Ushirika ya kwanza katika nchi yetu na Serikali imewekeza na benki hii imeanza ikiwa na matawi manne, lakini na mawakala 50 katika nchi yetu na mtaji wa bilioni 58. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatua ya pili kwa mara ya kwanza mikopo kwenye sekta ya kilimo imefikia trilioni nne katika nchi yetu, hii ni hatua kubwa sana katika mabadiliko yanayofanyika katika eneo hili. Uzalishaji wetu wa kahawa tumetoka tani 50,000, sasa tuko tani 85,000 na Serikali inagawa miche bure inawapelekea wakulima, parachichi sasa hivi nchi yetu ni wazalishaji wa tatu Afrika baada ya Kenya na South Africa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zote ambazo zimechukuliwa na Serikali ni kwa sababu ya hatua mbili tu, moja ni *political will,* lakini hatua ya pili ni Serikali kutoa *public fund* na kuwekeza. Nitumie Bunge lako Tukufu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, katika hatua hii, lakini niishukuru sana Wizara ya Fedha, ninamshukuru sana Mwigulu, ninamshukuru sana yeye na Naibu Waziri wake na wataalam wote wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa *flexible* hata kubadilisha *tax measures* sasa hivi wataona katika *finance bill* inayokuja *incentives* kwenye *cotton* tumetoa *incentives* kwenye *tobacco,* tunatoa *incentives* kwenye mafuta ya kula hizi zote ni hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kumhakikishia mkulima kuweza kupiga hatua inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona umewasha taa nimalizie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ehee malizia kilimo ni jambo kubwa sana…

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu la mwisho. Taifa letu liko *dominated* na *small holder farm,* wakulima wadogo. Wakulima wadogo hawawezi kupiga hatua na nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Kitila, *vision* itakayokuja hapa ime-

*accommodate* sana namna ya kumlinda mkulima mdogo na kumkuza, njia pekee ya kuweza kumwezesha mkulima mdogo ni hatua hizi zinazochukuliwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na huu ndiyo msingi wa chama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru Chama kwenye Ilani iliyopita na Ilani mpya tuliyoipitisha kuendelea kuipa sekta ya kilimo uimara na msisitizo mkubwa kwa ajili ya kuwaondoa Watanzania kwenye umaskini, tusipoelekea na mwelekeo huu hatuwezi kuwaondoa watu katika umaskini katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, nimshukuru Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Spika, Naibu Spika na Bunge lako Tukufu. Mwisho niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Nzega, *insha Allah* tarehe 28 tutakuwa wote tutakutana *field* ili tuweze kuendelea na siasa na demokrasia ya Chama chetu Cha Mapinduzi. Niishukuru Kamati ya Bajeti, sana ninamshukuru Mwenyekiti Njeza na Kamati nzima ya Bajeti kwa *engagement* inayoendelea ambayo tumekuwa nayo siku zote, ninawashukuru sana Wabunge kwa *support* ambayo wametupa leo tunaanza kutekeleza Mradi wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitangazie Bunge lako Tukufu. Ziwa Victoria na Lake Tanganyika usanifu umeshatangazwa, *tender* imeshafunguliwa. Sasa hivi wanamtafuta mshauri elekezi mradi huu utatekelezwa katika mikoa saba, wilaya 69, vijiji 900 kwa jumla ya hekta milioni tatu. Tumeshapata mkandarasi Bugwema, tumeshapata mkandarasi Rufiji *Basin* hekta 67,000, tumeshapata mkandarasi Mto Ngono ambayo imekuwa ni kilio cha muda mrefu cha Wabunge wa Ziwa wanaotoka Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, ahsante sana. Nilikuachiachia muda maana yake kilimo kweli ni jambo kubwa. Nilishamwita Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Waziri atafuatiwa na *Chief Whip.*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu, hoja ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka wa 2024 pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliotangulia kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa afya njema na kuendelea na mjadala ndani ya Bunge lako Tukufu. Nichukue nafasi hii pia kwa moyo wa dhati kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayofanya, lakini pia kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii nyeti ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nimhakikishie Mheshimiwa Rais kwamba na Watanzania kwamba nafasi hii nitatumia kwa manufaa mapana na makubwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa miongozo yao na maelekezo yao ambayo yamekuwa chachu kubwa katika utendaji kazi ndani ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nimpongeze pia Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa anayoifanya, umahiri wake, Naibu Spika pamoja na wewe Mwenyekiti na Wenyeviti wenzako kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan. Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ilikuwa shillingi bilioni 939 lakini hiyo bajeti inayoendelea mwaka huu wa fedha 2025/2026 ni trilioni 2.067 ni ambayo ni ongezeko la 120%. Ongezeko la bajeti hii limefanikiwa sana katika utendaji kazi kwenye Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*. Tunatambua kwamba Vitambulisho vya Taifa kwanza ni usalama wa nchi yetu, lakini pili ni hitaji kwenye

masuala ya uchumi na ya kijamii na Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka miaka miwili mitatu nyuma kulikuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa namba pamoja na Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Fedha wametupatia fedha shilingi bilioni 45.2. kwa kipindi cha Julai hadi Aprili mwaka huu 2025. Julai, 2024 hadi mwezi Aprili, 2025 jumla ya wananchi 844,994 walisajiliwa na kutambuliwa na kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 watu wenye umri wa miaka 14 na kuendelea ni milioni 31,582,976.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa, jumla ya wananchi wenye sifa waliosajiliwa na kutambuliwa ni wananchi milioni 25,854,970, lakini vitambulisho vilivyozalishwa mpaka sasa ni milioni 21,514,741 na vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa kwa wananchi ni milioni 21,191,588 kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ni kuanzishwa kwa suala zima la kusajili watoto wa miaka 18 na kurudi chini kwa maana ya kutoa jamii namba. Ninaomba nikuarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jambo hili linaanza na tunaanza majaribio katika Wilaya tatu, Wilaya ya kwanza ni Wilaya ya Kilolo iliyoko Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Rungwe iliyoko Mkoa wa Mbeya pamoja na Mkoa wa Kusini Unguja kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha unaokuja 2026/2027, sasa tunaanza kufanya kazi hii katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa upande wa Jeshi la Polisi, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mapinduzi makubwa sana jambo kubwa la kwanza kwanza ni kudumisha amani, utulivu na usalama katika nchi yetu, wameongea hapa Waheshimiwa Mawaziri kila Waziri aliyesimama ameelezea utekelezaji wa Ilani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii inafanikiwa kwa sababu kuna amani na utulivu katika nchi yetu na nitoe wito kwa Watanzania wote kila mmoja ajue kwamba suala zima la amani na utulivu ni suala la kila mmoja wetu na kila ahakikishe kwamba analifanya jambo hili ili miradi hii ya maendeleo iweze kutekelezeka ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeti, nilipongeze Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ambavyo vinaendelea kusimamia amani, utulivu katika Taifa letu. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya makosa ya jinai yaliyoripotiwa Polisi yalikuwa makosa 40,022, ukilinganisha na makosa ya 43,147 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, ambayo ni sawasawa na kupungua kwa asilimia 7.2. Hatua hii ni kubwa, kama ulivyosema kila Mtanzania ajue kwamba thamani ya usalama ya nchi hii uko mikononi mwetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vitendeakazi tunashukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita. Tumepokea magari zaidi ya 218, ninavyozungumza Makamishna wa Polisi, Naibu Makamishna, ma-*RPC* wetu na kubwa sana ma-*OCD* wetu nchi nzima sasa wamepokea magari mapya. Ifikapo mwezi Agosti mwaka huu ma-*OC CID* (Makamanda wa Upelelezi) wilaya zote nchini pia watapokea magari kwa ajili ya utendaji kazi na huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na magari ya Jeshi la Polisi, katika mwaka wa fedha huu unaoendelea ipo miradi ambayo imeshakamilika. Ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi katika mikoa mbalimbali nchini, imetumika shilingi bilioni 8.8 kwa ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja, Mtumba – Dodoma, Kanda Maalum ya Tarime - Rorya kule kwa Mheshimiwa Esther Matiko, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkoa wa Singida na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwezi huu wa Mei tumepelekewa shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kukamilisha Ofisi za Makamanda wa Polisi katika mikoa mingine kama Mikoa ya Geita, Simiyu, Manyara, Mtwara, Songwe pamoja na Kanda Maalum ya upande wa Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja pia ya Mheshimiwa Mbunge dada yangu Mwantumu Haji Dau ambaye alitaka kupata ufafanuzi lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi katika Mkoa wa Kusini Unguja. Ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika mwaka wa fedha uliopita 2024/2025 na mwaka wa fedha 2023/2024, tayari Serikali imetumia shilingi bilioni nne kwa ajili ya kukamilisha nyumba za Makazi ya Askari wetu katika maeneo mbalimbali nchini, upande wa Tanzania Bara na Zanzibar. Pia, tayari Serikali kupitia Jeshi la Polisi ilishapeleka shilingi milioni 291 kwa ajili ya kujenga nyumba nne ya Makazi ya Askari katika Mkoa wa Kusini Unguja eneo la Tunguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza, ninaomba nitoe taarifa kwamba utakumbuka kuwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 tulikuwa na msongamano mkubwa sana wa wafungwa wa mahabusu katika magereza yetu. Tulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 33,764. Kufika mwezi Aprili, 2025 tuna wafungwa na mahabusu 27,088. Hili ni sawasawa na kupungua kwa 20%. Haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Tume ya Haki Jinai na bado kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo mengine ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba magereza yote nchini yanatumia nishati safi ya kupikia. Ninaomba niwahakikishie Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sasa magereza yote 129 hapa nchini yanatumia nishati safi ya kupikia. Kwa maana hiyo imetekeleza agizo hili kwa 100% na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ni kwamba kati ya magereza 129, magereza 66 sasa yanatumia Mahakama mtandao na jambo hili lina manufaa makubwa. Moja, ni kwamba unaharakisha usikilizaji wa mashauri ya wafungwa na mahabusu; Pili, inapunguza gharama kwa Serikali ya kuwapeleka wafungwa kuwasafirisha katika maeneo ya mbali na kuwarudisha kwenye mahabusu; Tatu, kuokoa muda wa kusikiliza mashauri; Nne, upatikanaji wa haki kwa wakati; na tano, kuboresha hifadhi na kumbukumbu za mashauri ya wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mambo makubwa yamefanyika. Kwa sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa dola milioni 100 ambao kufikia Mwezi Mei mwaka huu tayari tumeshapokea magari 40 ya kubebea majeruhi kwenye majanga, magari 30 ya mawasiliano yanapotokea maeneo ya zimamoto na uokoaji, karakana sita za kuhamisha na zisizohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nikijibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani, tayari tunasubiri magari 150 ya zimamoto na uokoaji kwa ajili ya mikoa yote na wilaya zote nchini. Pia, tunasubiri *helicopter* moja, boti za kuzimia moto 22 kwenye Bahari na Maziwa Makuu hapa nchini. Haya ni mapinduzi makubwa sana kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na ndiyo maana tunasema ikifikapo Oktoba tuna-*tick* kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na vifaa hivi, ninavyozungumza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha shilingi bilioni 2.59 kwa ajili ya kujenga vituo saba katika Mikoa ifuatayo: Songwe, Simiyu, Manyara, Geita, Kagera, Njombe pamoja na Katavi. Haya ni mapinduzi makubwa na hivi ni vituo vikubwa vya zimamoto na uokoaji katika mikoa hii ambayo nimeitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Uhamiaji; mapinduzi makubwa yamefanyika. Kuanzia Julai 2024 hadi Aprili mwaka huu wageni walioingia nchini wanafika 1,800,000 ukilinganisha na wageni 511,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa iliyofanyika katika suala zima la kuhakikisha kwamba wageni wanaingia salama, wanakaa na kutoka salama hapa nchini kwa ajili ya mustakabali na usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nikushukuru wewe tena na Spika wetu kwa kazi kubwa inayofanyika. Pia, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuniamini na niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote

kuhakikisha changamoto mbalimbali zinazowakabili zinakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, mwisho kabisa nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Waheshimiwa Wabunge kila Mbunge akisimama hapa hakuna ambaye hana miradi kwenye Jimbo lake. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza sana na ifikapo Oktoba tuna jambo moja la ku-*tick* kwa ajili ya kuendeleza kazi hii kubwa iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Baran Sillo. Ninamwita sasa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutufikisha siku ya leo salama ikizingatiwa kuwa tunakaribia kuhitimisha Shughuli za Bunge letu Tukufu katika kipindi hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua katika kazi hii ya kumsaidia kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu nikiwasaidia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kazi kubwa ya uratibu wa Shughuli za Serikali, pia kama mshauri wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi cha Awamu hii ya Sita. Sote ni mashahidi wa mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali kama ambavyo wote tumewasikia Waheshimiwa Wabunge, hotuba nzima hii ya siku zote hizi karibu wiki nzima wamekuwa wakifafanua na wakieleza mambo mbalimbali ambayo yamefanywa na Serikali ya

Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii pia tumeshuhudia kuanzia asubuhi mpaka sasa Waheshimiwa Mawaziri mbalimbali na sekta zao tumewasikia wakiwa wanaeleza mafanikio makubwa sana yaliyopatikana kwenye sekta mbalimbali kwa miaka minne hii ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana wenzangu Waheshimiwa Mawaziri wa sekta mbalimbali waliosema maneno haya na utekelezaji mzuri wa kazi walizofanya. Pia, ninawapongeza watumishi mbalimbali, watendaji na viongozi wenzetu wa Serikali, mikoa na wilaya kwa kufanikisha kazi za utekelezaji wa Ilani, pamoja na maono na ndoto za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vilevile, Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanazozifanya za kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Mkutano Mkuu taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita zilipokelewa kwa kishindo na Waheshimiwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu walipokea kwa kishindo sana kazi hizi. Pia, matokeo ya Mkutano Mkuu umemteua Ndugu Dkt. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea Mwenza wa uchaguzi ujao. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza. Pia, tumempata Mheshimiwa Wasira kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama chetu Cha Mapinduzi; ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameyasema vizuri na wamesema yote. Waheshimiwa Mawaziri leo wamesema kwa

kujidai kabisa mafanikio lukuki ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumeshuhudia maendeleo makubwa katika maeneo yote ya huduma, uchumi, ulinzi na usalama. Siri kubwa ya mambo na mafanikio haya ni ubunifu, uwezo na utashi wa kisiasa katika kutekeleza jukumu hili na tumeshuhudia mapinduzi makubwa sana ya *style* ya utendaji kazi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuliozoea humu ndani tulikuwa tunajua bajeti za siku za nyuma Bunge likipitisha mafungu yote yanaenda kwa Mkurugenzi halafu wakati mwingine hatupo kwenye vikao vyao na wakati mwingine unakuta zimepangwa lakini kule wanapanga tena. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja na ubunifu mpya. Kama ni fedha za kujenga kituo cha afya zinakwenda kwenye kijiji ambacho kituo cha afya kinajengwa. Kama ni fedha za kujenga darasa zinaenda moja kwa moja kwenye Akaunti ya Kijiji chenye darasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunashuhudia Wabunge wote na sisi wote wawakilishi yale yote ambayo tumetumwa na tumesema, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametekeleza. Pia, tumeshuhudia wananchi wakituambia kule tunapokwenda kwamba yametekelezwa kwa sababu kwanza wameshududia pesa zimeingia na wameshiriki na ujenzi na mafanikio wanayaona. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ubunifu huo na ndiyo umetuwezesha sisi Waheshimiwa Wabunge humu kutoka kifua mbele kwa sababu ya kazi kubwa ambayo imefanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata mimi wa siku nyingi mambo yangu ambayo yalikuwa hayajafanyika miaka yote yamefanyika katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mradi wa Maji Ismani ndio unakamilishwa ambao haukuwepo. Barabara ya kwenda *Ruaha National Park* ndio inajengwa. Leo hii miradi ya maji ya umwagiliaji ambayo sikuwa nayo, mradi mkubwa kabisa umejengwa katika Jimbo la Ismani na hivi leo *RC* wangu Serukamba na *Mr.* Raymond (Mkurugenzi wa Umwagiliaji) wapo kwenye kata moja inaitwa Ilolo Mpya wanasaini Mradi mpya wa Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uwezeshaji katika sekta zote. Sekta za uchumi ukiacha suala la uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake, watu wasiojiweza na vijana amegusa pia makundi mbalimbali ya bodaboda na mama ntilie. Bodaboda wanaitwa Maafisa Usafirishaji siku hizi na mama ntilie na wote wale wengine. Hayo yote yamefanyika kwa kishindo na kila Mtanzania anashuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uratibu huu wa Shughuli za Serikali, ninaomba niseme kidogo juu ya mengine yafuatayo. Kwanza nizungumzie kidogo Bunge kwa maana ya kumpongeza zaidi sana, ninapaza sauti kama walivyopaza wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kazi kubwa aliyoifanya kipindi hiki cha Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza mafanikio ya Dkt. Samia humu ndani ya Bunge Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na yeye ametuwezesha katika mafanikio haya ya Bunge kwa sababu kazi ya Bunge ni kuisimamia Serikali. Mheshimiwa Dkt. Tulia ametuongoza vizuri, tumeisimamia Serikali ambayo imeweza ku-*deliver* na kutoa mafanikio haya makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Dkt. Tulia ninampongeza sana Mheshimiwa Rais aliyemteua kwanza kama Mweyekiti wa Chama kuja kugombea huo uspika wenyewe. Haikutosha hapo, Mheshimiwa Spika akamuunga mkono katika kugombea nafasi ile kubwa kabisa ambayo ameshinda amekuwa mwanamke wa kwanza au Mwafrika wa Kwanza kuwa kiongozi wa Bunge lile kubwa kabisa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa makubwa aliyosimamia ya kuisimamia Serikali na leo tunatoka kifua mbele tunajidai kwa kazi kubwa ambayo tumefanya. Niwapongeze sana Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu, Mwenyekiti na Wenyeviti wenzako kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia. Ninawapongeza sana Wenyeviti wa Kamati zote kwa kazi kubwa ambazo wamezifanya kwa ajili ya kusimamia haya. Pia,

ninawapongeza sana Katibu wa Bunge na Menejimenti yake kwa kufanya haya yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuratibu masuala ya siasa na kutekeleza wajibu wake katika Mhimili wa Bunge. Kwa upande wa shughuli za siasa Serikali imeendelea kutekeleza falsafa ya *4R* iliyoasisiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Falsafa ya *4R* ambazo ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga Upya imeendelea kutumika ipasavyo katika kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau mbalimbali wa kisiasa, kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia, na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili la 12, Ofisi ya Bunge imeendesha mikutano 19 mpaka sasa. Mpaka tarehe 20 Juni, 2025 jumla ya maswali ya msingi yaliyoulizwa na kujibiwa Bungeni ni 5,192. Maswali ya nyongeza ni 17,701 na maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni 248. Aidha, idadi ya Miswada iliyowasilishwa na Serikali na kisha ikapitishwa na Bunge lako Tukufu ni 63 ikiwemo Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uipande wa idadi ya Maazimio *(Declarations)* na Itifaki za Kimataifa zilizowasilishwa na kuridhiwa na Bunge ni 16. Pia, yamo Maazimio 922 yaliyoazimiwa na Waheshimiwa Wabunge kutokana na taarifa mbalimbali za Kamati au masuala mahususi kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nizungumzie kidogo juu ya Ujenzi wa Mji wa Serikali (Mtumba). Wote tunajua kwamba Mheshimiwa Rais anapoingia madarakani alikuta majengo ya muda ambayo sisi tulianza nayo, majengo 23. Ameendelea na ujenzi wa majengo ya kudumu mapya 34 ya Ofisi za Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali (Mtumba), Awamu ya Pili iliyoanza Mwaka wa Fedha 2020/2021 ikilinganishwa na majengo 23 ya muda mfupi yaliyojengwa

na kukamilika katika Awamu ya Kwanza ya ujenzi iliyoishia mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Awamu ya Pili unaendelea ambapo hadi Juni, 2025 wastani wa ukamilishaji wa majengo yote hayo yaliyoanza kujengwa 34 umefikia 90.1% na yote yanajengwa kwa fedha zinazokusanywa zinazolipwa na walipakodi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; kukamilisha ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 59.1 katika Mji wa Serikali ambazo mwaka 2021 zilikuwa katika hatua za awali za ujenzi. Vilevile, kukamilisha upembuzi yakinifu wa barabara inayounganisha Mji wa Serikali na Ikulu yenye urefu wa kilometa 9.9. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kudumu ikiwemo umeme ambao umefikia 55%, mitandao ya mawasiliano, mifumo ya *camera CCTV* ambao umefikia 47%. Kazi hizi hazikuwa zimeanza kabla ya mwaka 2020. Kukamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa ambao kwa mwaka 2020 Serikali haikuwa imeanza kuujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kengele imegonga, lakini ninataka nirudie tena shukrani zangu za dhati pamoja na kwamba sijagusia mambo mengine yaliyotekelezwa kutoka kwenye ofisi yetu, lakini ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali katika hotuba yake atakayoitoa kabla ya Bunge hili atagusia maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwetu sisi kuturahisishia kazi za wananchi walizotutuma kama Mbunge mmoja mmoja. Pia, kwa usimamizi na utekelezaji mzuri wa Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana wenye hoja yao leo ambao tunaiunga mkono Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa hotuba yao ambayo inatufungia Bunge hili na kila mmoja ameisifu sana. Ni hotuba nzuri na

ya uwezeshaji inayotupeleka katika ushindi katika uchaguzi ujao wa Mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, lakini na kuwatakia kila la kheri. Ninamtakia kila la kheri Mheshimiwa Spika ambaye anaenda kuwa Mbunge mpya wa Jimbo la Uyole. Historia inaanza upya, anakuwa Mbunge mpya wa Jimbo la Uyole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waheshimiwa Wabunge wengi ninajua wengi kama siyo wote tunakwenda kugombea na wale wakinamama wanaokwenda kugombea Viti Maalum na vya makundi mbalimbali, tumwombe Mwenyezi Mungu atubariki sote tuweze kutimiza jukumu hili tunalolipenda sana na tumalize salama na *insha Allah* Mwenyezi Mungu ataturejesha kwenye viti vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza sana, ninajua mpaka sasa huna mgombea kule Njombe, ninakupongeza uendelee hivyo hivyo, ninajua Mungu atakurejesha katika kiti chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya, ninaomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Chief Whip,* Mheshimiwa William Lukuvi kwa maneno hayo uliyoyasema na hasa ya kule Njombe.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli yetu ya leo kadri ya *Order Paper* na wachangiaji. Ni kukumbushana tu kwamba kesho ndiyo siku yetu kwa mujibu wa Kanuni ya 126(2) ni siku ya maamuzi kama alivyosema Mheshimiwa Spika asubuhi. Ni muhimu sana kwamba wote tuwe hapa siku ya kesho kwa ajili ya kazi hiyo ambayo ipo mbele yetu.

Sina tangazo lingine, lakini niseme kwamba hoja hii itahitimishwa kesho na tutakuwa na wachangiaji wawili watakaomalizia ambao ni Naibu Mawaziri halafu watoa hoja watakuja kumalizia hoja zao.

Baada ya kusema hayo, niwatakie jioni njema na niahirishe Bunge mpaka kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.41 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 24 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*